JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA PILI

Kikao cha Tatu – Tarehe 28 Januari, 2016

(Kikao Kilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wetu wa Pili, lakini leo ni Kikao cha Tatu. Katibu!

DKT. THOMAS D. KASHILILLAH – KATIBU WA BUNGE: Maswali kwa Waziri Mkuu.

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

SPIKA: Maswali kwa Waziri Mkuu, kama ilivyo ada swali la kwanza linaulizwa na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Mbowe!

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kumuuliza Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, wewe ukiwa kama Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni na wewe ukiwa kama mwanasiasa mzoefu, nina hakika unatambua kwamba ujenzi wa demokrasia ni gharama na ni mchakato wa muda mrefu. Nina hakika utakuwa utajua vilevile kwamba nchi yetu imepiga hatua kubwa katika kujenga jamii inayoheshimu demokrasia, inayoheshimu Sheria na inayoheshimu Katiba ya nchi. Katika muda mfupi tangu Serikali ya Awamu ya Tano imeingia madarakani, yapo mambo matano makubwa yaliyotokea ambayo yanaashiria, aidha Serikali hiyo haiheshimu kukua kwa demokrasia katika Taifa ama pengine ina dhamira ya kuondoa lengo kubwa hilo lililowekwa na Katiba ya Taifa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, mambo hayo ni pamoja na baada tu ya uchaguzi wa mwaka 2015, Jeshi la Polisi limeweka makatazo nchi nzima kwa Vyama vya Siasa kufanya kutokufanya kazi zake za kisiasa, haki ambayo ni haki ya kikatiba.

Leo tayari ni miezi mitatu na siku tatu katazo hilo linaendelea na katazo hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu ulilliunga mkono na kulisisitiza katika mkutano wako uliofanywa katika Jimbo lako la Ruangwa, kwamba wenye haki ya kufanya ni wale walioshinda, lakini Vyama vya Siasa haviendelei kuruhusiwa kufanya kazi hiyo ya siasa. *(Makofi)*

Swali langu sehemu (a) ni kama ifuatavyo; Mheshimiwa Waziri Mkuu unataka kuithibitishia Bunge hili, nchi hii na dunia hii, kwamba wewe kama Kiongozi Mkuu wa Serikali una kusudio la kuendelea kuzuia Vyama vya Siasa kufanya kazi zake za kisiasa ambayo ni haki yao ya Kikatiba? Hilo ni swali la kwanza. *(Makofi)*

Swali la pili, Mheshimiwa Waziri Mkuu, tukiendelea hapo hapo unatambua vilevile kwamba urushaji wa matangazo ya moja kwa moja ni haki ya Kikatiba ya wananchi kupata taarifa na Shirika la Habari la Taifa ni shirika la umma, lakini ndani ya Bunge kuna taarifa zilizo rasmi kabisa kwamba Serikali yako imetoa kauli hapa kuzuia urushaji huo wa matangazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na uzuiaji wa urushaji huo wa matangazo kumeendelea kuwepo matumizi makubwa ya majeshi yetu kuanzia Zanzibar hadi hapa na Zanzibar katika kupinga matokeo ya uchaguzi wa Zanzibar ambao ulikuwa ni uamuzi wa wananchi?

Mheshimiwa Waziri Mkuu unaiambia nini dunia kwamba Awamu yako ya Tano sasa imekubali kuwa na utawala wa kijeshi kwa mgongo wa utawala wa kidemokrasia? *(Makofi)*

SPIKA: Kabla ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kujibu kuna Mbunge kajitokea huko, nafikiri mmemwona wote, akapita mbele ya Mheshimiwa Mbowe akiongea, basi nimemvumilia tu kwa sababu ya ugeni na nini, lakini tusome Kanuni tuzielewe, hupiti mbele ya Mbunge anayeongea na Spika, hukatizi katikati yao, Kanuni zinakataa, naomba tu-*observe* Kanuni.

Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu!

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, kwanza niseme namshukuru sana Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwa maswali yake mawili ambayo yanahitaji ufafanuzi na Watanzania waweze kujua, kwamba uongozi huu wa Awamu ya

Tano ni uongozi ambao unaongoza kwa kufuata demokrasia, kanuni, sheria na taratibu kadri ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo mambo yanajitokeza na tunapojaribu kutoa maelekezo ya kimsingi ya kuweza kufuatilia na kwa sababu ya utaratibu wa mazoea tu yanaweza kutafasiriwa vinginevyo. Suala lako la makatazo ya Vyama vya Siasa kufanya mikutano, ni jambo ambalo naweza kusema msemaji wa kwanza kabisa hakutumia nafasi yake ya uandishi kuandika kwa mfululizo kwa sababu ni mimi ndiye ambaye nilikuwa nimefanya ziara kwenye Jimbo langu kusalimia wapiga kura wangu.

Mimi ni Mbunge kama nyie na ninapokuwa Ruangwa sivai koti la Waziri Mkuu bali nakuwa Mbunge nazungumza na watu wangu. Nimekuwa na vikao mbalimbali vya makundi mbalimbali nikiwashukuru binafsi kwenye Jimbo langu ambako najua tuna utamaduni wetu. Nimepita pia kwenye Kata ambazo pia Madiwani wetu ni wa Vyama vya Upinzani, lakini tumeweka msimamo wa vyama vyote katika Jimbo lile kwamba lazima sasa tufanye kazi za maendeleo kwenye Jimbo letu.

Mheshimiwa Spika, kama mwandishi yule angeweza kuweka mtiririko wa ziara zangu na matamko yetu ndani ya Wilaya yangu kwa Jimbo langu, angeweza kunitendea haki, kwa sababu nilichotamka mimi kilifuatiwa na kauli zilizotamkwa na Madiwani kwenye Kata ambako nimetembela wakiwemo wa upinzani, ambao walisisitiza na kutoa msimamo kwamba sasa Jimbo hili tunataka tufanye kazi suala la siasa tunaliweka pembeni na tunaondoa tofauti zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya yanazungumzwa na Madiwani wenzangu wa vyama vingine. Kwa hiyo, ni jambo jema wanapolitamka kwa wananchi kwa maana ya kuweka msimamo wa maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtiririko ule tulizungumza pia na Baraza la Madiwani, nimezungumza na wafanyakazi wa Halmshauri, nimezungumza na Baraza la Wazee, nimezungumza na akinamama na pia nikazungumza na Jeshi la Polisi, wale ni sehemu ya raia walioko kwenye Jimbo langu. Mimi nimefanya kazi nyingi kwao na wao wamefanya kazi nyingi sana kwangu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kauli yangu ilikuwa inatokana na mazingira yale, kama mwandishi angeamua kufanya kazi yake vizuri kwa kueleza shughuli zangu hata nilipotamka kwamba kuanzia sasa sisi tumeamua tufanye kazi, bila kuzingatia itikadi za vyama vyetu na kwamba sasa mambo ya siasa tuache pembeni. Wale wote ambao sasa wangetakiwa kupita kwenye maeneo ya walioshinda ni wale tu ambao wameshinda kwenye maeneo yao. Kwa hiyo

jambo lile kama lingekuwa limeelezwa, limeripotiwa kwa mtiririko ule wala lisingeweza kuleta tafsiri ambayo imekuja kutolewa.

Mheshimiwa Spika, najua utawala wa sheria, najua Vyama vya Siasa vina haki yake, najua nchi inatambua kwamba chama cha siasa kinaweza kufanya mkutano. Pia kama msingi ule wa kauli ya Wanajimbo wa Ruangwa unaweza kufuatwa na watu wengine unaweza kuwaletea tija pia.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo niliyosema, niseme tu kwamba, jambo lile lilitokana na mazingira ninamoishi na sikulitamka kama Waziri Mkuu, nilitamka kama Mbunge wa Jimbo na lilitokana na matamko ya sisi wawakilishi wa Vyama vya Siasa kutoka kwenye Jimbo lile Mheshimiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni lile ambalo Mheshimiwa ametaka kujua suala la kauli ya Serikali juu ya TBC kuacha kutangaza siku nzima na badala yake watatangaza vipindi vya maswali na majibu, lakini baada ya hapo wataendelea na shughuli zao na huku waki-*record* ili waweze kututangazia baadaye.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo amelifafanua vizuri sana jana kwenye kipindi maalum na naamini Watanzania wametuelewa. TBC haijaacha kutangaza, walichofanya ni kubadilisha ratiba. Matangazo ya Bunge yataendelea kutangazwa, lakini tumebadilisha muda, badala ya muda ule ambao wao wangeweza kufanya matangazo ya kibiashara na matangazo mengine, suala la Bunge waandishi wao wako, TBC ina wawakilishi Dodoma, watafanya *recording,* halafu baadaye watatafuta muda mzuri ambao pia tunaamini Watanzania wengi watapata muda mzuri wa kuweza kuyasikiliza matangazo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huo ni mpango wa Taasisi yenyewe wa ndani, unaotokana na kazi wanazozifanya, wanajua matatizo na faida wanazozipata ndani ya Taasisi. Kwa hiyo, wanapoishauri Wizara, wanapoieleza Wizara na kwa kuwa walishaanza kutekeleza na Watanzania waliona mkatiko wa matangazo, lakini pia kulikuwa na mwongozo ulitolewa hapa. Kwa hiyo, tukasema jambo hili ni lazima sasa tulieleze kesho yaani lazima kuwe na kauli ya Serikali kwa Watanzania kwa sababu Mwongozo ulitolewa na mmoja kati ya Wabunge wetu anataka kujua kwa nini kuna mkatiko wa matangazo. Kwa hiyo, ndivyo ilivyokuwa na huo nadhani ni msimamo wa TBC na ndiyo msimamo wa Serikali.

SPIKA: Tunaendelea na Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani swali la nyongeza!

MBUNGE FULANI: La majeshi bado.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa ametaka pia kujua matumizi ya Majeshi. Majeshi yetu yapo kwa malengo kwamba lengo kuu ni kutunza amani na utulivu ndani ya nchi. Wajibu wao mkubwa ni kuhakikisha kwamba watu kwa maana ya Watanzania kwa Majeshi ya Tanzania, wajibu wake ni kuhakikisha kwamba watu wetu wanafanya shughuli zao kwa amani na utulivu na wako nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jukumu lao ni kumlinda Mtanzania popote alipo bila ya kukiuka misingi ya jambo ambalo anatakiwa kulifanya wakati huo. Wapo Zanzibar, wapo pia Tanzania Bara na wote hao kazi yao na jukumu lao ni lilelile. Sasa wanaweza kulazimika kutumia nguvu pale ambapo wanaona utaratibu uliowekwa eneo hilo unakiukwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo ndiyo kazi ya Jeshi la Polisi, kwamba wataendelea kutunza amani ili Watanzania waliokuwa kwenye eneo hilo kila mmoja afanye shughuli yake. Kila mahali kuna utaratibu wake na kila mahali kuna msingi wake na tunatarajia katika eneo, wote walio kwenye hapo, wanaofanya jambo hilo, wafanye jambo hilo kwa msingi unaofanana, usiokiuka taratibu za eneo hilo.

Kwa hiyo, Jeshi la Polisi lipo na litaendelea kufanya kazi yake kwa uaminifu, kwa uadilifu na naomba sana tuwasaidie Jeshi la Polisi kufanya kazi yao bila ya usumbufu ili wasionekane wanafanya kazi nje ya utaratibu wao. Hilo ndiyo jibu la msingi. *(Makofi)*

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Nakushukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majibu yako, lakini ningependa kuuliza maswali ya ziada kama ifuatavyo:-

Kauli yako Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba katika Jimbo lako la uchaguzi mmekubaliana muache siasa mfanye kazi, niliomba tu utambue kwamba siasa vilevile ni kazi. Vilevile kwa sababu kauli ya Waziri Mkuu ni agizo bila kujali umeitolea Jimboni kwako ama nyumbani kwako Mheshimiwa Waziri Mkuu, kauli yako unapoitoa mahali popote kama Kiongozi Mkuu ni agizo. Sasa kwa sababu Mahakama Kuu Mwanza wakati ikisikiliza kesi ya Alphonce Mawazo ilitoa hukumu kwamba Jeshi la Polisi halina mamlaka ya kisheria ya kuzuia mikutano ya Vyama vya Siasa yakiwemo maandamano kwa kisingizio cha...

Mheshimiwa Spika, narudia hapo kwa kisingizio cha wana taarifa za kiintelijensia na Mahakama Kuu ikaagiza Jeshi la Polisi kama mna taarifa za kiintelijensia ina maana mna msingi mzuri wa kulinda usalama. *(Makofi)*

Kwa hiyo *solution* siyo katazo, *solution* ni Jeshi la Polisi kuwasiliana na wahusika ili waweze kuwalinda vizuri kwa sababu tayari wana taarifa za uvunjifu wa amani.

Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu uko tayari sasa kutoa tamko kwa Taifa na kwa kupitia Bunge hili, kwamba lile katazo la mikutano ya siasa ya vyama vya siasa, sasa unalisitisha rasmi?

La pili hapo hapo, je, kwa kutoa tamko lile vilevile uko tayari tena kulieleza Jeshi la Polisi, liheshimu mhimili wa tatu ambao ni Mahakama ambayo ime-*declare* kwamba hawana mamlaka ya kutoa katazo wakati wanapopata taarifa za kiintelijensia?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa maswali mawili ya nyongeza ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Mbowe. Kama ambavyo nimeeleza awali kwamba Katiba inaeleza, lakini Sheria ndiyo inayoongoza nchi hii kuweka miongozo ya utaratibu. Siasa nchi hii haijaanza leo, upo utaratibu na zipo taratibu za kimsingi, kama chama kinahitaji kufanya mikutano lazima wafuate utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la Mahakama kuzuia Jeshi la Polisi kufanya kazi, hii ni mihimili miwili tofauti, Mahakama siwezi kuzungumzia habari za mhimili mwingine na kuutolea kauli. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Wauliza maswali wengine kwa Waziri Mkuu, jumla wako ishirini na nne na tumebakia na robo saa. Kwa hiyo, nitawachukua baadhi, wachache sana. Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso ni zamu yako!

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kuuliza swali kwako Mikoa ya Kanda ya Magharibi, Mkoa wa Rukwa, Katavi, Tabora na Kigoma, ni Mikoa pekee ambayo hayaijaunganishwa barabara kwa kiwango cha lami. Mikoa hii inazalisha chakula kwa wingi, kwa bahati mbaya bado miundombinu iko duni na kuwafanya wananchi wa mikoa hii kudumaa kiuchumi.

Je, Serikali ina mpango gani ya kuunganisha hii mikoa ili iweze kupata barabara za lami, kwa maana ya barabara kutoka Sumbawanga kuja Mpanda, barabara kutoka Mpanda kwenda Kigoma, barabara kutoka Mpanda kupitia Wilaya ya Mlele-Sikonge kwenda Tabora, halikadhalika kumalizia barabara ya Tabora kwenda Kigoma. Serikali ina mpango gani

kuwasaidia wananchi wa Mikoa hii ambayo walisahaulika kwa kipindi kirefu toka uhuru? *(Makofi)*

Naomba kupata majibu ya Serikali juu ya umuhimu wa kuimarisha miundombinu ya kujenga barabara kwa kiwango cha lami na ukizingatia Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, amewaahidi wananchi hao na mkoa wake wa kwanza wakati wa harakati za kuomba kura za Urais alianzia Mkoa wa Katavi na kutoa ahadi nzito, Serikali ina dhamira ipi ya kukamilisha miundombinu hiyo? *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Kakoso, Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu ya swali hilo!

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Kakoso, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mkoa ule hatujamudu kuunganisha maeneo yote na mikoa yote ya jirani. Hata hivyo, Mheshimiwa Mbunge anajua jitihada ambazo Serikali hii inafanya sasa za kuimarisha miundombinu na hasa barabara kwa miradi tuliyonayo nchi nzima, yenye malengo ya kuunganisha mikoa yetu tuliyonayo. Tayari ipo miradi inaendelea Mkoani Katavi ya kuunganisha na mikoa ya jirani, ikiwemo Katavi kwenda Mbeya. Pia upo mpango wa ujenzi wa barabara kutoka Katavi kupitia Sikonge mpaka Tabora na tunaimarisha barabara kutoka Katavi kwenda Kigoma kupitia Uvinza na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, miradi hii ambayo sasa inatekelezwa nchi nzima, inawezekana yako maeneo ambayo tumeanza na mengine tunaendelea, lakini mengine yapo kwenye mpango wa uendelezaji. Kwa hiyo, nataka nimpe imani na hii niwaambie wananchi wote walioko mikoa ile kwamba Serikali inayo nia ya dhati ya kuhakikisha kwamba tunaunganisha mikoa yetu yote kwa barabara za kiwango cha lami. Kazi tunayoifanya sasa ni kuhakikisha tu kwamba, tunatenga fedha kwa barabara ambazo zinaendelea, lakini zile ambazo hatujaanza kabisa, tunapeleka wataalam kwa ajili ya upembuzi yakinifu ili tuanze michoro na kazi hiyo tuweze kuanza. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tutaendelea pia kushirikiana na wananchi wa Mkoa wa Katavi kuhakikisha kwamba barabara zao zote tunaziunganisha, kama ambavyo sasa tunaendelea kuunganisha mikoa mingine kama Mkoa wa Dodoma na Manyara, Dodoma na Iringa, Dodoma tumeshaanza kwenda Singida sasa tunakwenda Tabora kupitia Manyoni. Kwa hiyo jitihada hizi ni za nchi nzima na wote ni mashahidi kwamba kazi hizi zinaendelea vizuri.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kazi hiyo inaendelea na Katavi pia watanufaika pia na mpango wa Kitaifa wa kuunganisha mikoa yetu.

SPIKA: Mheshimiwa Kakoso umeridhika?

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Spika, nishukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, swali langu la nyongeza; kwa kuwa mvua zinazoendelea kunyesha katika mikoa hiyo ni nyingi na zimeharibu miundombinu. Serikali ina mpango upi wa dharura kuhakikisha mikoa hii inapata huduma ili katika kipindi inapojipanga waweze kupeleka huduma itakayosaidia kutatua matatizo ya barabara ambazo zimeharibika sana? *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Kakoso, Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu!

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Kakoso, ni shahidi kwamba juzi tulipata taarifa kutoka Katavi, kwamba barabara zetu kule zimekatika kutokana na mvua nyingi. Hakuna mawasiliano sasa ya kutoka Mpanda, kwenda Tabora kupitia Sikonge, hakuna mawasiliano kutoka Mpanda kwenda Kigoma kupitia Uvinza, hata tuta la reli nalo limetetereka.

Mheshimiwa Spika, tulichofanya juzi tumechukua hatua za haraka na Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano amefanya kazi hiyo vizuri, amepeleka Wataalam, hapa ninapozungumza wataalam wapo pale wanaimarisha barabara ile, ili kuweza kurudisha mawasiliano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kuwa mvua zinaendelea tumeamua tutafute njia nzuri, ambayo itakuwa na uhakika wa kuunganisha mawasiliano kati ya Mpanda na mikoa ile pamoja na Tabora kwa kurudisha reli, njia ya treni kutoka Dodoma itakwenda Tabora - Kaliua ili iweze kwenda Mpanda. Ile sehemu ya tuta ambalo lilikuwa limeharibika tumeshakamilisha na tayari tumeliambia Shirika la Reli, wauze tiketi Dar es Salaam, abiria wote wanaokwenda Mpanda wapewe mabasi waletwe Dodoma kupanda treni inayokwenda Mpanda.

Mheshimiwa Spika, hiyo ndio njia ambayo tumeamua tuitumie sasa ili kuimarisha usafiri wa kwenda Mpanda; huku *Tanroad* wakiendelea na ukarabati wa barabara zote ambazo zimekatika na malengo yetu barabara hizo tuziimarishe ili ziweze kupitika wakati wote.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Swali linalofuata litaulizwa na Mheshimiwa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala. Mheshimiwa Zungu!

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Waziri Mkuu, nami nichukue nafasi hii kukupongeza wewe na Serikali yako kwa kazi nzuri mnayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, viwango vya *VAT* sasa hivi Tanzania ni 18% na viwango hivi havitofautishi biashara, kati ya katikati, kubwa na za chini. Je, Serikali haioni sasa ikipunguza viwango vya *VAT* kwa biashara za chini, *compliance* ya watu wa biashara za chini, wengi wataweza kulipa *VAT* hii kwa kiwango cha chini na kuiongezea mapato Serikali kwa kiwango kikubwa sana. Naomba kujua kama Serikali inaweza ikapokea ushauri huu na kulifanyia kazi na kuhakikisha kila mtu alipe *VAT* kwa kiwango cha shughuli ya biashara anayofanya.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukienda *Super Market* sasa hivi ukinunua chochote, unalipa 18%. Kwa hiyo, inaongezea mzigo kwa wale wachache ambao wanalipa kodi hii, lakini kodi hii ikishushwa kwa viwango, 18, 14, 10 na labda na tano itafanya *compliance* ya wananchi wote ambao wanafanya biashara waweze kulipa kodi hii na Serikali kujiongezea mapato. Naomba majibu yako Mheshimiwa Waziri Mkuu.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu!

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala, kama ifuatavyo:-

Swali hili, pia nimewahi kupata bahati ya kukaa na wafanyabiashara wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa lengo la kuwatia moyo wa kufanya biashara zao zaidi.

Moja kati ya mambo ambayo yalijitokeza kwenye vikao vile ni mjadala ambao leo umeuliza swali linalofanana sana kama ambavyo walikuwa wameomba. Pia tuliweza kuwaeleza wafanyabiashara na naomba nijibu swali lako kama ambavyo tuliweza kujibu, kwamba, *VAT* ya 18% mara nyingi huwa inatozwa kwa wafanyabiashara wanaofanya biashara kuanzia milioni arobani na kuendelea kwa mwaka au wanaopata pato la milioni kumi ndani ya miezi mitatu na miezi minne. Chini ya hapo hawausiki na *VAT*.

Mbili, kuruhusu biashara zote za aina zote zile kutoza 18%, kuna matatizo mengi. Moja, ni ngumu sana kumwacha Afisa wetu wa *TRA* kwenda kutoza *VAT* kulingana na biashara aliyonayo hasa kwa sababu ni ngumu pia kiutawala katika kutambua thamani ya jambo hilo, halafu pia, menejimenti yake inakuwa ngumu sana.

Mheshimiwa Spika, pia unaweza kutengeneza mianya ya rushwa ya wale watendaji wetu wanapofanyakazi ya kufanya tathimini ya biashara hizi za aina mbalimbali, lakini unapoweka 18%, wewe unaangalia tu pato lake la jumla kwa mwaka au kwa miezi mitatu, unafanya *calculation* ya 18%, kuliko kuanza kupitia biashara yenyewe ukubwa wake, unapata shilingi ngapi kwa mwezi, inakuwa ngumu sana.

Kwa hiyo, tumefanya *study* maeneo mengi na nchi mbalimbali tumegundua kwamba, njia nzuri ni ya kuweka *flat rate,* kwa biashara hasa kuanzia ile milioni arobaini kwa mwaka na milioni kumi kwa miezi mitatu, minne; inakuwa rahisi zaidi, hata menejimenti yake pia inakuwa ni nzuri.

Kwa hiyo, tumegundua kwamba jambo hili linaweza likasumbua hata wafanyabiashara, linaweza likawasumbua pia hata watendaji wetu wa *TRA*. Kwa hiyo, tunaendelea kukutana na wafanyabiashara, kupeana mawazo zaidi, lakini jambo hili sasa linahitaji utafiti wa kina, tutakapokuja kufanikiwa, tunaweza pia tukalitambulisha, lakini kwa kuwa tumejifunza pia na nchi za jirani jambo hili lina matatizo haya ambayo nimeyaeleza.

SPIKA: Mheshimiwa Zungu swali la nyongeza!

MHE. MUSSA AZZAN ZUNGU: Mheshimiwa Waziri Mkuu nakushukuru kwa jibu lako, lakini bado niko hapo hapo.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, nchi jirani moja hapa katika hizi za Afrika Mashariki, *informal sector* watu hawa wa madaladala, vinyozi, *welders* na kazi za kawaida ambazo siyo rasmi, wamewekwa katika viwango hivyo na wameweza kuchangia kwenye pato la Serikali trilioni nane mwaka 2009.

Hoja yangu ni kwamba, najua changamoto ambazo zipo kwenye Idara za *TRA* na zingine, basi Serikali ijaribu tu kulipitia na kutazama kwa sababu trilioni nane, kwa *informal sector* ni sawasawa na kiwango ambacho *TRA* ndiyo ilikuwa inakusanya miaka minne, mitano iliyopita.

Kwa hiyo, naomba tu Mheshimiwa Waziri Mkuu, mlitazame na mlifikirie kwa siku zinazokuja kama Serikali itaona upo umuhimu wa kuongeza mapato yake, *informal sector* nayo iweze kulipa *VAT* na Serikali ipate mapato yake. Nakushukuru.

SPIKA: Ahsante. Ameleta ombi tu Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu ya ombi lake!

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Azzan Zungu Mbunge wa Ilala, kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa ametoa ombi na kwenye jibu langu la msingi nimesema, bado tunaendelea kukaa pamoja na wadau wetu; ambao ni wafanyabiashara wakiwemo na hao wa *informal sector*. Kwa hiyo, kadri tutakavyokuwa tunakutana, tunabadilishana mawazo, tunaweza pia kuboresha mfumo mzuri wa ukusanyaji wa mapato, tukitambua pia kwamba, sekta hiyo nayo ina mchango mkubwa sana kwenye pato la Serikali.

SPIKA: Ahsante. Swali la mwisho kwa siku ya leo inabidi niwape *CUF*, Mheshimiwa Mohamed Kuchauka, hayupo, haya Mheshimiwa Gekul.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nimuulize swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, hivi karibuni Serikali imetoa Waraka katika Halmashauri zetu kuhusu elimu bure na Waraka wenyewe ni wa tarehe 6 Januari, 2016.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waraka huu umezua sintofahamu katika sehemu ya chakula cha wanafunzi katika shule zetu. Mfano, Waraka huu unasema kwamba wanafunzi wanaosoma *day* wazazi walipe chakula, lakini wanafunzi wanaosoma shule za bweni ambao wazazi wao wana uwezo hata wameweza kuwafikisha katika shule hizo, hawatakiwi kulipa hata chakula, Serikali itapeleka chakula.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali inasemaje katika hali hii ambayo imezua mtafaruku kwa wazazi kuona kwamba wamebaguliwa wale ambao hawana uwezo na Serikali imewaongezea uwezo wale ambao kidogo wana uwezo?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu kwa kifupi!

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pauline Philip Gekul, Mbunge wa Jimbo la Babati Mjini kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba ipo mikanganyiko imejitokeza sana hasa baada ya kuwa tumeanza kutekeleza mfumo wa elimu bure. Hata hivyo, nataka niwajulishe Watanzania wote maeneo ambayo Serikali imejikita, kuwa ni ya bure.

Moja, kwa upande wa sekondari, tulikuwa na ada ya shilingi 20,000/= kwa mwaka kwa shule za kutwa, eneo hilo sasa hawatalipa. Eneo la sekondari za bweni, wazazi walikuwa wanalipa shilingi 70,000/= kwa mwaka eneo hilo

halilipiwi, ni bure. Eneo la tatu, kwa shule za msingi na sekondari mitihani yote ya darasa la nne na kidato cha pili, iliyokuwa inafanywa kwa wanafunzi kuchangia, eneo hilo sasa wanafunzi hawatachangia. Serikali itatenga fedha kwa ajili ya mitihani hiyo ya kidato cha pili na darasa la nne, watafanya bure.

Mheshimiwa Spika, eneo la lingine kwa shule za sekondari za bweni ambazo wanakula chakula tunaendelea na utaratibu wa kuwalipia, kuwagharamia. Sasa mkanganyiko unaojitokeza kwa uelewa wangu, Mheshimiwa Mbunge na Watanzania wote, ni pale ambako zipo shule za kutwa, ambazo kisera shule za kutwa, ni za mtoto anatoka nyumbani anaenda shuleni, anasoma anarudi kula nyumbani. Hizi sasa ndiyo ambazo zimeleta mkanganyiko hasa kwa wazazi ambao walikuwa wamejiwekea mpango wao, wao wenyewe ili kuweza kuwafanya vijana wetu waweze kupata lishe shuleni.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili nikiri kwamba pamoja na mkanganyiko ikiwemo na hili, Wizara sasa inaandaa utaratibu mzuri wa maelezo mazuri ya namna tutakavyotekeleza kwenye eneo hili halafu tutatoa taarifa, kwa sababu ndiyo tumeanza kutekeleza mwezi Januari, hizi changamoto zimeanza kujitokeza, yako maeneo mengine wanaendelea kuchangisha. Kwa hiyo, tunataka tutoe Waraka ambao sasa utaweka wazi kila kitu na Waheshimiwa Wabunge, tutawaletea nakala ili mtusaidie katika kuratibu jambo hili. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, muda wetu ni nusu saa na nusu saa imeshapita. Tunakushukuru sana kwa majibu mazuri ya ufasaha. Tutaendelea tena Alhamisi ijayo. *(Makofi)*

Basi Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na utaratibu wa maswali ya kawaida, lakini naomba nimwite Naibu Spika ili aweze kuendelea hapa mezani. *(Makofi)*

Hapa Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ni kipindi cha maswali ya kawaida, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, Mheshimiwa Ally Saleh Ally, Mbunge wa Malindi.

MHE ALLY SALEH ALLY: Spika ameamua. Napenda sasa...

NAIBU SPIKA: Samahani Mheshimiwa, linaanza la Silinde, nilikuwa nimefunuliwa sehemu nyingine, samahani. Tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Momba.

Na. 30

Serikali Kutoa Fedha kwa Wilaya ya Momba

MHE. DAVID E. SILINDE aliuliza:-

Wilaya ya Momba ni moja kati ya Wilaya mpya zilizoanzishwa hivi karibuni ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi:-

Je, kwa nini Serikali imekuwa ikisuasua kutoa fedha ili ziweze kujenga ofisi na nyumba za watumishi katika Makao Makuu ya Wilaya ya Momba eneo la Chitete?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Momba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2013/2014, ilifanikiwa kupeleka fedha shilingi milioni 250; ambazo zimetumika kuanza ujenzi wa nyumba ya Mkuu wa Wilaya na ujenzi wa nyumba mbili za Viongozi waandamizi ambao umefikia hatua ya msingi. Katika mwaka wa fedha 2014/2015 fedha zilizotengwa kwa kazi hizo hazikupelekwa. Aidha, katika mwaka 2015/2016, Serikali imetenga shilingi milioni 282.7 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa nyumba hizo na shilingi milioni 200 zimetengwa kuanza ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa ujenzi wa Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Momba, Serikali katika mwaka wa fedha 2014/2015, ilitoa shilingi milioni 450; kwa ajili ya kuanza ujenzi wa ofisi hizo. Katika jitihada za kuhakikisha Halmashauri inawapatia watumishi wake nyumba bora, Serikali imezielekeza Halmashauri kutumia mapato ya ndani, kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za watumishi. Aidha, Halmashauri imeingia mkata wa ujenzi wa nyumba 20 kwa gharama ya shilingi bilioni 2.1 na Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)* ili kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kujenga nyumba na Ofisi za Viongozi katika Wilaya mpya kwa kadri upatikanaji wa fedha utakavyoruhusu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Silinde swali la nyongeza!

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini niseme Serikali inaonekana haiko *serious* katika hizi Halmashauri mpya ambazo tumekuwa tukizianzisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2014/2015 Halmashauri ya Wilaya ya Momba tuliomba shilingi bilioni mbili fedha maalum, maombi maalum, kwa ajili ya kuanzisha ujenzi wa Makao Mkuu yaani kwa maana ya kujenga boma na nyumba za watumishi ili watumishi watoke katika Halmashauri mama ya Mbozi kwenda Momba eneo la Chitete wakaanze kazi maalum. Mwaka 2014/2015 ukiangalia hapa hapa Serikali haijatenga kitu chochote, ni kwa nini Serikali inakuwa haiko *serious* inapoanzisha Wilaya mpya kwa ajili ya maandalizi ya watu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali (b), Halmashauri ya Momba ipo katika Mkoa mpya wa Songwe ambao na wenyewe umeanzishwa hauna Mkuu wa Mkoa, hauna ofisi, hauna chochote. Ni kwa nini Serikali imekuwa ikianzisha jambo la msingi lakini utekelezaji imekuwa ikishindwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka kupata majibu lini Mkoa Mpya wa Songwe utapelekewa Mkuu wa Mkoa na ofisi itakuwepo pamoja na Halmashauri ya Mombo? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Silinde anasema kwamba Serikali haina nia ya dhati. Kikubwa zaidi naomba kwanza Bunge lako hili, tukiri kwamba miongoni mwa mambo ambayo Watanzania wametendewa haki na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni pale ambapo maombi yamepelekwa ya Mikoa, Halmashauri na Wilaya mpya na Serikali ikaamua kutekeleza hili ili mradi suala la kuleta huduma kwa wananchi, naomba tukiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo ukija kuangalia katika ujenzi wa Ofisi za Wilaya peke yake, takribani Serikali ilitenga ujenzi wake kupitia *TBA* zaidi ya bilioni 12.9. Katika mchakato huo zaidi ya bilioni 5.6 zimepelekwa na mchakato mwingine unaendelea. Naomba tukiri kwamba rasilimali fedha ndiyo lilikuwa tatizo, lakini Serikali inajitahidi kuhakikisha kwamba, Halmashauri na Wilaya zilizojengwa na Mikoa iweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala zima hususan la Mkoa wa Songwe, Serikali imejipanga itajitahidi kwa kadri iwezekanavyo na ukija kuangalia hivi sasa, tuna Mikoa hii mipya iliyoanzishwa na lengo kubwa ni kukusanya mapato. Mwisho wa siku ni kwamba ofisi hizi na hasa masuala ya kiutawala, ngazi za utawala ziweze kukamilika ilimradi wananchi waweze kupata huduma, lakini Serikali imejidhatiti katika hilo kwa ajili ya kuleta huduma kwa wananchi.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE - WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa. Pengine bila kurudia yale aliyoyasema, nimesimama ili tu niongezee jibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Silinde anasema Mkoa wa Songwe umeanzishwa, mchakato wa Mkoa wa Songwe kuanzishwa haujakamilika kwa sababu hadi sasa hatuja-*gazette*. Kwa hivyo, huwezi ukaanza kumhudumia mtoto kabla hajazaliwa, unamnunulia nguo za kwenda shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakachofanya kwa sasa baada ya muda tutatoa tamko rasmi la Serikali na tamko la Serikali huwa lipo kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, tukishaipa *GN,* tutatamka kwamba Rais ameuanzisha huo Mkoa. Naomba uvumilie, lakini napongeza pia, najua una hamu kweli kuanza kuingia katika Mkoa wa Songwe, lakini taarifa hiyo uliyoitoa ni kwamba bado hatujauanzisha rasmi Mkoa wa Songwe, subiri tutatamka wakati wowote Serikali itakapokuwa tayari imemaliza mchakato wake. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Waziri. Swali la mwisho la nyongeza Mheshimiwa pale mwisho.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ofisi ya TAMISEMI ina kauli gani kutokana na Halmashauri mpya zilizoanzishwa ili kuziwezesha rasilimali watumishi, fedha na vitendea kazi, kwa kuwa ni mahitaji makubwa ya wananchi kupata huduma hizo, katika maeneo ya Halmashauri mpya zilizoanzishwa? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba nini kauli ya Serikali. Kauli ya Serikali ipo pale pale kwamba Halmashauri zimeanzishwa na lengo kubwa ni kwamba, Halmashauri hizi ziweze kupata vitendea kazi, watumishi na ndiyo maana katika ziara zetu za juzi juzi tulivyokuwa tunapita, miongoni mwa Halmashauri tulizozipitia ni Halmashauri mpya. Jambo lililofanyika ni kwamba michakato ya kuomba vya watumishi kupitia Ofisi ya Utumishi, imeshakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, juzi juzi tulikuwa kule Wanging'ombe mambo haya yanakwenda. Mwisho wa siku, lengo kubwa ni kwamba Serikali imeji-*commit,* Halmashauri zimeanzishwa na ziweze kupata miundombinu ya ujenzi, lakini hali kadhalika zipate watenda kazi, ili mradi mwisho wa siku wananchi waweze kupata huduma.

Kwa hiyo, Serikali imejizatiti katika hilo, lengo kubwa ni kwamba wananchi wapate huduma katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tuendelee, swali linalofuata ni la Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, Mheshimiwa Ally Saleh Ally, Mbunge wa Malindi.

Na.31

Mafanikio ya Mkutano wa Dunia Kuhusu Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Mazingira

MHE. ALLY SALEH ALLY aliuliza:-

Hivi karibuni ulifanyika Mkutano wa Dunia wa Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Mazingira *(COP21)* ambapo Katibu Mkuu wa *UN* alisema Mkataba uliofikiwa ni *momental triumph for people and our planet aimed at ending poverty, strengthening peace and ensuring life of dignity and opportunity to all*:-

(a) Je, Serikali ya Tanzania ilishiriki vipi katika Mkutano huo?

(b) Je, Serikali itatekelezaje maazimio ya Mkutano huo kisera, kisheria na kiutendaji?

(c)Je, Serikali ina mikakati gani ya kupambana na umaskini, kuimarisha amani, heshima na fursa sawa kwa kila mtu?

NAIBU WAZIRI WA MUUNGANO NA MAZINGIRA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Saleh Ally, Mbunge wa Malindi, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Mkutano wa 21 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi ulifanyika Paris, Ufaransa tarehe 30 Novemba hadi 12 Desemba, 2015. Ujumbe wa Tanzania uliongozwa na Begum Karim Taj, Balozi wa Tanzania nchini Ufaransa, wataalam kutoka Ofisi ya Makamu Rais, Kilimo na Zanzibar walishiriki pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushiriki wa Tanzania katika Mkutano huu ulilenga kutekeleza msimamo wa Tanzania katika majadiliano ikiwa ni pamoja na:-

(i) Upatikanaji wa fedha na teknolojia za kushughulikia mabadiliko ya tabianchi;

(ii) Upunguzaji wa gesijoto kwa ajili ya nchi kwa kuzingatia historia ya chanzo cha mabadiliko haya na uwezo wa nchi husika kukabiliana na tatizo hilo;

(iii) Kuweka kipaumbele katika uhimili wa mabadiliko ya tabianchi kwa sekta zote; na

(iv) Kushiriki katika miradi ya kupunguza gesijoto na nchi zilizoendelea kuendelea na jukumu la kutoa feda na tekinolojia kwa nchi zinazoendelea.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itatekeleza maazimio ya Mkutano huo kisera, kisheria na kiutendaji kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Tanzania inatarajia kutia saini Mkataba wa Makubaliano ya Paris kati ya tarehe 22 Aprili, 2016 na 21 Aprili, 2017. Hatua hii itaimarisha utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Mabadiliko ya Tabianchi wa mwaka 2012.

(ii) Serikali pia itahakikisha kuwa Tanzania inanufaika na fursa zilizo chini ya Mfuko wa Dunia wa Mabadiliko ya Tabianchi *(Green Climate Fund),* unaofadhili shughuli za Mkataba wa Makubaliano ya Paris.

(iii) Aidha, Serikali itaendelea kuzibana nchi zote zenye kuzalisha hewa ya ukaa ili zipunguze uzalishaji huo kulingana na misingi ya utekelezaji wa Mkataba huo.

(iv)Zaidi ya hayo, Serikali itaendelea kuwasiliana na washirika wa maendeleo ili kuanzisha maeneo ya ushirikano kwa muktadha wa utekelezaji wa Mkataba wa Paris.

(v) Mwisho Serikali itaimarisha juhudi na kujenga uwezo wa elimu kwa umma kuhusu athari za mazingira ya tabianchi na namna ya kukabiliana nazo ili kuimarisha juhudi za kuhimili athari za mabadiliko haya.

(c)Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutekeleza mkakati wa kupambana na umaskini, kuimarisha amani, heshima na fursa sawa kwa wote. Mikakati hiyo ni kama MKUKUTA, MKUZA, MKURABITA, na matumizi ya Mifuko mbalimbali katika kukabiliana na tatizo hili kama vile; Mfuko wa Mazingira, Mfuko wa Jamii chini ya Ofisi ya Rais *TASAF*, Benki ya Wakulima, Benki ya Wanawake na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, juhudi kwa sasa za Serikali ya Awamu ya Tano za kupambana na ufisadi, kuimarisha utawala bora, uadilifu na uwajibikaji, zitatoa mchango mkubwa katika kuleta amani na maendeleo kwa wananchi wote. Kujenga uwezo na kuimarisha ushirikishwaji wa Serikali za mitaa katika

utekelezaji wa miradi ya mabadiliko ya tabianchi unazingatiwa ili fursa zinazopatikana ziwafikie Watanzania wengi zaidi kadri iwezekanavyo.

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Swali la nyongeza Mheshimiwa Suzan Lyimo, Ah! *Sorry* Mheshimiwa Ally Saleh sikuwa nimekuona, samahani.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Haya ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza ni suala lile la kwamba masuala ya gesijoto na tabianchi yanasimamiwa na Mkataba wa Kimataifa unaoitwa *United Nation FrameWork Convetion on Climate Change*. Katika mfumo wake kunakuwa na mtu au sehemu inaitwa *focal point* ambapo ndipo mambo yote yanapopitia.

Ni kwa nini hakuna sauti ya Zanzibar katika hiyo *focal point* ya Tanzania, hakuna mwakilishi wa Zanzibar ama *alternatively* au kutoka Zanzibar ili kuhakikisha maslahi ya Zanzibar yanalindwa katika suala hilo? La kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kumekuwa na taarifa na hali ndiyo ilivyo kwamba Zanzibar kama visiwa vingine vidogo vingi vinaweza kukabiliwa na tatizo hili la ongezeko la gesi na mabadiliko ya tabianchi na kwa hivyo hata uwepo wake upo hatarini. Je, Serikali ina mpango gani wa kudumu na wa muda mrefu katika kuhakikisha kwamba Zanzibar inatoka katika *loop* kubwa zaidi ya kuilinda ili iendelee kuwepo katika uso wa dunia. Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza anasema kwamba ushirikishwaji wa Zanzibar hasa katika suala zima la *climate change* pamoja na ongezeko la gesijoto kwamba Zanzibar inashirikishwa namna gani. Tumekuwa tukishirikiana na Zanzibar kwa karibu na ndiyo maana hili suala la mazingira limewekwa Ofisi ya Makamu wa Rais ili kuweza kufanya ushirikiano mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Mkutano wa Paris tunaouzungumza ulihudhuriwa na watu kumi na saba, watano walitoka Zanzibar na Ofisi ya Makamu wa Rais imekuwa ikifanya kazi bega kwa bega na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kitengo cha Mazingira, ambapo tumekuwa tukishirikana kwa kila hali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi juzi hapa kuna suala lilitokea la kudidimia kwa ardhi, kuna sehemu kumedidimia kule Zanzibar, Ofisi yangu hapa ya Mazingira pamoja na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Kitengo cha Mazingira

wameshiriki kufanya utafiti kuona tatizo hili linasababishwa na nini. Kwa hiyo, kwa ujumla tumekuwa tukishirikiana vizuri sana na Zanzibar hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo limezungumzwa hapa na Mheshimiwa la kuhusu Zanzibar kama kisiwa, kama tunavyojua ni kweli kabisa kwamba, sasa hivi ni dunia nzima ipo kwenye hali ngumu ya mabadiliko ya tabia ya nchi. Joto la dunia limeongezeka kutoka kwenye *standard* ya kawaida na kufikia nyuzi joto zero *point* nane tano. Dunia nzima tunahangaika sasa hivi kuhakiksha kwamba hizi nyuzi joto haziongezeki kufikia kuzidi nyuzi joto moja *point* tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kina cha bahari kimeongezeka kwa sentimita kumi na tisa. Kwa hiyo, hili ni tishio kubwa ambalo lazima tuchukue hatua za dhati za kuhakikisha kwamba tunakabiliana na matatizo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwenye Mpango wa Maendeleo *(framework)* ambayo tumeanza nayo sasa hivi, Kitaifa tunajipanga kuhakikisha kwamba Tanzania kama Tanzania inatenga fedha za kutosha kukabiliana na suala la mabadiliko ya tabianchi. Vilevile wahisani wetu, tunaendelea kuhakikisha kwamba wanashiriki katika kuhakikisha kwamba Tanzania inapata fedha za kutosha kuhusu suala zima la mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchini Ufaransa kwenye Mkutano wa Paris, Tanzania imepata fedha dola laki tatu kwa ajili ya kukabiliana na tatizo la mabadiliko ya tabianchi. Vile vile tumepata fedha dola laki nne kwa ajili ya kuripoti mpango wa ripoti ya tatu kwa ajili ya kukabiliana na matatizo ya tabianchi. Pia tumepata fedha dola za marekani mia tatu hamsini na mbili, kwa ajili ya kuandaa tathmini ya kwanza ya kupunguza gesijoto nchini. Kwa hiyo, mikakati hii yote tunayoifanya na hatua ambazo tunazozifanya kupitia mpango wa maendeleo na bajeti yetu, zote hizi zitalenga katika kupunguza athari ya mabadiliko ya tabianchi.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika…

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Suzan Lyimo kwa sababu nilikuwa nimekutaja!

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, hakujibu hata swali moja nililomuuliza, amemeza takwimu, amekuja na takwimu, lakini hakujibu hata swali moja nililomuuliza. Labda nitawaona pembeni, hawezi kujibu, hana uwezo wa kujibu.

NAIBU SPIKA: Naomba uzime kipaza sauti Mheshimiwa Ally Saleh. Kama hukuridhika na majibu unaweza kuandika! Samahani Mheshimiwa Suzani Lyimo.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niongeze machache katika kuyakamilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Mkutano wa Paris, kila nchi ilitakiwa kutengeneza *program* inaitwa *intended national determined contributions*, yaani kila nchi itengeneze mpango wa namna ya kutekeleza makubaliano ya Paris. Katika kutengeneza mpango ule tumeshirikana na wenzetu wa Zanzibar kwa kutambua changamoto mahususi ya kwamba Zanzibar ni kisiwa, uchumi wake unategemea utalii, utalii unategemea fukwe na fukwe zinaathiriwa sana na kupanda kwa kina cha bahari. Kwa hiyo, tumefanya hivyo na tutaendelea kufanya hivyo ili kuhakikisha kwamba Zanzibar inabaki kama ilivyo katika uzuri wake na ubora wake ili isiathiriwe na changamoto hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *focal point* tumeomba kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais ndio iwe *focal point* ya Taifa letu katika utekelezaji wa mkataba ule. Ile Ofisi ya *focal point* itajumuisha Wazanzibar, tutahakikisha hilo linatokea kwa sababu changamoto zetu hizi ni changamoto za pamoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Waziri, swali la mwisho la nyongeza Mheshimiwa Suzan Lyimo!

MHE. SUZAN A. LYIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Ni wazi kwamba Tanzania imeathirika sana na mabadiliko ya tabianchi, lakini vilevile sababu kubwa pamoja na kwamba kuna sababu za nje, lakini kuna sababu za ndani ambayo kubwa ni ukataji hovyo wa miti, lakini Serikali kwa muda mrefu imekuwa na kaulimbiu ya kusema kwamba kata mti panda miti.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nilikuwa nasikiliza au naangalia vyombo vya habari hapa Dodoma ambapo ni kati kati ya nchi na Makao Makuu, Mkuu wa Mkoa alikuwa anapanda miti na ikatolewa taarifa kwamba katika miti milioni mbili na laki tatu iliyopandwa ni miti mia tisa tu imeota, sawa na asilimia 0.039. Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba wanafuatilia ili miti inapopandwa iweze kuota ili kuondoa tatizo la mabadiliko ya tabianchi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la ukataji miti na suala la kupanda miti isiote. Sasa hivi tunaandaa mkakati wa pamoja, Ofisi ya Makamu wa Rais,

Mazingira, pamoja na Maliasili na Utalii na wadau wengine kuhusu mkakati wa Taifa hili katika kuhakikisha kwamba tunapanda miti ya kutosha nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo, tunawashirikisha kwa karibu sana wataalam wetu wa Chuo cha *SUA* ili kuweza kujua ni miti gani au ya aina gani inaweza kuzalishwa katika mazingira ya mkoa gani ikastawi kwa uzuri zaidi.Katika kufanya hivyo tayari *report* ya kwanza tumekwishaipata na tutahakikisha kwamba tunawashauri mikoa mbalimbali namna ya upandaji miti kulingana na mazingira waliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nichukue wito huu kuwahamasisha Watanzania wote, tumeshaagiza kila Halmashauri kupanda miti 1,500,000 kila Wilaya kwa mwaka. Zoezi hili lifanyike na tutahakikisha kwamba wataalam wetu wanawasaidia katika kuhakikisha kwamba mbegu zinapatikana, zinazokubalika kulingana na mazingira hayo na wananchi wapande miti yenye faida na wao miti ya matunda na miti ya mbao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema pia hata suala ambalo lilizungumzwa jana na Mheshimiwa hapa kwamba, unapanda miti lakini mwisho wa siku viwanda vyetu vya *juice* vinakosa matunda ambayo yanastahili kwa ajili ya *juice hiyo*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango huu tunafanya utafiti pia wa kutosha kuona kwamba, miti inayopandwa, inatuletea na inatupatia matunda ambayo yatakuwa ni chanzo cha *raw material* kwa ajili ya viwanda vyetu vinavyojengwa hapa nchini. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji na swali litaulizwa na Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 32

Tatizo la Maji – Mji wa Makambako

MHE. NEEMA W. MGAYA aliuliza:-

Kumekuwa na tatizo kubwa la upatikanaji wa maji katika Mji wa Makambako:-

Je, Serikali imejipangaje kutatua tatizo hilo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kupita awamu ya kwanza ya programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji *(Water Sector Development Program - WSDP)* imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa mradi wa maji wa Makambako. Kazi zitakazotekelezwa katika mradi huu ni pamoja na ujenzi wa bwawa la Tagamenda, uchimbaji wa visima virefu vya Idofi na chemichemi ya Bwawani, ujenzi wa bomba kuu na mfumo wa usambazaji wa maji na matanki makubwa ya kuhifadhi maji. Mradi huu unakadiriwa kugharimu kiasi cha wastani wa shilingi za Kitanzania bilioni 70.3 sawa na dola za Marekani milioni 32.39 na unatarajiwa kunufaisha wananchi wapatao 155,233.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi wa Mradi wa Maji Makambako utatekelezwa katika awamu ya pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji *(WSDP II)* katika mwaka wa fedha 2016/2017. Hivi sasa Serikali inakamilisha taratibu za kupata mkopo wa gharama nafuu kutoka Serikali ya India kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Serikali ilitenga shilingi bilioni moja ili kuboresha hali ya huduma ya maji katika Mji wa Makambako. Wakati mradi mkubwa unasubiriwa na pindi fedha zikipatikana kabla ya mwaka kumalizika fedha hizo zitatumwa.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa…

NAIBU SPIKA: Mwenye swali una swali la nyongeza?

MBUNGE FULANI: Anayo anayo.

NAIBU SPIKA: Yuko wapi? Neema Mgaya nilikuwa sijakuona haya endelea.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yenye matumaini, hata hivyo, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, tatizo la maji ni sugu katika Kata ya Saja, Kijombe, Wanging'ombe na Njombe Mjini, je, Serikali itatatua lini tatizo hili nimekuwa nikiulizia mara kwa mara swali hili katika Bunge lililopita? *(Makofi)*

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba niongezee kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Neema Mgaya kama ifuatavyo:-

Kwanza tunakiri kweli kuna upungufu mkubwa wa maji maeneo hayo unayoyataja, Njombe Mjini kuna tatizo kubwa, Makambako kuna tatizo kubwa, hizo Kata za Saja, Kijombe na Wanging'ombe zote zina matatizo makubwa. Ndiyo maana Serikali imeshafanya usanifu wa kukarabati miradi iliyopo na kuongeza miradi mipya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari Serikali imepata milioni 500 *US dollar* sawasawa na shilingi za Kitanzania trilioni moja kwa ajili ya kuweza kukarabati miradi pamoja na Miji mingine 17. Kwa hiyo, kazi hii tuko kwenye hatua ya mwisho ya kuanza kutekeleza na tutafanya hivyo kwa kuanzia mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana wananchi wa huko wawe na imani na Serikali ya Awamu ya Tano kwamba tunakwenda kumaliza tatizo hili. Mheshimiwa Rais alipokuwa Makambako, nakumbuka kabisa alisema nipeni Urais, nitakwenda kumaliza tatizo la maji Makambako. Mheshimiwa Sanga alikuwepo nataka nikuhakikishie tatizo la maji Makambako tunakwenda kulimaliza. Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Deo Sanga nilikuwa nimekutaja!

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, vilevile niishukuru kauli ya Serikali kwa kunipa matumaini kwamba sasa wananchi wangu wangu wa Makambako watapona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tatizo la Makambako ni la muda mrefu takribani zaidi ya miaka 30 na kitu, mradi ambao tunao pale ulikuwa unahudumia watu 15,000 na sasa tumeshaongezeka na tumefikia zaidi ya watu 160,000. Je, Serikali imejipangaje kuona sasa tatizo hili linatatuliwa mapema na kama Rais alivyokuja alituahidi kwamba tatizo hili atalitatua?

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri Waziri mwenye dhamana alikuwepo siku ile wakati Rais anazungumza kwamba, atakapomteua Waziri aanzie Makambako leo unawaambiaje watu wa Makambako?

La pili…

WABUNGE FULANI: Aaaa!

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sanga swali ni moja tu.

MHE. DEO K. SANGA: Namalizia, namalizia Mheshimiwa.

NAIBU SPIKA: Swali ni moja, tafadhali naomba ukae ili Mheshimiwa Waziri aweze kujibu.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyotoa maelezo ya nyongeza kwa muuliza swali la msingi niseme tu kwamba, nitakachofanya sasa baada ya Bunge hili mimi nitatembelea Makambako, tutakwenda kuongea na wananchi ili tuwape mpango ambao tunao wa kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Tatizo la maji la Makambako kwa asilimia kubwa linafanana na Jimbo la Bunda Mjini. Natambua Serikali ya Awamu ya Nne ilianza mradi mkubwa wa maji tangu mwaka 2006 ni wa muda mrefu sana na ulikuwa ukamilike, lakini mpaka sasa hivi haujakamilika.

Mheshimiwa Naibu spika, mradi ule unaanzia Kata ya Guta lakini hauna vituo na kama mradi ule wa kupeleka maji katika Mji wa Bunda ukiwa na vituo, vile vijiji jirani Kinyambwiga, Tairo, Guta A, Guta B, Gwishugwamala, vyote vitanufaika na mradi wa maji. Sasa je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba kuna haja ya kuweka vituo ili vijiji hivyo vinavyopita mradi kwenda Mji wa Bunda vinufaike na mradi huo? *(Makofi)*

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna mradi ambao tumetekeleza katika Mji wa Bunda tumeweza kujenga bomba kubwa kutoka Ziwa Victoria, tumeweza kujenga matanki, hiyo ni awamu ya kwanza. Sasa awamu ya pili tutakwenda kusambaza katika maeneo yale ambayo bomba hilo limepita. Kwa hiyo, naomba niseme tu kwamba, kazi hiyo tutakwenda kuifanya kwa manufaa ya wananchi wa Bunda. Ahsante. (*Makofi)*

MHE. SULEIMAN A. SADDIQ: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa katika Wilaya ya Mvomero ipo miradi ya maji iliyo chini ya Wizara katika maeneo ya Tarafa za Mgeta, Mlali, Turiani na Mvomero na kwa kuwa miradi hiyo imeanza, lakini bado haijakamilika na kwa kuwa Serikali imeshatumia mamilioni ya fedha. Je, Serikali sasa iko tayari kuleta fedha zilizobaki ili miradi ikamilike katika maeneo hayo na wananchi wapate maji safi na salama Wilayani Mvomero?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, jana kwenye jibu la msingi la matatizo ya maji nilieleza katika awamu ya kwanza ya programu ya maji iliyoanza mwaka 2007 na imeishia mwaka 2012 tulikuwa na miradi 1,855.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi iliyokamilika ni miradi 1,143 na miradi inayoendelea ni miradi 454 ambapo katika hii miradi inayoendelea ipo miradi katika Jimbo la Mheshimiwa Saddiq, sasa hivi mwezi Januari tunaanza progamu ya pili ya Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Maji. Kwa hiyo, katika mpango huu nimhakikishie Mheshimiwa Saddiq kwamba fedha itatolewa kuhakikisha miradi hii inakamilika.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Mheshimiwa Haji Khatib Kai!

Na. 33

Soko la Afrika Mashariki

MHE. HAJI KHATIB KAI aliuliza:-

Tanzania ni mwenyeji mkubwa kati ya nchi zilizounda Umoja wa Afrika Mashariki, hivyo basi, hupelekea au hupaswa Watanzania kufaidika na soko la Afrika Mashariki:-

(a) Je, Serikali inawashauri nini wananchi wake wanapokwenda kibiashara kwenye nchi zinazounda umoja huo?

(b) Je, pindi wanapopata matatizo au vikwazo katika nchi husika ni wapi watapeleka malalamiko?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, WASANII NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Haji Khatib Kai, Mbunge wa Micheweni, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimendoleana ushuru wa forodha mipakani, hatua ambayo inapanua soko la bidhaa za Tanzania kufikia Wanaafrika Mashariki takribani milioni 143 katika nchi tano Wanachama wa Jumuiya za Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi. Hivyo ni dhahiri kuwa, endapo soko hilo litatumika kikamilifu litachangia kwa kiasi kikubwa kukuza uchumi wa Taifa na kupunguza umaskini wa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Serikali inawashauri wananchi kuzichangamkia fursa za kibiashara, ajira, uwekezaji na kadhalika zitokanazo na Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kujiharakishia maendeleo.

Pili, Serikali inawashauri wananchi kuzitambua taratibu za kufuatwa katika kuzitumia fursa za kibiashara zilizopo katika Jumuiya kama nchi wanachama zilivyokubaliana ikiwa ni pamoja na kuwa na cheti kinachobainisha kuwa bidhaa imezalishwa ndani ya Jumuiya yaani cheti cha uasili wa bidhaa- *EAC certificate of Origin* na vibali/nyaraka kutoka mamlaka husika kutegemeana na aina ya bidhaa mfanyabiashara anazotaka kuuza au kununua.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa katika kufanya biashara katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, vikwazo visivyo vya kiforodha hujitokeza kwa wafanyabiashara wetu kinyume na makubaliano ya nchi wanachama. Napenda kutoa rai kwa wafanyabiashara kuwasiliana na Wizara yangu pindi wanapopata matatizo au vikwazo vya kibiashara katika Jumuiya, Balozi zetu au Vyama vya Wafanyabiashara kama vile *Tanzania Chamber of Commerce Industry and Agriculture (TCCIA), Tanzania Private Sector Foundation (TPSF), Tanzania Exporters Assosiation (TANEXA)* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha Wizara imeweka mabango makubwa yani *double sided billboards* yenye ujumbe wa taratibu za kufuatwa na wafanyabiashara wadogo, wa kati, wa kuuza au kuagiza bidhaa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki katika mipaka ya Horohoro, Rusumo, Kabanga, Namanga, Sirari na Mtukula na vilevile imeweka Maafisa wake katika mipaka ya Rusumo, Mtukula, Namanga na Sirari kwa ajili ya kuwasaidia au kutatua changamoto za wananchi wanapofanya biashara na nchi wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge kuwahamasisha wananchi katika Majimbo yao kuzitumia fursa zitokanazo na Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Haji Khatib Kai, swali la nyongeza!

MHE. HAJI KHATIB KAI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Baada ya kupata maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imeshauri wananchi kuzitambua na kuzitumia fursa za soko la Afrika Mashariki na kwa kuwa Serikali na Wizara husika, ina wajibu wa kutoa elimu kwa wananchi wa Tanzania kuhusiana na soko la Pamoja la Afrika Mashariki. Ni kwa nini na ni lini Serikali au Wizara husika itatoa elimu kwa wananchi wa Kaskazini Pemba hasa Jimbo

langu la Micheweni ili waepukane na tabu ambazo wamekuwa wakizipata kila mara?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema, endapo matatizo yatatokea au vikwazo vitatokea wananchi wawasiliane na Wizara yake au Balozi zetu. Binafsi wananchi hawa au Watanzania hawa wapatao 130 wanaotoka Jimbo langu na Majimbo mengine, waliposhikwa nchini Kenya waliwasiliana na mimi na mimi nikawasiliana na Balozi zetu zote mbili Nairobi na Mombasa kwa ajili ya msaada, msaada ambao ulishindikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilifuata utaratibu wa kwenda Ofisi ya Wizara ya Mambo ya Nje kwa msaada zaidi na nilikutana na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara na tulikubaliana kilichofanyika si sahihi. Kwa bahati mbaya, naomba kumwuliza swali Mheshimiwa Waziri, hadi sasa sijapata mrejesho wowote, je, atakubaliana nami kwamba Watanzania hawa ambao hawakupata msaada si ni wazi kwamba, kutokana na itikadi yao ya kisiasa ndilo jambo ambalo lilipelekea kushindwa kupatikana msaada wowote? (*Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waziri Mwakyembe!

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya swali la msingi. Ningependa nimjibu Mheshimiwa Kai, Mbunge wa Micheweni maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine kwa upande wa Tanzania nimekuwa Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri la Afrika Mashariki kwa mwaka mzima. Hili suala analolieleza hapa ndiyo nalisikia kwa mara ya kwanza. Kwa hiyo, ningeomba tu Mheshimiwa Mbunge hilo analolisema ni kitu kizito sana, itabidi tukae chini na Wizara husika tuweze kuelewa kilitokea kitu gani hata kama alikwenda Ubalozi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kifupi, naomba kutoa wito kwa wananchi wa Tanzania wanaofanya biashara katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, ukipata matatizo kama Naibu Waziri alivyosema kwenye jibu la swali la msingi, hakikisha unakwenda Ubalozi, ukishindwa nenda Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa, ukishindwa nenda *TCCIA (Tanzania Chamber of Commerce and Industrial and Agriculture)*, ukishindwa nenda *Tanzania Exporters Association (TEA)*.

Kwa hiyo, taasisi zote hizi zitakusikiliza lakini hakikisha Wizara inapata taarifa kwa sababu tuna miundombinu tayari ya kulalamika.Wenzetu wanajua sana kulalamika, Watanzania tunalalamika chini kwa chini.

La pili, lini tutatoa elimu kwenye Jimbo lake? Elimu tunatoa kuanzia hii Wizara ilipoanzishwa, tunatoa kupitia vipindi vya redio, *television*, *pamphlets*, kupitia mikutano, hatuwezi kufanya *specifically* kwa Jimbo moja, lakini naomba niwahakikishie Watanzania kwamba biashara Afrika Mashariki sasa hivi imeongezeka kwa kasi na Watanzania tunachangia kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe wito tu kwa wafanyabiashara wa Kitanzania, tutumie hii fursa ya kupeleka bidhaa katika nchi za Afrika Mashariki kwenye bei nzuri, hulipi chochote kwa bidhaa zote ambazo zina uasilia wa Afrika Mashariki, unachotakiwa tu ni kupata hiyo *certificate* ya *origin* pale unapofika mpakani hasa kama bidhaa yako haizidi *dola* 2,000 na kwa wafanyabiashara wakubwa wao wanapata kutoka *TCCIA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbatia!

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ametuelekeza Watanzania wachangamkie fursa zinazojitokeza katika Soko la Pamoja la Afrika Mashariki na Jimbo la Vunjo ni sehemu ya kuchangamkia fursa hizo *especially* eneo la Taveta. Sasa lini Serikali itaharakisha ujengaji wa soko la Kimataifa la Lokolova pale Himo ili fursa hizo ziweze kutumika kwa Watanzania?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa soko la analolieleza Mheshimiwa Mbatia ni moja tu ya miradi mingi ambayo Serikali imefanya kuongeza fursa ya Watanzania kushiriki katika biashara ya Afrika Mashariki. Yeye mwenyewe atakuwa ni shahidi kwamba Serikali sasa hivi ina miradi ambayo nusu yake imekamilika ya kujenga vituo vya pamoja kwenye mipaka vinane, tunaita *one stop boarder post* na tumejenga vituo vizuri sana ambavyo vimeharakisha biashara katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile analolisema Mheshimiwa Mbatia ni suala ambalo tunafikiri ni muhimu kwa Wizara sasa hivi ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa maeneo yote ya mipakani, kwa kweli tuharakishe kumalizia miradi yote ambayo tumeianza na ambayo tunaifikiria ya masoko ya pamoja kwa sababu wenzetu upande wa pili wamechangamkia kweli fursa hiyo. Nadhani huo ni wajibu wa Serikali kuliangalia hilo kwa makini kwa kila mpaka siyo tu kwenye Jimbo la Vunjo.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tuendelee. Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, Mbunge wa Busokelo.

Na. 34

Kukamilika kwa Ujenzi wa Barabara ya Katumba-Mbambo- Tukuyu kwa kiwango cha lami

MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE aliuliza:-

Kwa muda mrefu wananchi wa Busokelo wamekuwa wakikumbana na adha kubwa ya ubovu wa barabara ya Katumba - Mbando - Tukuyu yenye urefu wa kilometa 82 inayoanzia Katumba *(RDC)* kupitia Mpombo, Kandete, Isange, Lwangwa, Mbwambo *(BDC)* hadi Tukuyu *(RDC)* na barabara hii imekuwa kwenye mpango wa kujengwa kwa kiwango cha lami kwa muda mrefu na Mkandarasi yuko eneo la ujenzi wa kipande cha kilometa kumi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha barabara hiyo kwa kujenga sehemu iliyobaki yenye kilomita 72?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete, Mbunge wa Busokelo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Katumba - Mbwambo - Tukuyu yenye urefu wa kilometa 82 ni barabara ya Mkoa inayohudumiwa na Wakala wa Barabara *(TANROADS)* Mkoa wa Mbeya. Barabara hii ni ya changarawe na ipo kwenye hali nzuri kwani inapitika vizuri isipokuwa maeneo machache yenye miteremko mikali inayoteleza wakati wa mvua. Serikali imekuwa ikifanya matengenezo ya aina mbalimbali ili barabara hii iendelee kupitika wakati wote bila matatizo.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa barabara hii, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Serikali kupitia Wakala wa Barabara ilianza maandalizi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami ambapo upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ulikamilika mwezi Februari, 2012.

Baada ya usanifu wa kina kukamilika katika mwaka 2013/2014 kiasi cha shilingi milioni 1,270 kilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya kilomita 2.5 kwa kiwango cha lami. Aidha, baadaye Serikali iliamua kujenga kilimeta 10 ambapo mwezi Aprili, 2014 Wakala wa Barabara uliingia mkataba na kampuni ya *CICO* kujenga kilometa 10 kuanzia Lupaso hadi Bujesi kipande kilichopo Wilayani Busokelo kwa gharama ya shilingi milioni 8,929.724. Ujenzi wa Kipande hicho unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2016.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na ujenzi wa kilometa 72 zilizobaki kulingana na upatikanaji wa fedha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwakibete, swali la nyongeza!

MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini pia niseme tu kwamba barabara hii katika maeneo mengi, kama ulivyokiri kwenye jibu lako la msingi kuna baadhi ya maeneo inateleza, kuna utelezi mkali. Je, Serikali ina mipango gani kuhakikisha kwamba kwa kipindi hiki cha mvua ambapo haipitiki inaweza kujengwa kwa haraka iwezekanavyo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa tuna maeneo mengi sana katika nchi hii yenye matatizo ya mawasiliano ya barabara. Tumetoa maelekezo mahsusi kwa kila Meneja wa *TANROADS* Mkoa kuhakikisha kwamba muda wote wanapata taarifa wapi kuna matatizo na wayashughulikie haraka. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, maelekezo hayo yamekwenda Mkoa Mbeya na pengine nichukue nafasi hii kama walikuwa hawana taarifa sasa wamepata taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge, wakalishughulikie hilo eneo kwa kadri ya maelekezo ya jumla ambayo Mameneja wote wameelekezwa.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa hapo nyuma, ujitaje na jina.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Naibu Spika, naitwa Nkamia. *(Kicheko)*

NAIBU SPIKA: Hapana sio wewe, huyo hapo.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Aaaa, sio mimi.

NAIBU SPIKA: Naam, endelea, ujitambulishe tafadhali!

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana…

MHE. OSCAR R. MUKASA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Jamani tusikilizane, nimemruhusu mtu mmoja.

MHE. OSCAR R. MUKASA: Naitwa Oscar…

NAIBU SPIKA: Huyu hapa, ujitambulishe tafadhali!

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kujua barabara ya Tunduma - Mpemba yenye kilometa 12 itajengwa lini na Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi kwa sababu barabara ile inasababisha msongamano mkubwa sana wa magari kwenye Mji wa Tunduma na wananchi kushindwa kutimiza majukumu yao. Kwa hiyo, nataka Waziri atueleze ni lini barabara hii itaanza kujengwa kwenye Mji wetu wa Tunduma haraka iwezekanavyo? Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri!

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii inahitaji takwimu, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge, avute subira tuwasiliane na wataalam ili tuweze kumpa jibu lililo na uhakika.

NAIBU SPIKA: Swali la mwisho, Mheshimiwa pale, jitambulishe tafadhali, Mama!

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Naibu Spika ahsante sana, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa kususua kwa barabara ya hizi za Busokelo inafanana sana na kusuasua kwa ujenzi wa barabara ya kutoka Dodoma kwenda Babati na hasa kipande cha Mayamaya kwenda Bonga, naomba kujua Serikali inasema nini kuhusu changamoto hiyo kubwa ambayo imechukua muda mrefu na ahadi ilikuwa mwisho wa mwaka 2015 kumalizika?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba barabara ya Busokelo na anayoongelea zinafanana, lakini hii ilikuwa inaongelea matengenezo na hiyo nyingine inaongelea ujenzi. Namwomba Mheshimiwa Mbunge, anafahamu kuna Mbunge ameleta swali kuhusiana na hii barabara. Ni hivi karibuni tu tutapata taarifa kamili na tutalijibu swali linalohusiana na barabara hii ndani ya Bunge hili linaloendelea.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tuendelee. Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa naomba uulize swali!

Ujenzi wa barabara ya Magu hadi Hungumalwa

MHE. RICHARD M. NDASSA aliuliza:-

Je, ni lini barabara ya Magu - Bukwimba - Ngudu - Hungumalwa itajengwa kwa kiwango cha lami?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kuchukua nafasi hii kujibu swali la Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011 na 2011/2012, Wizara kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* ilitenga jumla ya shilingi milioni 1200 ambazo zilitumika kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Magu - Ngudu - Jojiro sehemu ya Ngudu Mjini yenye urefu wa kilometa 1.9

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 na 2015/2016, Serikali ilitenga jumla ya shilingi milioni 200 kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara hiyo yenye urefu wa kilometa 70 na taratibu za kumtafuta Mhandisi Mshauri zinaendelea. Baada ya kukamilika kwa usanifu na gharama za mradi huo kujulikana, Serikali itatafuta fedha za kuanza ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

NAIBU SPIKA: Swali la nyongeza Mheshimiwa Ndassa!

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pia nishukuru kwa majibu ya utangulizi, lakini naomba tu kuiambia Serikali kwamba barabara hii ni muhimu sana kwa ajili ya uchumi pamoja na kijamii. Pia niseme barabara hii ni ahadi ya Rais wa Awamu ya Nne na wakati barabara hii inaahidiwa na Rais wa Awamu ya Nne, Rais wa sasa Dkt. John Pombe Magufuli alikuwepo. Sasa hili suala la upembuzi yakinifu, ni lini hasa kwa sababu swali hapa la msingi, ni lini barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami kwa kuzingatia kwamba hii ni ahadi ya Rais wa Awamu ya Nne?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna nilivyomwelewa, anasisitiza tu kwamba hii kazi ya upembuzi yakinifu ikamilike haraka ili ahadi ya Marais wetu, Rais wa Awamu ya

Nne na Rais wa Awamu ya Tano wakati alipokuwa Waziri wa Wizara ya Ujenzi itekelezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumthibitishia kwamba Wizara yetu itatekeleza ahadi hiyo kikamilifu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Aweso!

MHE. JUMAA H. AWESO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa ujenzi wa barabara ni kichocheo kikubwa kwa shughuli za kiuchumi.

Je, ni lini ujenzi wa barabara ya Tanga - Pangani - Saadani utaanza?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge, barabara hii ili tuweze kuitendea haki, tuwasiliane Wizarani ili wataalam nao watoe mchango wao ili tunapotoa tarehe ya lini itaanza iwe taarifa sahihi. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tuendelee na Wizara ya Maliasili na Utalii, swali litaulizwa na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso.

Na. 36

Mgogoro Kati ya Hifadhi ya Ziwa Manyara
na Kijiji cha Buger

MHE. CECILIA D. PARESSO aliuliza:-

Katika Bunge la Kumi aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii aliunda Kamati Ndogo ya kushughulikia mgogoro uliopo kati ya wananchi wa Kata ya Buger na Hifadhi ya Taifa ya Manyara:-

(a) Je, ni nini matokeo ya Kamati Ndogo iliyoundwa?

(b) Je, ni lini wananchi watapewa taarifa ya Kamati Ndogo iliyokuwa inashughulikia mgogoro huo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, kabla hujaanza kujibu nina tangazo kidogo hapa Waheshimiwa Wabunge. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti anawaomba Wajumbe wa Kamati mkutane Ukumbi wa Msekwa sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Waziri karibu!

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii alifanya ziara katika Wilaya ya Karatu tarehe 2 Juni, 2015 na kuteua Tume iliyopewa Hadidu za Rejea kuhusu kutatua mgogoro baina ya wananchi wa Kata ya Buger na Hifadhi ya Taifa ya Manyara.

Tume ilifanya mahojiano na makundi mbalimbali na kupitia taarifa zote zilizotolewa na Shirika la Hifadhi za Taifa *(TANAPA)* na Taarifa ya awali imeandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Tume imebaini kuwa kwa ujumla chanzo kikubwa cha migogoro baina ya wananchi na Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara ni idadi kubwa ya mifugo na kukosekana eneo la kuchungia katika Kijiji cha Buger. Tume imependekeza hatua za kuchukuliwa ambazo ni pamoja na hizi zifuatazo:-

(a) Kufanya sensa ya mifugo kwa vijiji vilivyopo katika Kata ya Buger ili kubaini idadi ya mifugo iliyopo dhidi ya ukubwa wa ardhi waliyonayo;

(b) Vijiji kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi;

(c) Kutoa elimu ya uhifadhi na Sheria katika vijiji vinavyozunguka hifadhi, hasa Msitu wa Marang;

(d) Kuanzisha Kamati za Mazingira za Vijiji na kuimarisha zilizopo ili kutekeleza vema majukumu yake; na

(e) *TANAPA* kuweka nguvu katika kuchangia miradi ya maendeleo ya jamii kwenye vijiji vinavyozunguka hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaandaa kikao cha wadau ndani ya miezi mitatu ili kuwasilisha mapendekezo ya Kamati na kujadili utekelezaji wake.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza!

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Mgogoro huu kati ya wananchi na Hifadhi ya Ziwa Manyara umedumu kwa muda mrefu na chanzo cha mgogoro ni ardhi ya wananchi kuchukuliwa na Hifadhi bila ridhaa yao.

Huko nyuma waliwaruhusu waweze kutumia angalau umbali wa mita 100 kwa ajili ya kuchungia mifugo yao na baadaye hifadhi ikanyang'anya tena.

Je, Serikali haioni suluhisho la kuondoa mgogoro huu ni kuwaachia hizo mita 100 tu ili mgogoro uishe kabisa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Waziri alipokuja alitoa ahadi kwa wananchi kwamba, kuna fedha shilingi milioni 160 zitapelekwa; shilingi milioni 100 kwa ajili ya madarasa na shilingi milioni 60 kwa ajili ya soko la akinamama, lakini mpaka leo fedha hizo hazijatolewa! Ni lini fedha hizi zitatolewa?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza kuhusu kuwaachia wananchi eneo linalozungumziwa. Swali la msingi lilikuwa ni nini matokeo ya Kamati. Sehemu yake ya pili, ni lini wananchi watapewa Taarifa ya Kamati hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu ya kikamilifu ya swali hili yamo katika Taarifa tunayoizungumzia. Kwa hiyo, kwa kuwa, Taarifa tayari ipo na tumemwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba Taarifa hiyo itakuwa tayari kuwasilishwa mbele ya wananchi ndani ya muda wa miezi mitatu. Nikisema ndani ya muda wa miezi mitatu, inaweza kuwa wiki moja, itakuwa ni vema tukasubiri wakati utakapofika tujue wale waliofanya utafiti wa kitaalam na wakaandaa taarifa wamesema nini, kuliko jibu ambalo linaweza kuwa la haraka haraka tu hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi ya fedha halikadhalika kwa sababu waliofanya utafiti wameangalia mgogoro kwa ujumla wake na upana wake na muundo wa Kamati yenyewe iliyofanya uchunguzi ulijumuisha wananchi pia, nina hakika kama hili ni mojawapo ya mambo yaliyozungumziwa, litakuwemo ndani ya ripoti hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo naomba Mheshimiwa Mbunge, akubaliane na mimi tu kwamba kwa kuwa, nimesema ndani ya miezi mitatu na nimesema ndani ya miezi mitatu inaweza kuwa wiki moja, akavumilia tu Wizara itakapokuja kuwasilisha taarifa hii mbele ya wananchi na mambo yote yatakayojitokeza yatakuwa yameamuliwa wakati huo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bura, swali la nyongeza!

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mgogoro uliopo kati ya Wananchi wa Buger na Hifadhi ya Taifa ya Manyara ni sawasawa na mgogoro uliopo kati ya Hifadhi ya Mkungunero na

wananchi wa vijiji 11 vya Wilaya ya Kondoa. Katika mgogoro huo wananchi wameuawa, Askari wa Hifadhi ya Mkungunero wamekufa na mgogoro huu ni wa muda mrefu na tumeiomba Serikali washughulikie mgogoro huo na wananchi wanaomba kilometa 50 tu ili mgogoro umalizike.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mawaziri waliopita wametembelea na wamefanya mikutano na wananchi wa vijiji 11 wa Wilaya ya Kondoa pamoja na Chemba. Je, Mheshimiwa Waziri ni lini mgogoro wa wananchi wa Wilaya ya Kondoa, vijiji 11 utaisha kati ya Hifadhi ya Mkungunero na wananchi hao?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kujibu swali la nyongeza kuhusu Mbuga ya Mkungunero. Wizara yangu pamoja na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, imeandaa mpango wa kupima maeneo yote ambayo yana mgogoro kati ya wananchi na Hifadhi za Taifa ili kufanya juhudi za kutatua matatizo haya moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia nichukue fursa hii kutoa jibu la nyongeza kwa swali la nyongeza ambalo limetolewa na Mheshimiwa Cecilia Paresso kuhusu kijiji cha Buger na Pori la Manyara. Katika Mkutano ambao tumeuandaa na wananchi wa Buger, tumeandaa kutatua matatizo yote ambayo yameelekezwa katika ripoti ile. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Paresso kwamba fedha zilizoahidiwa na Mheshimiwa Waziri zitatolewa mara fedha zitakapopatikana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbunge hapo!

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona. Migogoro ya ardhi kati ya hifadhi zetu na wananchi wanaozunguka hifadhi imekuwa ni migogoro ya muda mrefu na imeenea katika nchi nzima. Katika Jimbo langu la Liwale sisi ni miongoni mwa tuliozungukwa na Hifadhi ya *Selous.*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao mgogoro mkubwa sana kati ya hifadhi ya *Selous* pamoja na Kijiji cha Kikulyungu wakigombea bwawa la Kihurumila. Mgogoro huu umeshapoteza maisha ya watu kwa muda mrefu na hata Mbunge aliyepita wa Jimbo la Liwale mgogoro huu umemfanya asirudi tena Bungeni pale alipotamka Bungeni kwamba anasikia watu wamefariki katika bwawa hilo, badala ya yeye kwenda kujiridhisha na kuangalia hali halisi ya mgogoro huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini basi Mheshimiwa Waziri atashiriki katika kutatua mgogoro huu ili maisha ya watu wa Liwale yasiendelee kupotea wakigombea bwawa la Kihurumila? Naomba majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo amemaliza kuuliza Mheshimiwa Mbunge hivi punde. Waheshimiwa Wabunge karibu wote wanaopakana na hifadhi wakisimama hapa watazungumza matatizo yanayofanana kuhusiana na suala la mipaka baina ya hifadhi na wananchi wanaoishi jirani nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niseme tu kwa jibu la ujumla ili kila mmoja ajiandae kupokea matokeo katika hili. Ni kwamba Serikali ya Awamu ya Tano ambayo inatekeleza Ilani ya CCM ya Uchaguzi ya mwaka 2015 - 2020, imejipanga vizuri kwa kuweka suala hili baada ya kuliona kuwa ni tatizo kubwa sana; imejipanga vizuri kwa kuliweka waziwazi kwenye Ilani yake na imesema hivi:

"Katika kutatua migogoro hii, Chama kitaendelea kusimamia Serikali yake kuhakikisha kwamba, kinaendelea kujenga mahusiano mema baina ya Hifadhi za Taifa na wananchi wanaoishi karibu na hifadhi hizo kwa namna ambayo wananchi hao watanufaika na uwepo wa hifadhi hizo."

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia, Ilani hiyo hiyo ukurasa wa 23 mpaka 25 inasema:

"Tutasimamia zaidi katika kutatua migogoro ya mipaka kati ya wananchi na maeneo ya jirani na hifadhi kwa kushirikisha wadau katika kuhakiki mipaka ya maeneo ya hifadhi kwa kuweka alama za kudumu, kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi na kuzingatia utawala wa sheria katika kusimamia rasilimali za maliasili."

Sasa hata wale wanaoingilia katikati ninavyozungumza, pengine wanataka kusema kwamba, hilo ndilo lililoandikwa, lakini wanasubiri utekelezaji. Sasa nataka niseme kwamba, Serikali ya Awamu ya Tano imejipanga sasa kutekeleza kwa vitendo haya ambayo nimeyasema, kama ambavyo yamekuwa yakisemwa siku zote, lakini sasa hivi tumejipanga vizuri zaidi katika utekelezaji.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa migogoro iliyozungumzwa katika hifadhi haitofautiani na malalamiko ya muda mrefu yanayotolewa na Jumuiya za Wapagazi, Waongoza Watalii na Wapishi katika Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro na hifadhi nyingine za Taifa, wakigombana au wakilalamikia *Tours Operators* wao.

Je, Serikali kwa sababu, inalifahamu hili, ni lini itatatua migogoro hii ili maslahi na mazingira ya kikazi ya Jumuiya hizo za Wapagazi, Waongoza Watalii na Wapishi yaweze kuboreshwa, kama mabalozi wema wa kustawisha utalii katika nchi yetu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri lenye mwelekeo wa kuboresha zaidi huduma kwenye sekta ya utalii huku tukitambua wote kwamba, utalii unaongoza katika kuliingizia Taifa hili fedha za kigeni. Si zaidi ya wiki mbili nilikuwa *KINAPA* pale *Kilimanjaro National Park,* lakini baada ya pale niliungana na Mheshimiwa Waziri, Arusha Mjini ambako tulikutana na Vyama vya Watoa Huduma wote kwenye Sekta ya Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, zilijitokeza changamoto nyingi, mojawapo ilikuwa ni hiyo na kwamba, sasa Serikali tayari imeshaweka jedwali la changamoto zote hizo ambazo zimezungumziwa na sasa tumejipanga kuhesabu moja baada ya nyingine ili kuweza kupata majawabu na kuweza kutatua migogoro hiyo na matatizo hayo ili tuweze kuboresha Sekta ya Utalii.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tuendelee na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake!

Na. 37

Benki ya Wanawake Kutoa Huduma Zanzibar

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR aliuliza:-

Je, ni lini Benki ya Wanawake itaanza kutoa huduma zake Zanzibar?

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Faida kwa kufuatilia na kuuliza swali hili kwa mara ya tatu sasa. Hii

inaonesha dhamira ya dhati aliyonayo kwa wanawake na wananchi wa Zanzibar. Mheshimiwa Faida aliuliza swali hili mara mbili katika Bunge la Kumi na aliendelea kuuliza swali hilo kwenye vikao mbalimbali vya iliyokuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii katika kipindi kilichopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Wanawake ilianzishwa kwa mtaji wa shilingi bilioni 2.8 ambao ni kiasi kidogo sana. Ili Benki iweze kutimiza kigezo cha kuwa Benki ya Biashara kamili na kuweza kupata kibali cha Benki Kuu cha kufungua Matawi nchi nzima, inahitaji mtaji wa zaidi ya shilingi bilioni 15. Hivi sasa benki hiyo ina mtaji wa shilingi bilioni 8.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi za kuanzisha shughuli za kibenki Zanzibar zilianza tangu mwaka 2013, kwa Menejimenti kutembelea Zanzibar katika lengo lake la kupata jengo zuri kwa shughuli za kibenki. Hata hivyo, juhudi hizi hazikuzaa matunda na ndipo Makamu wa Rais wa sasa, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, aliporidhia kutoa Ofisi yake ndogo iliyokuwa katika Hoteli ya Bwawani ili kuanzisha huduma hiyo na kuwanufaisha wananchi wa Zanzibar, hususan wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa, benki ipo katika hatua za mwisho za kupata kibali cha Benki Kuu ili kuanzisha rasmi Kituo cha Mafunzo na Mikopo kwa Wajasiriamali wa Zanzibar na tunategemea kitaanza shughuli zake kabla ya mwezi Juni mwaka huu yaani mwaka 2016 na kama nilivyoeleza awali mtaji wa benki hii ukiimarika benki itafungua tawi kamili Zanzibar.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Faid Bakar, swali la nyongeza!

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri Kigwangalla, kwa niaba ya wananchi na wanawake wa Zanzibar, tunapenda kuishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuridhia kufungua Benki ya Wanawake, Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kumshukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kukubali kutoa ofisi yake. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa baadhi ya Wabunge wanawake wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tulikuwa ni miongoni mwa waanzilishi wa benki hii kwa kutoa hela zetu kuweka hisa, lakini mpaka hii leo hatujui chochote kinachoendelea na hatujapatiwa gawio la hisa kutokana na Benki hii ya Wanawake.

Je, Serikali itaanza lini au inasema nini kuhusu gawio letu la hisa la wananchi wote, sio lazima Wabunge tu na wananchi wote? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kabla sijajibu swali lake, nitumie nafasi hii kwa namna ya kipekee kumpongeza sana aliyekuwa Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Sophia Mnyambi Simba, kwa chachu ya kuanzisha benki hii. Pia nimpongeze aliyekuwa Naibu Waziri wa Wizara hiyo ambaye sasa ni bosi wangu, Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu, kwa kutia chachu ya kukua kwa kasi ya benki hii. Zaidi nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kujitolea kufanya uamuzi makini wa kuchangia mtaji kwenye benki hii wa shilingi bilioni mbili kila mwaka. Naamini Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ataendelea kuipa uwezo benki hii kwa kuendelea kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niwapongeze Wabunge wote wa Viti Maalum ambao nao kwa dhati kabisa waliamua kujitolea michango kwa kununua hisa kwenye benki hii. Kilichokwamisha wao kupata hisa hizi rasmi kwa maana ya utaratibu wa kisheria ni kwamba wakati benki inaanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002, *Cap. 212*, ilikuwa imesajiliwa kama *Private Limited Company*. Kwa maana hiyo ilikuwa na benki binafsi ya wanahisa binafsi ambao walikuwa wameteuliwa kuianzisha benki hiyo na Mheshimiwa Rais wa wakati huo na kwa maana hiyo Wabunge walipochangia michango ile kwa maana ya kununua hisa kwa ajili ya kujiunga kwenye benki hii haikuweza kurasimishwa kwa haraka kwa sababu ya utaratibu wa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumbukumbu za Wabunge wote walionunua hisa pale awali wakati benki inaanzishwa zipo. Machi, 2012 baada ya kutambua michango hii ya Waheshimiwa Wabunge wote wa Viti Maalumu bila kujali itikadi zao, ilionekana kwamba usajili wa benki kwa mujibu wa sheria ubadilike, badala ya kuwa *private* sasa iwe *public* kwa maana ya kuwa *Public Limited Campany* ambapo kwa mujibu wa sheria sasa inaruhusiwa kuongeza wanahisa wengi zaidi. Lakini benki imeenda mbele, sasa hivi itakuwa benki ya wananchi wote kwa maana ya kwamba tuna mkakati wa ku-*issue IPO,* kufanya *Initial Public Offering* kwenye Soko la Hisa ili wananchi wengi zaidi wanunue hisa na iweze kuwa na mtaji mkubwa na kufika kwa wananchi wengi zaidi. Kwa

maana hiyo, wale Wabunge walionunua hisa wakati huo, watapewa hati rasmi za hisa zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupewa hati rasmi za hisa na wananchi wengine watakaonunua hisa nao pia watapewa hati za hisa hizo. Sasa benki kwa kuwa imeanza kupata faida kuanzia mwaka jana na mwaka huu, itaweza kutoa gawio. Huo ulikuwa ni utaratibu wa kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakusukuru kwa kunipa nafasi hii.

(Hapa Waheshimiwa Wabunge kadhaa walisimama kwa nia ya kuuliza maswali ya nyongeza)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae. Tuna taarifa kwamba Kivuko cha Mto Kilombero kimezama na vyombo vya dola viko huko vitatuletea taarifa baadaye pengine kwenye mchana hivi tutakapokutana tutaweza kuambiwa taarifa za awali zilizopo huko.

Waheshimiwa Wabunge, nichukue nafasi hii kuwapa pole wale wote ambao wameumia na wale ambao wamepoteza ndugu zao.

Waheshimiwa Wabunge, nichukue pia fursa hii kumkaribisha Waziri aweze kutoa ufafanuzi zaidi juu ya jambo hili. Mheshimiwa Waziri, karibu.

WABUNGE FULANI: Maswali hayajaisha.

NAIBU SPIKA: Maswali hayajaisha tutaendelea nayo kipindi kijacho.

KAULI YA SERIKALI

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mhehimiwa Waziri Mkuu, kwa masikitiko makubwa, naomba nitoe tu taarifa ya awali kuhusiana na taaarifa ambayo Mheshimiwa Naibu Spika umeitoa hapa na umesema meza yako imeipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepokea taarifa usiku wa jana kuamkia leo kwamba Kivuko cha Kilombero kimepata ajali na kuzama. Kwa maelezo ya awali kulikuwa na abiria 31 ambapo abiria 30 walishaokolewa. Hata hivyo, kivuko hicho kilikuwa magari matatu na bajaji mbili kwa taarifa za awali. Hali ya mawasiliano ya barabara kupitia kivuko hicho yamekatika na kuacha kutokuwepo kwa kmawasiliano kati ya Wilaya ya Kilombero na Ulanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwaambie Watanzania jitihada za uokozi zilianza toka jana katika maafa hayo yaliyotokea ili kuhakikisha kwamba abiria, mali na hasa maisha ya abiria yanaokolewa kwa haraka. Kamati zote za Ulinzi na Usalama katika ngazi ya Wilaya na Mkoa, vilevile taasisi zinazoshughulika na masuala ya maafa katika ngazi ya mkoa zimeendelea kushughulikia suala hilo kwa guvu zote. Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasilianao aliondoka toka jana usiku kwa agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu kuelekea eneo la tukio kwa kazi maalum ya usimamizi na uongozi wa uokoaji katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, timu za utendaji za Serikali ziko kazini katika kushughulikia tatizo hilo la maafa lakini hasa pia kuona ni namna gani tunaweza kurudisha mawasiliano ya Wilaya hizo mbili, hii ni pamoja na kulishirikisha Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania kuona wanaweza kutoa msaada gani wa haraka ili wilaya hizo mbili zirudishe mawasiliano kwa haraka. Nawaomba Watanzania watulie, Serikali toka ilipopokea taarifa hiyo jana imekuwa ikifanya kazi kubwa ya kuona nini kifanyike kwa wakati gani ili kuweza kutatua tatizo la janga la maafa hayo yaliyotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutoa taarifa ya tukio hilo mara kwa mara ili Watanzania wajue hatua zinazochukuliwa na zitakazoendelea kuchukuliwa katika maafa hayo.

Niendelee kutoa wito kwa wananchi wote wa Tanzania, nchi yetu inatabiriwa kuwa na mvua nyingi na huenda tukapata upepo na dhoruba za namna tofauti, kwa hiyo tuendelee kuchukua tahadhari katika maeneo tuliyopo ili kuweza kusaidiana kuepusha maafa yanayoweza kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kutoa wito kwa Kamati za Maafa kwenye ngazi ya Kata, Wilaya, Mkoa kuendelea kushirikiana na Kamati ya Maafa ya Taifa ili kuona ni namna gani tunaanza kuchukua tahadhari lakini vilevile panapotokea maafa tupeane taarifa za haraka kuhakikisha kwamba tunachukua hatua na kuokoa maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tumepokea taarifa hiyo na tunatoa pole sana kwa wale wote waliokumbwa na kadhia hiyo kwa namna moja ama nyingine na tutaendelea kutoa taarifa ya tukio hili. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Spika akisimama mnapaswa kukaa, tafadhali. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba ukae, Spika akisimama unakaa, ndiyo Kanuni zinavyosema.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamruhusu Mheshimiwa Waziri kutoa hiyo taarifa ya ufafanuzi nilisema Kipindi cha Maswali kimesitishwa na maswali yataendelea kipindi kijacho kwa maana ya kesho asubuhi kwa sababu ya muda uliopo.

Niwatangaze wageni waliopo pamoja na sisi asubuhi hii. Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, kundi la kwanza ni wageni watatu wa Mheshimiwa Deo Sanga, Mbunge wa Jimbo la Makambako – Njombe. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wageni sita wa Mheshimiwa Ali Hafidh Tahir, Mbunge Jimbo la Dimani, wakiongozwa na Sheikha Mohamed ambaye ni mke wake. *(Makofi)*

Kundi lingine ni mgeni mmoja wa Mheshimiwa Njalu Silanga, Mbunge Jimbo la Itilima, Ndugu Nestory Kubilu.

Wageni wengine ni wageni watatu wa Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini wakiongozwa na Ndugu Kala Jeremiah. *(Makofi)*

Katibu!

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI: Mwongozo wa Spika.

HOJA ZA SERIKALI

NDG. JUSTINA M. SHAURI – KATIBU MEZANI: Hoja ya kujadili hotuba ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa wakati wa ufunguzi wa Bunge la Kumi na Moja, tarehe 20 Novemba, 2015

(Majadiliano Yanaendelea)

MHE. PETER A.P. LIJUALIKALI: Mimi ni Mbunge wa Kilombero, nataka Mwongozo.

NAIBU SPIKA: Naomba ukae. Mheshimiwa Ester Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) lakini nitaisoma sanjari na Kanuni ya 63(1). Kanuni ya 68(7) inaeleweka naomba nisome Kanuni ya 63(1), inasema:- "Bila kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, ni marufuku kabisa kusema uongo Bungeni na kwa sababu hiyo, Mbunge yeyote anapokuwa akisema Bungeni ana wajibu wa kuhakikisha kwamba anatoa kauli au maelezo kuhusu jambo au suala ambalo yeye mwenyewe anaamini kuwa ni la kweli na siyo jambo la kubuni au la kubahatisha tu".

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Waziri Mkuu akijibu swali la Mheshimiwa Pauline Gekul kuhusiana na elimu bure ambapo Mheshimiwa Gekul aliainisha hususani kwenye eneo la chakula, Mheshimiwa Waziri Mkuu alilieleza Bunge lako Tukufu kwamba maeneo ambayo Serikali imeyachukua ni ada ya shilingi 70,000 kwa shule za bweni akataja na chakula. Pamoja na kwamba dhana nzima ya elimu bure haikidhi hizo fedha ndogo ambazo wamewaondolea Watanzania, lakini napenda kusema kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu aidha amebahatisha au hajapata maelezo ya kutosha kuhusiana na shule za bweni hapa Tanzania na nalisema hili hususani kwenye Jimbo langu la Tarime Mjini, Shule ya Sekondari ya Mogabili ina shule ya bweni na kutwa lakini watoto wa bweni wametakiwa waende na vyakula shuleni. Wanaambiwa waende na magunia ya mahindi, mchele na maharage.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nipate Mwongozo wako ni kwa nini Waziri Mkuu anatoa kauli ambayo hana uhakika nayo, atueleze ni kwa nini baadhi ya shule za bweni bado wanawaambia Watanzania wapeleke vyakula unakuta mwisho wa siku gharama ni zaidi ya shilingi 500,000 na bado mnasema elimu ni bure. Napenda kujua kuhusu hilo. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka Waziri wa TAMISEMI, Vikao vya Bunge vilipoanza na kwa kurudia pia alitoa maelezo kwamba huu ni mwanzo na ziko changamoto ambazo zimekusanywa Wizara inazifanyia kazi. Hayo maelezo amekuwa akiyatoa mara kwa mara. Mimi nadhani tukubaliane kwamba elimu ni bure ndiyo lakini ziko changamoto kadhaa ambazo zimetokea maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Wewe ni Serikali?

(Hapa Waheshimiwa Wabunge kadhaa walikuwa wakizungumza bila mpangilio)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba tuelewane, hakuna Kanuni inayosema kwamba Spika akiwa anaongea unatakiwa kumjibu kwa namna mnavyojibu. Tafadhali Waheshimiwa Wabunge, wote hapa nawaona. Mheshimiwa Lema tafadhali, wewe ni Mbunge wa siku nyingi siyo mgeni, unazijua taratibu. Nimeombwa Mwongozo ndiyo natoa majibu yake.

Waheshimiwa Wabunge, maelezo niliyotoa ndiyo mwongozo wa jambo hilo, tunaendelea na uchangiaji.

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na uchangiaji.

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo.

NAIBU SIPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Silinde, wote mnazijua taratibu, bado nimesimama na ninyi mnasimama. Haya mwongozo nimekwishatoa tunaendelea na uchangiaji.

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nimesema hivi tuendelee na uchangiaji, tafadhali naomba mkae. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Utakataaje Miongozo?

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge
walikuwa wamesimama kuomba Mwongozo)

NAIBU SPIKA: Tafadhali naomba mkae tuendelee na uchangiaji, Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama.

(Hapa Waheshimiwa Wabunge wa Upinzani walitoka
nje ya ukumbi wa Bunge)

NAIBU SPIKA: Waheshimia Wabunge, tutulie wakati Wabunge wengine wanatoka.

MBUNGE FULANI: Mmeshasaini.

MBUNGE FULANI: Haikuhusu.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na uchangiaji kwa muda huu uliobaki halafu mwisho nitaleta matangazo mengine yako hapa. Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama.

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda nimshukuru sana Mwenyenzi Mungu aliyenijalia wakati huu kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia kwa unyenyekevu mkubwa sana niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Madaba ambao kwa umoja wao wamenituma nifanye kazi yao wakiamini kwamba nitawatendea haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kupongeza sana hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa kwa Bunge lako Tukufu. Hotuba hii imejaa hekima kubwa lakini pia imejaa matumaini makubwa sana kwa wananchi wa Tanzania na hasa kwa wananchi wa Jimbo langu la Madaba. Hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa sehemu kubwa imetoa mwelekeo wa Taifa letu kwa kipindi cha miaka mitano. Kwa hakika hotuba yake imeshakwishaanza kutafsiriwa kwa vitendo kupitia utekelezaji wa kazi hizo, lakini pia kwa kupitia Baraza lake la Mawaziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Mawaziri wote wa Awamu ya Tano, wanafanya kazi kubwa kwa ajili ya Watanzania. Kwa namna ya pekee sana naomba sana niwashukuru sana Mawaziri ambao tayari wameshakuja kwenye Jimbo langu na tayari wameanza kufanya kazi na wananchi wa Jimbo langu. Kwa namna ya pekee nimshukuru Mheshimiwa Ummy Mwalimu, tayari amekuja kuangalia changamoto za afya na sasa yupo kwenye mchakato wa kuhakikisha kwamba tunapata hospitali ya Wilaya, tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa heshima kubwa nimshukuru sana Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo, Waziri wa Nishati na Madini katika mazingira magumu na muda mgumu alifika katika Jimbo langu kuangalia changamoto ya umeme na kuipatia majibu pale pale. Namshukuru na kumpongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchangiaji wangu nitajikita katika maeneo machache muhimu yanayohusu maslahi ya Taifa letu. Moja ni eneo la viwanda. Katika hotuba ya Mheshimiwa Rais toka ukurasa wa 13 – 16 anaeleza ni namna gani Serikali ya Awamu ya Tano imejipanga kuifanya sekta ya viwanda iwe sekta mama itakayotoa ajira za uhakika kwa Watanzania. Mheshimiwa Rais anakwenda mbali zaidi na kueleza namna gani hiyo sekta ya viwanda inakwenda kujibu matatizo ya masoko ya mazao, mifugo pamoja na uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta hii kwa uzito ambao Mheshimiwa Rais ameupa na kwa hali halisi ya Tanzania ni sekta muhimu sana. Nitumie nafasi hii

kupongeza hatua ya Mheshimiwa Rais kuzingatia viwanda lakini naomba nitoe tahadhari kwa wale ambao wamepewa kusimamia utekelezaji wa jukumu hili. Moja, lazima tujue kwamba sekta ya viwanda ina mahusiano makubwa sana na sekta ya biashara lakini pia kwa sababu hivyo viwanda vinahusu kilimo, uvuvi na mifugo, sekta hizi zote zinafanya kazi kwa karibu sana. Sera ya kuimarisha viwanda ndani ya Tanzania siyo sera ngeni, kigeni katika Awamu hii ya Tano ni mikakati mipya ambayo Mheshimiwa Rais amekuja nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tujifunze ni nini kilisababisha viwanda vyetu vya miaka ya 1980 na 1990 na kuelekea mwaka 2000 vikafa. Mikakati ya ndani ni mizuri, mitaji ilipelekwa lakini naomba wanaohusika na maandalizi na usimamizi wa eneo hili wakubali kurudi tena kwenye kusoma uzoefu hasa unaogusa sera zetu za nje, mikataba yetu na makubaliano ya kibiashara na mataifa mbalimbali zikiwemo jumuiya mbalimbali zenye maslahi ya kibiashara na Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukifuatilia kwa undani pamoja na jitihada za ndani za kuzalisha mazao ya viwandani, mazao yetu yameendelea kukosa soko kwa sababu tumefungulia kiholela mazao ya viwandani yanayotoka mataifa mengine. Ndani ya Mkoa wa Ruvuma nimepambana sana kwa miaka zaidi ya sita kuhakikisha kwamba sekta ya mazao ya mafuta yakiwemo alizeti inakuwa sekta tegemezi kwa uchumi wa Mkoa wa Ruvuma kwa kuhakikisha kwamba tunazalisha mafuta ya kula ya kutosha yatakayoweza kukidhi mahitaji ya mkoa. Hata hivyo, jitihada hizo zimeangamizwa na mafuta ya bei rahisi yanayoingizwa toka Malaysia na nchi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hilo eneo halitaangaliwa vizuri, Watanzania tutaenda kuwekeza kwenye viwanda na tutafilisika na tutabaki maskini wa kutupwa kwa sababu Tanzania mpaka sasa imeendelea kuwa soko kubwa la mazao ya viwandani yanayotoka nchi zingine. Kwa hiyo, nashauri sera yetu inayohusiana na maeneo hayo iangaliwe vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ni mama kwa uchumi wetu ni kilimo na mifugo. Niishukuru sana Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Waziri Mwigulu na timu yake wananchi wa Madaba kwa namna fulani wamefaidika sana na Wizara hii kwa asilimia 75 ya wakazi wake kufanikiwa kupata pembejeo za ruzuku.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo huu wa ruzuku siyo endelevu. Msimu wa mwaka jana wananchi wa maeneo yale hawakupata pembejeo za ruzuku iliathiri sana uzalishaji wao. Najua mfumo huu umechukua uzoefu kutoka Malawi na maeneo mengine na hapa tunau-*apply*. Naomba Wizara inayohusika na kilimo na mifugo tuchukue hatua za makusudi kujifunza mifumo mingine inayopendekezwa na wadau mbalimbali wa kilimo. Najua kumekuwa na miradi

mbalimbali ya wadau wa kilimo inayojaribu mifumo mbalimbali ya kuhakikisha kwamba wananchi wanapata pembejeo kwa namna endelevu. Naomba sana Wizara hii iandae utaratibu maalum wa kufanya utafiti wa mifumo inayofaa. Mfumo huu hauna uendelevu kwa sababu unategemea asilimia 100 ruzuku ya Serikali, ruzuku ambayo hatuna uhakika nayo. Kuna mifumo ya kuwaunganisha wasindikaji, wanunuzi wa mazao, wasambazaji pembejeo pamoja na vikundi vya wakulima kwa kupitia mfumo wa mikataba ambayo itawasaidia kupata mikopo ya pembejeo, uhakika wa masoko ya kilimo na uhakika wa uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maeneo mengi nyeti yanayowagusa wananchi wa Jimbo la Madaba, eneo la soko la mazao ni mgogoro sana kwa sababu mpaka sasa tunategemea Serikali pekee kununua mahindi kupitia *NFRA*. Nashukuru sana Wizara ya Kilimo wamefanya jitihada kubwa sana kukarabati maghala ya kuhifadhia mazao wakati wa mavuno. Hata hivyo, maghala yale yametengenezwa kwa pesa za wakandarasi, wakandarasi hawajalipwa, hawajamaliza na mwezi wa sita wananchi wanaanza kuvuna hawana mahali pa kuhifadhia mazao yao, tunaomba hilo nalo liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini eneo gumu sana kwetu Madaba ni maji. Wananchi wa Madaba hawana maji, Jimbo la Madaba ni jipya, Halmashauri ya Wilaya mpya, Makao Makuu maji ni mgogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Tutamsikiliza Mheshimiwa Mary Chatanda atafuatiwa na Mheshimiwa Goodluck Mlinga halafu atafuata Mheshimiwa Mwanne Ismail Mchemba. Mheshimiwa Mary Chatanda.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipatia nafasi nami niweze kuchangia hotuba ambayo aliitoa Mheshimiwa Rais alipokuwa anafungua Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu na kuwashukuru wananchi wa Wilaya ya Korogwe Mjini kwa kunipa nafasi ya kuwawakilisha katika Bunge hili Tukufu. Mwenyezi Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii vilevile kumpongeza Waziri wa Habari, Utamaduni, Wasanii na Michezo kwa nafasi aliyoitumia jana usiku kupitia vyombo vya habari alipotoa ufafanuzi juu ya jambo ambalo wenzetu wameamua kufanya upotoshaji wa makusudi kabisa. Ni ukweli usiopingika kwamba Waziri wa Habari, Utamaduni, Wasanii na Michezo ameeleza wazi nia na madhumuni ya Shirika letu la *TBC* kusitisha matangazo kwa maana ya kutaka

matangazo hayo yaweze kuelezwa katika muda muafaka ambapo wananchi wanaweza wakawa tayari wako majumbani wametulia na wanasikiliza vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika tumezungumzia sasa hivi kauli mbiu ya 'Hapa Kazi Tu' maana yake kila mtu anastahili kufanya kazi na masaa ya kufanya kazi ni kuanzia asubuhi saa kumi na mbili hadi saa tisa au kumi. Wafanyakazi wanakwenda ofisini asubuhi saa moja na nusu hadi saa tisa na nusu. Wakulima wanakwenda mashambani muda wao wa kurudi ni kuanzia saa kumi. Kwa hiyo, suala la *TBC* kufanya mabadiliko hawajakosea, tunazingatia hilo suala la 'Hapa Kazi Tu' kwamba kila mtu aende akafanye kazi akirudi baada ya muda huo atasikiliza matangazo ambayo yatakuwa yametolewa au mijadala ya Wabunge iliyotoka Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri wenzetu hawa ni vizuri wakawa wanatambua mambo muhimu ingawa wamezoea kupinga na sioni ajabu kwa sababu hata kipindi ambapo Serikali ilikuwa imetoa maelekezo kwamba usafiri wa mabasi usifanyike usiku watu walipinga lakini Serikali ilikuwa na nia njema na jambo hilo limeendelea kutekelezwa na linafanyika vizuri. Watu walikuwa wanatekwa kwenye mabasi usiku ule, lakini sasa hivi hali imekuwa ya utulivu na amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi ya kupongeza hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Tanzania aliyoitoa wakati ule akizindua Bunge letu. Hotuba hiyo ilikuwa na mvuto mkubwa wa aina yake na iliweza kukonga mioyo ya Watanzania wakiwemo hata wenyewe wa Upinzani. Kwenye maeneo yetu tunaishi na wapinzani, baada ya hotuba ile wapinzani wengi walishabikia na kusifu hotuba ya Rais wetu. Kwa hiyo, hata kile kitendo cha wenzetu tokea juzi walipokuwa wanaambiwa kwa nini wachangie wakaingiwa hofu kwamba kwa nini mnataka kuwatoa walikuwa wanakiri kwamba hotuba iliyotolewa na Mheshimiwa Rais ni nzuri hawakujitambua wakati ule ndiyo maana waliamua kutaka kubaki sasa kuendelea kuchangia. Hili dhoruba lililowapata ni jambo dogo tu lakini ni matarajio yangu kwamba wenzetu hawa tuko pamoja katika hii hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa hatua ambazo ameanza kuzichukua ikiwa ni pamoja na kubana matumizi na kuwachukulia hatua wale wote ambao hawakuwajibika vizuri katika utendaji wao. Kila mwananchi hivi sasa ikishafika kipindi cha taarifa ya habari saa moja, saa mbili, hata kama mtu hana *TV* anakimbia kwa jirani yake kwenda kusikiliza leo kunafanyika kitu gani, leo Rais atasema nini, leo Mawaziri watasema nini, jinsi walivyokuwa na hamu na utekelezaji wa hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niendelee kupongeza sana jitihada za Mheshimiwa Rais ambazo ameshaanza kuzichukua. Nawapongeza pia Mawaziri kwa kazi nzuri ambayo na wenyewe wameanza kufanya kazi, msirudi nyuma kazeni buti. Achene kuwasikiliza watu wachache wanaosema inawezekana huu ni moto wa kifuu, huu siyo moto wa kifuu utaendelea kuwaka na hautazimika ili kuweza kuwaletea maendeleo wananchi wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nieleze juu ya kauli ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba Tanzania yenye viwanda inawezekana. Mimi nafikiri kauli hii ya Mheshimiwa Rais ya Tanzania na viwanda inawezekana, itawezekana endapo tutaondokana na urasimu ambao unazaa rushwa. Wapo wawekezaji wengi ambao wanapenda kuwekeza katika nchi yetu, lakini wanapofika kwenye ofisi zetu za Serikali wanakutana na urasimu mkubwa. Urasimu ule unaashiria rushwa. Rais wetu amesikitishwa sana na suala la rushwa lililoko serikalini. Kwa hiyo, niwaombe ndugu zangu suala la urasimu tukiliacha Tanzania ya viwanda inawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono vilevile kauli ya Mheshimiwa Rais ya kukemea suala la rushwa. Shughuli zetu hata kwenye Halmashauri zetu zimeingiliwa sana na suala la rushwa hasa kwenye kitengo hiki cha ugavi, cha ukusanyaji wa mapato, watu wanafanya vile ambavyo wanataka wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe basi Waziri anayehusika kwenye hizi Serikali zetu za Mitaa, hebu tuingie kwenye vitengo hivi vya ugavi na ukusanyaji wa mapato, watu hawa wanatusababishia Serikali kukosa mapato katika Halmashauri zetu. Wanatumia vitabu vya aina mbalimbali katika ukusanyaji wa mapato, wanakubaliana na wafanyabiashara hawawatozi ushuru ambao unatakiwa. Kwa hiyo, niombe sana kama tunatumbua majipu hebu sasa tufike mpaka huku chini kwenye hizi Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la elimu. Suala la elimu bila malipo ni mpango mzuri ambapo wananchi wameufurahia sana. Nitoe ushauri kwenye Serikali mpango huu uende sambamba na kuwajengea mazingira bora walimu. Bila kuwajengea mazingira bora walimu mpango huu unaweza ukasuasua. Walimu wana matatizo mengi, wanatakiwa waandaliwe mazingira kama vile vitendea kazi, nyumba za kuishi, kuwalipa stahiki zao zile ambazo wanadai ikiwa ni pamoja na malimbikizo ya likizo.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Chatanda muda wako umekwisha.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Sasa tumsikilize Mheshimiwa Goodluck Mlinga, hayupo, Mheshimiwa Mwanne Mchemba.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hotuba iliyopo mbele yetu ya Mheshimiwa Rais wetu mpendwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe masikitiko yangu kidogo au nitoe angalizo, nisamehewe kwa sababu nina mafua, nina *flu* kali kwa hiyo sauti yangu inawezekana isisikike vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais ni hotuba ambayo imekonga mioyo ya watu, ni hotuba ambayo mjadala wake ni wa kumsifia tu. Kwa nini nasema hivi? Hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati anaitoa hiyo tarehe 20 Novemba alichokuwa anakazia ni yale aliyoyafanya wakati wa kampeni yake. Kampeni yake imezunguka Tanzania nzima na kila eneo, yale aliyoyasema alikuja kuwasilisha kwenye Bunge ili Serikali yake iweze kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais kwa kuwa alikuwa anakerwa sana na umaskini wa nchi hii aliona ni afadhali ajionee mwenyewe yale ambayo alikuwa anayasikia. Kila eneo alilokwenda wamempa malalamiko yake ambayo Kata, Wilaya au Jimbo lile linahusika, kwa hiyo, ni pongezi kubwa sana kwake. Lakini si hilo tu hotuba yake haikuchagua imegusa makundi yote. Wakati anaunda Baraza lake la Mawaziri ametambua hilo akaunganisha Wizara ili ufanisi wa ahadi zake uwe karibu na wananchi, kwa hiyo, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia kwa kuokoa muda, nianze na huduma ya afya. Nimpongeze sana Naibu Waziri wa Afya, alikuja katika hospitali yetu ya Kitete, akajionea hali halisi lakini baada ya hapo aliweza kuchukua majukumu mengine na akaweza kutoa ahadi. Hospitali ya Kitete ambayo iko Mkoa wa Tabora ina changamoto nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya kwanza, hospitali ile inaitwa ya Hospitali ya Rufaa lakini hivi navyoongea hatuna madaktari bingwa. Inawezekana tatizo hilo ni la Mkoa wa Tabora lakini pia inawezekana ni nchi nzima. Tuna upungufu wa Madaktari Bingwa hususani upande wa *gynecologist*, akina mama wengi wanateseka lakini madaktari bingwa wa mifupa hawapo. Mimi niombe, kwa kuwa Hospitali ya Kitete ya Rufaa kwa wilaya zake saba

ambazo ziko katika mkoa ule, niiombe Serikali itekeleze au angalau basi tuwe na madaktari ambao wanaweza wakawa na fani hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo katika hospitali ile tuna tatizo kubwa la mashine za kufulia nguo yaani *laundry*. Tatizo hilo linatokana na ongezeko la wagonjwa linalofanya ongezeko la nguo au mashuka kuwa kubwa. Mashine ile ina miaka zaidi ya 30. Hatujaletewa mashine ya kisasa ya kufulia nguo za wagonjwa, ukienda pale ni taabani. Ukiangalia mashuka hata upeleke leo, kesho halitakuwa katika hali nzuri. Kwa hiyo, naomba Serikali ya Chama cha Mapinduzi iangalie sekta hiyo ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna tatizo kubwa la madai ya wafanyakazi ingawa ni kidogo lakini ni mali yao. Niiombe Serikali, haya malimbikizo ya wafanyakazi inawavunja moyo ni lazima mtu alipwe kile ambacho amekifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vifaa tiba ni tatizo sana hasa kwa wodi ya akina mama. Kile kiwanda hakuna asiyekipitia hususani wanawake, ni kiwanda kigumu. Nashukuru Serikali angalau sasa hivi inapunguza vifo vya akina mama na watoto lakini huduma zingine bado zinalinganishwa na huduma za kawaida. Kwa hiyo, nashauri Serikali ya Chama cha Mapinduzi iangalie kwa jicho la huruma wodi za wanawake nchi nzima na hususani vijijini hakuna *gloves,* hakuna sindano, huyo mama unayemwambia *gloves* hazijui na wala maana yake pia haijui. Anachojua yeye ni kuongeza uzalishaji, tumeambiwa sisi tuongeze dunia. Kwa hiyo, niombe na nitoe angalizo kwa Wizara ya Afya iangalie ni jinsi gani inaweza kutusaidia kwa tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, si hilo tu, nimpongeze Mheshimiwa Rais, kazi aliyofanya pale Muhimbili kupitia Kitengo cha *MSD* ni sifa kubwa, ni kazi nzuri, ameokoa mamilioni ya watu ambao wangekufa wasiokuwa na uwezo wa kwenda kununua dawa kwenye maduka ya watu binafsi. Kwa hiyo, niombe hospitali za Mikoa, Wilaya *MSD* wasogeze huduma pale ili angalau watu wa kawaida waweze kununua dawa kwa bei nafuu. Kwa hiyo, vifaa tiba, nadhani navyo viwe ni angalizo kwa kumsaidia Rais wetu kama mfano uliotolewa Muhimbili sasa hivi kila anayesimama pale anazungumzia habari hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni ahadi ya Mheshimiwa Rais ya shilingi milioni 50 kila kata au kila kijiji. Wakati wa mfuko wa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete wapo wajanja walichakachua wakafanya ile miradi kama ni yao wakafungua *SACCOS* zao. Ombi langu kwenye pesa hizi, ifuate na iangalie vikundi vya akina mama lishe, vikundi vya kilimo, vikundi vya walemavu, vikundi vya wajane na vikundi vya *VICOBA*. Kwa kufanya hivyo, fedha alizosema Mheshimiwa Rais shilingi milioni 50 watafaidika wananchi wengi, nchi hii ina wajanja wengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ameelezea kuhusu ushuru mdogo mdogo, ni kero kwa akina mama, mtu anadaiwa Sh.200. Kwa hiyo, naomba hiyo nayo iwe angalizo kwa wale ambao watasimamia mfuko huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie habari ya barabara, ingawa Wabunge wote wa Tabora na mikoa mingine ya jirani wamezungumzia habari ya barabara. Barabara ya Chaya inaharibu utamu wa barabara yote na kazi zote zilizofanyika kutoka Itigi – Tabora, ni kilomita chache sana. Naomba Waziri mhusika atusaidie kwa hili. Tunazunguka tunahangaika, kilometa zinazozidi ni nyingi na walalahoi hawawezi kuzunguka kwa sababu bei inakuwa kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara ya Urambo – Kaliua, ni kilometa 32 tu kuunganisha. Watu wanapata taabu kutoka Kigoma wakifika Kaliua wanatumia saa nyingi wanaichukia na Serikali yao. Kwa hiyo, naomba sana hilo liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna barabara ya Sikonge. Naomba Waziri twende naye huko akaione barabara ya Sikonge inayokwenda Mpanda, kama atarudi amevaa hata koti, hawezi, wananchi wanateseka. Kwa hiyo, naomba barabara ya Tabora – Sikonge nayo ishughulikiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara nyingine ambayo inaunganisha Majimbo mawili, barabara ya Puge – Ndala – Simbo – Nkinga - Ziba ambayo inakwenda kwenye barabara kuu inayokwenda Singida, hii nayo ni kilometa chache. Naomba nayo waiweke katika mipango yao ili ikiwezekana twende pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kufufua viwanda, wamepewa miezi sita, kiwanda cha kwanza nchi hii kinachowadhulumu wananchi ni Kiwanda cha Nyuzi cha Tabora, ni mateso. Kiwanda kile Mbunge aliyepita Mheshimiwa Mzee Msigalo alitoa shilingi ndani ya Bunge hili.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, basi baada ya hapo, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais, mengine nitaandika kwa mkono, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimetaja orodha ya Wabunge wanaofuata kuchangia lakini naona matangazo yanazidi kuwa mengi hapa, naomba niyasome kwa haraka halafu tuendelee.

Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni wa Mheshimiwa Spika waliopo *Speakers Gallery*, ni Mheshimiwa Balozi Yasemin Eralp, Balozi wa Uturuki nchini Tanzania, akiambatana na Naibu Balozi wake Mheshimiwa Berat Colak. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tangazo lingine Wabunge wote wa Mkoa wa Kigoma mnaombwa kukutana saa saba mchana katika *lobby* ya Jengo la Utawala. Tangazo limetolewa na Mbunge wa Kasulu Mjini, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwako.

Tangazo lingine, Wabunge wanawake wote wa CCM, kukutana ni leo saa saba mchana ukumbi wa Pius Msekwa. Tangazo limetolewa na Katibu wa Wabunge Wanawake wa CCM.

Tangazo lingine ni kutoka kwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, anaomba kukutana na Wabunge wanaotoka maeneo yote yanayolima pamba, tumbaku ufuta, pareto, alizeti, katika ukumbi wa Msekwa saa nane mchana, imesainiwa na Waziri.

Tangazo lingine kutakuwa na kikao cha Kamati ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. Mtakutana katika ukumbi wa 227, Jengo la Utawala. Muda sijauona hapa, umesema baada ya kuahirishwa kwa Bunge mchana maana yake tukishaahirisha hapa Wabunge wa Kamati hii mnahitajika chumba namba 227, Jengo la Utawala.

Tangazo lingine, Kampuni ya Uwekezaji ya *UTT* inawakaribisha Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wafike nyuma ya Jengo la Utawala, karibu na Jengo la Habari ili kupata maelezo ya shughuli zinazofanywa na taasisi hiyo. Wako hapa Bungeni tangu jana mpaka tarehe 29 Januari yaani kesho, ndiyo wanamaliza zoezi lao. Kwa hiyo, mnaombwa mkaribie pale ili wawaeleze shughuli zao.

Baada ya kusema hayo, tuendelee na Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, akimaliza atafuata Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe, Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi tutamalizia na Mheshimiwa Hussein Bashe.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hotuba ya Rais wetu.

Kwanza kabisa, naunga mkono hotuba hii ambayo ni hotuba nzuri kabisa ametoa kwa Watanzania wote na wamemuelewa vizuri sana.

Mheshimiwa Hotuba hii inatoa mvuto sana siyo kwa Watanzania tu ni watu wote ulimwenguni. Kuna Marais wengi sana wanatoa hotuba, lakini

hotuba hii imekuwa ya mvuto kwa sababu amesema kile kitu ambacho wananchi wanakihitaji. Hotuba yake imetokana na jinsi alivyotembelea wakati wa kujinadi, amepita Wilaya zote za Tanzania na majimbo yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kero za wananchi zinaeleweka na Rais ameweza kuelezea vizuri sana kwenye hotuba yake. Kwa mfano, ameelezea vizuri sana masuala ya maji, barabara, umeme na afya. Wabunge wote tunaungana na hotuba hii ambayo imekuwa kama mwongozo kwa shughuli zote ambazo Wabunge tunazifanya kwenye majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais ameongelea sana Tanzania iweje na ameliongelea kwa mapana yake. Kitu ambacho kimenifurahisha, ahadi zake ambazo alizitoa wakati wa kampeni, ndani ya miezi mitatu sasa hivi tukianzia mwezi Novemba, Disemba na sasa ni Januari tayari ameanza kutekeleza zile ahadi ambazo aliahidi. Ahadi ya kwanza ambayo sisi Watanzania tunahakikisha kwamba ameanza kuitekeleza, alisema kwamba elimu bure kwa watoto wetu na hili limeanza kutekelezwa. Hakuna mtu ambaye hasikii wala haoni, tumeshaona. Kufanya utekelezaji ndani ya miezi tatu duniani haijawahitokea kwa Rais yeyote, huyu ni namba moja. Kuna watu wengine wameanza kusema anatekeleza kidogo kidogo, wewe hata nyumbani kwako umetekeleza mangapi, hicho kidogo kidogo umeweza? Nataka niwaambie Rais tusimkatishe tamaa, Rais wetu ameshaanza kufanya kazi na inaonekana kwa Watanzania na lazima tumuunge mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili alisema atapunguza matumizi makubwa kwa Serikali, Rais ameanza kupunguza na vitu vinaonekana. Jambo la kwanza alisema atapunguza Baraza la Mawaziri na amepunguza kutoka Mawaziri 60 kuwa 34 ni hatua kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu alisema atapambana na mafisadi na tumeona *TRA* kilichotokea ndani ya mwezi mmoja ilikuwa ni balaa, ilikuwa ni mtafutano, hiyo yote ni ahadi alisema ataifanyia kazi. Pia alisema atapeleka watu mahakamani na tumeona ameanza kufanya kazi hiyo. Sasa nataka niseme, kwa mwenendo huu Tanzania ambayo tunaihitaji ndiyo inakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ameongelea sana masuala ya viwanda kwamba Tanzania itakuwa nchi ya viwanda. Uchumi wa nchi yoyote ukitaka upande lazima uhakikishe viwanda ndani ya nchi yako vinafanya kazi ya uzalishaji vizuri, mimi nakubaliana naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo kwamba Tanzania hatuna viwanda lakini havifanyi kazi kwa ile *standard* ya viwanda vilivyoko duniani. Kwa mfano, mimi natoka kwenye Jimbo la Mufindi Kusini, Wilaya ya Mufindi tuna viwanda vingi

sana tukianza na Kiwanda cha Chai ambacho ni kikubwa katika Afrika; Kiwanda cha Karatasi pale *MPL* ni kikubwa sana katika *East Africa* na Kiwanda cha Pareto ni kikubwa katika dunia siyo Afrika. Tatizo kubwa ambalo tunalipata ili ku-*improve* uzalishaji ni miundombinu mibovu. Hivi sasa navyoongea kwenye Jimbo langu la Mufindi Kusini ambako kuna Kiwanda cha Chai na wakulima wa chai wako pale kuna magari mengi sana yanakwama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpongeze Rais kipindi alipokuwa Waziri wa Ujenzi barabara ile alishaanza kuifanyia kazi. Nina maana kwamba upembuzi yakinifu alishamaliza tayari na kwenye ripoti ya *RCC* waliyotoa walisema kwamba upembuzi yakinifu uliisha Mei, 2015. Kwa hiyo, nataka nitoe taarifa kwa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kwamba barabara ya kutoka Nyololo – Mtwango - Mgololo na kutoka Mafinga - Mgololo ambayo ina kilometa 84 na kutoka Nyololo - Mtwango ni kilometa 40 upembuzi yakinifu ulishaisha na Serikali iliahidi kwamba itaitengeneza kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, mategemeo yangu ni kwamba bajeti tunayokwenda kupitisha sasa hivi siyo ya upembuzi yakinifu tena ni ya kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga kwa kiwango cha lami ile barabara ambayo aliahidi Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli na kwenye kampeni alisema ataijenga. Ninavyomfahamu tukimaliza bajeti hii ataanza kujenga kule kwa sababu amesema anataka kuimarisha viwanda na hizi barabara zote zimekuwa *connected* kwenye viwanda siyo kwamba zimejengwa tu, unapojenga barabara lazima uangalie inaenda wapi. Hizi barabara zimejengwa kwenye viwanda ambapo tumesema Tanzania inakuwa ya viwanda tu, viwanda hivyo vipo lakini miundombinu ni mibovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine la muhimu sana kwenye viwanda hivi ni lazima tuhakikishe tuna-*improve* masuala ya umeme. Bahati nzuri juhudi za Serikali ni nzuri maana tunazungumzia masuala ya gesi, kila mtu anasikia na juhudi tumeziona na tumeona *REA* wanavyofanya kazi, wanapeleka umeme kwa kila kijiji. Nashukuru sana Mungu Waziri wetu Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo amerudishwa tena kwenye Wizara hiyo kwa sababu alifanya kazi vizuri sana, vijiji vingi sana vilipata umeme. Kwenye Jimbo langu la Mufindi Kusini kuna vijiji vingine hata ndoto tu kuota kwamba vitapewa umeme ilikuwa haipo sasa vilishapata umeme. Vijiji hivyo ni Kata ya Malangali, Ihoanza, Mbalamaziwa huo umeme unaelekea kwa jirani yangu wa Makambako. Ingawa juhudi ni nzuri lakini kuna vijijji kwenye Jimbo langu la Mufindi Kusini bado havijapata umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitoe ushauri kuhusiana na usambazaji huu wa umeme, tunataka umeme uende kwenye vitongoji kwa sababu utakuta umeme unafuata *line* kubwa tu. Sasa kuna kazi kubwa ya kuhakikisha wananchi wanapata umeme kwenye vitongoji. Nadhani hili tutasaidiana kusimamia ili

tuhakikishe vitongoji vyote vinapewa umeme. Kwenye Jimbo langu la Mufindi Kusini kuna vitongoji vingi, nina vitongoji 365, vijiji 88, tutataka tuhakikishe vijiji vyote vinapata umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, huu umeme unaotoka Mbalamaziwa ambao unaelekea mpaka kule Kinegembasi, kuna vijiji vya Mtambule mpaka kule Kilolo, Hiyawaga, Kiyowela mpaka kule Itika na Iholo mpaka kule Idete havina umeme. Kwa mpango huu, naiomba Serikali, siwezi kutaja vijiji vyote lakini tuhakikishe kwamba kwa mwaka huu tunaosema kwamba tunataka nchi yetu iwe ya viwanda tushughulikie suala hili la umeme. Tunaposema viwanda kuna viwanda vikubwa, vya kati na viwanda vidogo vidogo. Hivi viwanda vidogo vidogo viko kwenye kata na ili wananchi wawe na viwanda hivyo lazima tuhakikishe miundombinu ya umeme imekaa vizuri.

Suala lingine ambalo ni la mwisho ni maji. Kila Mbunge akisimama hapa anauliza masuala ya maji. Bahati nzuri Serikali ilijitahidi sana kujenga matenki ya maji katika kila kijiji. Kwenye Jimbo langu la Mufindi Kusini, kuna matenki 11 hayafanyi kazi mpaka mimi Mbunge niliamua kuanza kuchimba visima tu lakini huwezi kuanza kuchimba visima kwenye maeneo ambayo mikondo ya maji ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri wa Maji atambue kwamba hii siyo miradi mipya ni ukarabati wa miundombinu ya maji. Pale Igowole pameshakuwa mji kuna tenki la maji kubwa sana lakini halina maji, lina miaka zaidi ya 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda pale Nyololo kuna tenki la maji la muda mrefu, wananchi hawapati maji ya *gravity system*, mimi Mbunge nimechimba visima pale. Sasa namwomba Waziri haya matenki ambayo yapo ni miundombinu chakavu basi muweze kuitengeneza.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri kwenye swali la msingi lililokuwa limeulizwa hapa, anasema kwamba kuna shilingi trilioni moja imetengwa kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya maji. Namuomba Waziri asisahau Jimbo la Mufindi Kusini. Nimeshaanza kutaja pale Igohole, Nyololo, Nyigo, Idunda, Itandula mpaka Iramba kuna matenki ya maji tayari, ni kutengeneza miundombinu na kuwawezesha wananchi maji yaingie kwenye tenki na ku-*supply* kwa wananchi basi. Hizo shilingi trilioni moja siwezi kuzimaliza, mimi hata ukinipa shilingi milioni 800 za kuanzia siyo mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri wa Maji kwenye mgao huu unaokuja asinisahau kwa sababu hayo matenki yapo tayari. Wakati tutakapokuwa tuna-*discuss* bajeti inayokuja mwezi Mei au Juni, nikiona bajeti ya

vijiji vyangu haipo hiyo bajeti haitapita, nafuu nianze kusema mapema na nitakuwa namkumbusha kila wakati, haya ni masuala ya msingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni masuala ya ardhi. Masuala ya ardhi imekuwa kero sana. Bahati nzuri Waziri ameanza mpango mzuri sana, ametugawia barua tuwasilishe matatizo. Kuna mgongano kati ya Maliasili na Ardhi…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kigola muda wako umekwisha.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe atafuatiwa na Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ili nami niweze kuchangia Hotuba ya Rais ambayo inalenga moja kwa moja kutatua matatizo ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwa wananchi wangu wa Jimbo la Kavuu kwa imani kubwa waliyonipatia mpaka nikaweza kufika hapa nilipo, ni kutokana na uchapaji wangu wa kazi hawakuona kwa nini watoe kiongozi kutoka upinzani, wakaona wanipe mimi mwanamama, jimbo jipya, Mbunge mpya mwanamke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nianze moja kwa moja kujielekeza kwenye suala la elimu. Huu mpango wa elimu bure naomba niishauri Serikali yangu kwamba mpaka sasa bado una mkanganyiko, haueleweki kwa wazazi, walimu, wakurugenzi na wale wote wanaopaswa kuuelezea huu ukoje mpango, hata leo katika mijadala ya Maswali na Majibu limejitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niombe Serikali ifanye jitihada za makusudi ikauelezee mpango huu vizuri ili wazazi, wananchi waelewe majukumu yao ni yapi na nini kinatakiwa kufanyika mashuleni. Kwa sababu mmeshasema kuna changamoto na upungufu umeonekana basi mimi naamini Serikali itafanya kazi haraka iwezekanavyo kwa sababu tayari shule zimeshafunguliwa ili ziweze kuendelea vizuri na masomo. Naomba suala la elimu bure lifafanuliwe vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hili niliwaahidi wananchi wangu wa Jimbo la Kavuu kwamba nitachangia chakula mashuleni. Nawaomba wale

wote wanaopeleka propaganda hizi kwamba niliomba kwa sababu ya kupata Ubunge si kweli. Mimi ni mwalimu na najua maana ya elimu na nawahakikishia Wanakavuu ahadi zangu zote nitatekeleza kwa sababu ziko ndani ya uwezo wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende katika hotuba ya Mheshimiwa Rais ukurasa wa 11 inapoongelea kuunganisha barabara, Miji Mikuu ya Wilaya na Mikoa. Ukanda wa kwetu kule Rukwa, Katavi, Kigoma, Tabora bado barabara zetu hazijakaa vizuri. Barabara za ndani kati ya wilaya na wilaya bado hazijakaa vizuri. Naliongea hili na naomba Waziri wa Ujenzi kama yupo, nimeambiwa amekwenda kwenye dharura Kilombero lakini Serikali ipo, naomba ichukue hatua za dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu hakuna mawasiliano kati ya Kata ya Ikuba, Chamalendi, Majimoto mpaka Mbede. Hivi ninavyoongea hakuna mawasiliano yoyote na ni eneo kubwa ambalo lina wananchi wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Serikali ichukue hatua za dharura, waende wakaangalie, sina madaraja pale, madaraja manne yameporomoka kwa hiyo wananchi hawana mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu limetamkwa ndani ya Ilani na ndani ya mpango wa kutatua matatizo ya wananchi, naomba basi Serikali ijitahidi kwa kadri inavyoweza kuunganisha barabara za Mikoa, za Wilaya na maeneo mengine muhimu ya biashara. Nilishachangia katika Bunge lililopita, tutakapoweza kuunganisha barabara mpaka Kahama tutaweza kuuza mpunga na mahindi yetu sisi watu wa Katavi mpaka Darfur wanakopigana vita, hatutakuwa na shida tena ya soko la mazao yetu. Kwa hiyo, niwaombe kabisa mlichukulie kwa undani wake suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali yangu kwa namna ya pekee ambavyo imejitahidi kusambaza umeme vijijini. Niiombe tu sasa, kasoro ndogo ndogo zipo hasa kwenye nguzo. Nguzo zile ni nyembamba sana, nyingine jamani hata mguu wangu ni mnene. Zile nguzi nyingine hazina hata kamba za ku-*support* hivyo nyingi zimelala, mradi ni mzuri sana. Mheshimiwa Waziri Muhongo najua uko hapa, tumekuwa tukishirikana mara nyingi katika kubadilishana mawazo, kule kwetu mvua ni nyingi mno, naomba mtuletee nguzo nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo ni uwekaji wa nguzo zile, kijiji kinakuwa mbali nguzo inakuwa sehemu nyingine. Naomba wale mawakala wa *REA* kupitia kurugenzi husika ndani ya Wizara wafanye utafiti, waonane na watendaji wa maeneo husika kabla ya kuanza kuweka zile nguzo. Najua

unakuja tu umeelekezwa, sasa sisi siyo *robot*, lazima tufanye mawasiliano na tuone hiki tunachokifanya hatupotezi pesa sanasana kinakwenda kulenga wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naongea hilo kwa sababu kwangu mimi kutoka Milumba mpaka Manga kwenda Kibaoni nguzo zimewekwa karibu na Mbuga ya Katavi ambako wananchi hawaruhusiwi kwenda kule na kijiji kiko upande wa pili. Kwa hiyo, naomba kama hilo linawezekana muongee na mkandarasi aliyepo kule aweze kuzihamisha nguzo hizo. Najua itakuwa ni gharama kwa sababu alipewa ushauri akawa mjeuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la migogoro ya ardhi limeongelewa. Naomba Wizara ya Ardhi na Maliasili wafike kule kwangu kwani zaidi ya kata sita zinapakana na Mbuga ya Katavi na misitu ya hifadhi. Ndugu zangu wa Kavuu ni wafugaji na wakulima, wana ng'ombe wengi ambao wanapitiliza wanakwenda mpaka mbugani. Nakumbuka Mheshimiwa Rais alipofungua kampeni kwangu alianzia Majimoto, alitamka, kama *TANAPA* ama askari wa *TANAPA* wanakamata ng'ombe wale hawaruhusiwi kuwapiga risasi. Tunapowaua wale ng'ombe tunawatia hasara wale wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali sasa, kama ile sheria ya kutoza faini labda imekuwa ni ndogo basi bora tukaongeza faini lakini wale ng'ombe wakamatwe wakiwa wazima tuwatoze faini ili itusaidie sisi kufanya kazi. Utakamata ng'ombe 70 unaua ng'ombe 70 au mwenye ng'ombe anaweza kuja akakwambia ng'ombe wangu ni 500, sasa ukiwakamata wakiwa wazima ni rahisi kuwaangalia na kuwa-*identify* ukajua ni ng'ombe wangapi wamekamatwa na wakatozwa faini. Pia tunaendelea kutoa elimu kwa ndugu zetu wasiingie katika mipaka ya mbuga lakini haya ni matatizo ambapo Bunge lililopita Kamati iliundwa kwa ajili ya kuyashughulikia. Nimuombe Mheshimiwa Rais ashughulikie migogoro hii haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja kwenye suala la afya hasa katika kuwahamasisha wananchi kukata bima za afya. Tuna mifuko ya aina mbalimbali, tuna ule mfuko wa *CHF* ambao tunawahamasisha wananchi wajiunge. Kitu kinachojitokeza na changamoto iliyopo katika mfuko huu ni kwamba kama nimejiandikisha Kata ya Majimoto siwezi kutibiwa Kata ya Usevya, kama nimejiandikisha Usevya siwezi kutibiwa Kata ya Mamba, kwa maana mfuko ule unakubana pale ulipojiandikishia tu na ugonjwa hauwezi kukuambia utakupata pale ulipo. Mimi naweza kuwa nimetoka Mamba nimekwenda Mpanda Mjini nimeugua, ama nimepata *referral* kwenda Mpanda Mjini, siwezi kutumia ile kadi. Naomba hili nalo Wizara mliangalie kwa undani tuone tunatatuaje tatizo hili, ni sugu na lina-*embarrass* wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia naomba niongelee Mfuko wa Jimbo ambao umeongelewa katika hotuba ya Rais ukurasa wa kumi kwamba mfuko

huo sasa pesa itapatikana kwa wakati. Naomba Serikali ama Wizara husika isianze kuwa na kigugumizi, tutekeleze hili haraka iwezekanavyo ili tuweze kuwahudumia wananchi wetu kwa wakati muafaka kwa sababu tumesema 'Hapa ni Kazi tu' na tufanye kazi kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala la hati miliki za kimila, naomba Serikali iharakishe kuzitoa kwa wale wanaomiliki mashamba kihalali ili waweze kukopa na wajikwamue kutoka kwenye umaskini, japokuwa baadhi ya benki imekuwa hazizitambui.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwaombe sana, aidha mtuelekeze ni wapi wananchi wenye zile hati za kimila wanaweza wakapata mikopo ili waweze kujiendeleza badala ya kwenda benki unaambiwa sisi hiki hatukitambui, unataka kuweka dhamana ndugu yako kakamatwa, haitambuliki. Kwa hiyo, niiombe sana Serikali yangu, kwa *spirit* tuliyonayo mimi naamini tutashinda na naamini tutavuka malengo katika kutatua matatizo ya wananchi, la msingi ni ushirikiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu wa Kata ya Usevya, najua hamtaniona sasa hivi lakini baadaye mtaniona, niwaombe sana wazazi wangu wa Kata ya Usevya, hao wazazi wanaowaambia msichangie, mmojawapo anaitwa Bulimba, mwingine Emma Godfrey, najua wanatoka upande gani wa chama, ni walewale wasiotaka kuchangia maendeleo …

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba muda kidogo. Wazazi wangu wa Usevya, naomba mtumie busara katika kuchangia suala la elimu.

NAIBU SPIKA: Samahani Mheshimiwa muda wako umekwisha, naomba ukae.

MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Nasoro Kisangi, Mheshimiwa Hussein Bashe, Mheshimiwa Richard Philip Mbogo tutamaliza na Mheshimiwa Kiswaga Boniventura Destery.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii mchana huu ili na mimi niweze kuchangia hotuba ya

Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Dkt. John Pombe Magufuli aliyoitoa hapa Bungeni tarehe 20 Novemba, 2015. Waswahili husema, ada ya muungwana ni vitendo, Mheshimiwa Rais kauli hii ameenda nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais alipokuja hapa Bungeni alizungumzia mambo mbalimbali na kutoa mwelekeo wa Serikali yake itakavyofanya kazi. Baada ya hapo tumeona hakika kwamba anafanya kulingana na jinsi anavyosema. Tunampa hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, niwashukuru wananchi wa Jimbo la Mbogwe kwa kuniamini kwa mara ya pili niwawakilishe katika Bunge hili. Nasema ahsate sana na naahidi sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imempata kiongozi na imempata muungwana ambaye hakika anajua matatizo ya nchi hii. Sisi Wabunge na wananchi kwa pamoja tunachotakiwa kufanya ni kumuunga mkono moja kwa moja ili aweze kufanya kazi zake na tufanye lile ombi lake la kumuombea kwa Mwenyezi Mungu ili amtie moyo na nguvu aweze kuzitekeleza ahadi zote alizoziahidi na kuitendea haki Ilani ya Uchaguzi ya chama chetu, Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais kwenye kampeni zake na katika kauli zake amekuwa akisisitiza sana juu ya suala la kuwa na nchi yenye viwanda. Nchi yetu ili iwe na viwanda ni muhimu kuwa na umeme wa uhakika. Jambo hili linawezekana kwa sababu ameweka jembe katika Wizara hii, Waziri Mheshimiwa Profesa Muhongo ambaye kila mmoja ni shahidi wa kweli juu ya utendaji kazi wa mtu huyu. Mtu huyu tumuombee kwa Mungu aweze kutimiza ndoto zake juu ya taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda haviwezekani bila ya kuwa na umeme wa uhakika. Ukiwa na umeme wa uhakika utakuwa na uwezo wa kuweza kuvutia wawekezaji wa viwanda kutoka ndani na nje ya nchi. Kwa ajili hiyo ndugu yangu Mheshimiwa Muhongo Mungu akutie nguvu uweze kuitendea haki nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ya Tanzania kijiografia ni nchi ambayo imebarikiwa na Mwenyezi Mungu. Tunazo rasilimali mbalimbali, tunayo bahari, ardhi ya kutosha, anga la kutosha, maliasili za kila aina na wanyama wa kila aina. Kwa ajili hiyo, utajiri huu tukiutumia vizuri na tukienenda sambamba na Rais wetu, hakika tutafika haraka kwenye Tanzania ya watu wenye maisha ya kipato cha kati. Tunachotakiwa kufanya ni kupiga kazi na kushirikiana kwa pamoja kupiga vita rushwa na aina mbalimbali za uzembe.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la viwanda bila mawasiliano haliwezekani. Kwa maana hiyo, niiombe Serikali itilie mkazo ujenzi wa bandari katika bahari zetu, katika maziwa yetu na kuimarisha reli. Reli ndiyo usafiri wa uhakika wa kuweza kusafirisha mizigo mingi inayotoka nje ya nchi na inayotoka ndani ya nchi kwenda nje ya nchi. Ili reli yetu iweze kufanikiwa kufanya kazi zake vizuri basi ni vizuri tukawa na treni, ikiwezekana kama umeme utakuwepo ziwepo reli za umeme. Maana umeme ukishakuwa wa uhakika maana yake tutakuwa na treni zinazoendeshwa kwa umeme, zitapunguza muda wa kusafirisha bidhaa mbalimbali kutoka Bandari ya Dar es Salaam na kwenda katika nchi za jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niishauri Serikali itekeleze kwa wakati ujenzi wa reli ya kutoka Isaka - Msongati - Kigali nchini Rwanda. Kwa sababu nchi yetu iko vizuri kijiografia na wenzetu hawa wa Rwanda, Burundi, Mashariki ya Congo tumepakana nao. Kwa maana hiyo uchumi wa nchi hizi unaweza ukainufaisha nchi yetu kwa uzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika suala zima la elimu. Nchi yetu ili iweze kuendelea kwa uhakika ni vizuri tukawa na vijana wasomi ambao watahusika katika uendeshaji wa viwanda. Kwa maana hiyo suala la teknolojia ni jambo la muhimu na la msingi sana. Kwa maana hiyo, watu wa *COSTECH*, kwa maana na *Commission for Science and Technology* tunatakiwa tuwape nguvu na kuwapa kipaumbele ili waweze kutoa vijana ambao watakuwa wameelimika vizuri na katika vyuo vikuu mbalimbali masomo ya sayansi tuyape kipaumbele. Tutakapokuwa na wasomi wazuri hata viwanda vitakuwa vinaweza kuajiri watu ambao wana weledi wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe tu mfano, katika nchi hii migodi imekuwa inafanya kazi vizuri kutokana na wataalamu wa Kitanzania lakini *management* tu ndiyo unaweza ukakuta wamepata kutoka nje. Kwa mfano, katika mgodi wa Mkoa wa Geita pale *GGM*, Watanzania wengi wanafanya kazi pale na wanafanya kazi nzuri. Hata Mgodi wa Tulawaka ambao ulichukuliwa na Serikali, Watanzania wanafanya kazi pale ya uzalishaji wa dhahabu, kwa kweli inaonekana Watanzania tunaweza, kwa maana hiyo tujipe moyo na tujitahidi tu kujiamini kwamba tunaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe kwa mara nyingine nchi hii imejaliwa kuwa na neema ya maji basi maji ya Ziwa Victoria ambayo yamefika katika Wilaya ya Kahama kutoka Mwanza, tunaiomba Serikali itoe fedha kwa ajili ya kuyafikisha katika Wilaya yetu ya Mbogwe ambayo iko umbali wa kilomita 60 tu kutoka maji ya Ziwa Victoria yalipofikishwa. Itakuwa ni jambo la kheri na inaweza ikatusaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ambayo mara zote yamekuwa yakisababisha ukame katika maeneo mbalimbali ya nchi hii. Kwa

hiyo, kupatikana kwa maji ya Ziwa Viktoria katika Wilaya yetu ya Mbogwe inaweza ikawa ni ufumbuzi wa muda mrefu wa tatizo la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, niiombe Serikali kwa wakati wake izisaidie halmashauri, wilaya na mikoa mipya ili ziweze kujenga ofisi zake kwa wakati na tuweze kupiga hatua kama ilivyo katika mikoa mingine.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Masele ahsante.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuzungumzia machache kuhusu hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda nitoe pongezi kubwa sana kwa niaba ya Wabunge wenzangu kwa Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa nchi hii kwa kura nyingi za kishindo, mimi nampa hongera sana na Wabunge wenzangu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhusu niseme maneno yafuatayo kwa niaba ya Wabunge wenzangu kwa Chama changu cha Mapinduzi. Nakipongeza Chama cha Mapinduzi kwa kupata Wabunge 264 katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Haikuwa kazi ndogo, ilikuwa kazi kubwa kweli kweli, lakini ukweli umebaki ukwel, keki ya Bunge imeichukua Chama cha Mapinduzi imewaachia robo. Nakishukuru sana Chama cha Mapinduzi kamati zote za kampeni zilifanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Naomba sasa nichukue fursa ya kipekee kuwashukuru wanawake wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa kunichagua mimi nije niwawakilishe katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nawaahidi wanawake wa Dar es Salaam nitawafanyia kazi na sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nirudi kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais alitoa ahadi zake kwamba atakapopata Urais ataunda Baraza dogo la Mawaziri. Hili amelitimiza na ameunda Baraza la Mawaziri lenye Mawaziri 19 tu. Mheshimiwa Rais nampongeza kwa hilo. Pia ametuleta Mawaziri mahiri, wachapakazi ambao tuna imani nao kabisa

wataivusha Serikali hii kutoka pale ilipo kuipeleka mbele na kukipatia ushindi au mwenendo mzuri Chama cha Mapinduzi na tuonyeshe kwamba sasa tunataka kutengeneza CCM yenye mabadiliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la *TBC*. Kumekuwa na maneno mengi sana kuhusu *TBC*. Mheshimiwa Waziri ameeleza vizuri sana nini tatizo lakini bado maneno yanazungumzwa. Naomba niliambie Bunge mimi Dar es Salam nina tatizo kubwa la mfumuko wa bei ya vyakula. Wananchi wanahangaika, mchele unanunuliwa shilingi 2,500/= mpaka shilingi 2,800/=. Kama kweli kuna hali kama hiyo mtu mwenye njaa anaweza akangalia *TV*?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Serikali hili suala la *TBC* tuliangalie kama alivyozungumza Mheshimiwa Waziri kwamba yako matatizo. Kwa hiyo, haya matatizo ni jukumu letu sisi kama Wabunge kukaa chini na kuyatafakari. Hata hivyo, kuna umuhimu gani wa mimi kuonekana sasa hivi wakati sitafanya chochote Jimboni? Hivi kuongea kwangu kunawasaidia nini? Mimi naomba Serikali inisaidie kupunguza mfumuko wa bei jijini Dar es Salaam, vyakula vimekuwa bei juu sana, hilo mimi kwangu ndiyo naona changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuchukua zile fedha zote za sherehe ya Uhuru kuja kutujengea barabara ya Kawawa. Kwanza nasema kwa niaba ya Wabunge wale wa Majimbo waliopelekewa zile hela, Jimbo la Ubungo, Kinondoni pamoja na Kawe ambapo barabara ile ndipo ilipo, napenda nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutuletea zile fedha kuondoa msongamano wa magari barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba wananchi wa Dar es Salaam tunapotaka kufanya maamuzi tuhakikishe tunafanya maamuzi ya kweli kupata watu wa kututetea. Sisi kama Mkoa wa Dar es Salaam, Mheshimiwa Rais katupa hizo fedha ili barabara zetu zitengenezwe leo Mbunge wa Dar es Salaam unatoka nje wakati wa kuchangia hotuba ya Rais, hivi wewe ni kiongozi wa wananchi walio wengi au wa walio wachache?

Mimi naomba tuangalie sana nini tunakuja kuwafanyia wananchi ndani ya Bunge hili, tunakuja kuwasemea wananchi wetu tulete maendeleo. Leo mimi ningezungumza na mwenzangu wa Kawe, Ubungo nafikiri Mheshimiwa Rais angepata salamu zetu naye angeharakisha mradi huo. Nawaomba wananchi, CCM sasa ina mabadiliko na sisi tumejifunza, Wabunge tunakuja tukiwa wakali kwa lengo la kuwatetea wananchi wetu. Sasa kazi imeanza na tutafanya hivyo, hatukubali tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais, ukurasa wa 15, amesema tutajenga viwanda ili kukuza uchumi lakini pia kuleta ajira kwa vijana. Nimuombe Mheshimiwa Rais pamoja na yote tuangalie viwanda

vilivyokufa na vinavyosuasua pia. Kuna viwanda vingi Dar es Salaam kama *Aluminium Africa*, *Metal box, Bora Shoes*, *National Battery, Tanzania Cables*, *Mbagala Sheet Glass*, Tanita Mbagala, *National Milling, Tangold Africa*, Urafiki-Ubungo, UFI-Ubungo, hivyo vyote ni viwanda ambavyo miaka hamsini iliyopita vilikuwa vikifanya kazi na leo vingine vimegeuzwa maghala.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Kiwanda cha TANITA Mbagala kilikuwa kinawapatia ajira kina mama. Kiwanda cha Tanita ni cha korosho kilikuwa kinabeba akina mama leo kiwanda kile kimegeuzwa ghala sijui watu wanahifadhi madudu gani, takataka tupu mle ndani, hivi kweli tutafika kwa hali hii? Niiombe Serikali katika hii sera yetu ya kutaka kuvumbua viwanda hivi tuyaangalie na maeneo hayo ili wananchi na vijana wetu waweze kupata ajira.

Naomba sasa nizungumzie suala zima la elimu. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kusema kwamba elimu itatolewa bure kwa ngazi ya shule ya msingi na sekondari. Ninao mfano wa wazi kabisa katika Kata ya Charambe - Mbagala wameandikisha watoto 6,000 wa darasa la kwanza. Hii inaonyesha wazi kwamba kumbe watoto wengi walikuwa wako majumbani wanashindwa kupata kile kiasi cha fedha cha kuingilia shuleni. Kwa hiyo, nampongeza kabisa Mheshimiwa Rais kwa hili wazo lake ambalo amelitekeleza. Pia ziko changamoto kwenye hayo makundi au mchanganuo wa fedha zile na hasa katika fedha za utawala, naomba fungu kidogo liongezwe pale kwa sababu ya walinzi. Pia changamoto ndogo ndogo zinazowakuta walimu hata kupata sukari kilo moja kwa siku angalau na wao wanywe chai kwa asubuhi tu. Niombe sana Serikali hilo nalo liangaliwe. Awamu ya Rais Mkapa ilikuwa zinakuja fedha za *capitation* kama hizi kulikuwa na fungu la utawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaambie Watanzania hizi fedha zitategemea sana utendaji wa Mwalimu Mkuu. Mwalimu Mkuu aliye bora akizisimamia vizuri fedha hizi kwa kweli mambo yatakwenda vizuri. Maana naona yako matatizo yanaletewa Serikali kumbe ni ya ubinafsi wa mtu, amepelekewa fedha ameshindwa kuzitumia vile inavyotakiwa matokeo wazazi wanaleta maneno. Mimi ni mwalimu pia niwaombe walimu wenzangu waunge mkono hizi jitihada za Rais kwa kutumia mafungu hayo vizuri kama vile walivyoagizwa na siyo vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nichangie upande wa nishati. Hotuba ya Mheshimiwa Rais, ukurasa wa 6, imeeleza itaboresha na itaondoa kabisa matatizo ya kukatikakatika kwa umeme. Naona juhudi kubwa ya Mheshimiwa na nampongeza sana na mfano na sababu ya kumpongeza ninazo. Juzi nimepigiwa simu na watu wa Kigamboni eneo la Ungindoni wanasema haijawahi kutokea, wameomba umeme lakini wameletewa mita majumbani bila ya wenyewe kuwepo. Mita zimepelekwa, wenyewe hawajui,

wamepewa namba za simu, mita wameikuta iko nyumbani jambo ambalo halikuwa la kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kisangi muda wako umekwisha.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono hotuba hii ya Mheshimiwa Rais, nimwambie peleka zile fedha kwenye barabara ya Kawawa mara mvua itakapoisha na siku ya kufungua uniite. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Hussein Bashe.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa. Awali ya yote, nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha sote salama na kuendelea kulifanya Taifa letu kuwa salama na tulivu pamoja na misukosuko yote ambayo tumekuwa tukikabiliana nayo. *(Makofi)*

Vilevile nitumie nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Nzega kwa heshima walionipa ya kukichagua Chama cha Mapinduzi na kunichagua mimi kuwa Mbunge wao wa Jimbo la Nzega. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba aliyoitoa wakati wa ufunguzi wa Bunge. Wataalamu wengi wa utawala wametoa *criteria* na *quality* za viongozi ambapo viongozi wa aina mbalimbali na Taifa hili kwa muda mrefu tumekuwa tukiomba kupata kiongozi ambaye ni *transformational* wa kuweza kutusaidia kui-*transform society* yetu na kuipeleka mbele. Nitumie nafasi hii ku-*copy* sehemu ya *presentation* aliyowahi kuifanya Dkt. Mpango akielezea sifa za kiongozi ambaye ni *transformational*. Moja ya sifa ya kiongozi ambaye ni *transformational* ni kiongozi *uncompromising* katika jambo analoliamini na lenye maslahi ya watu wake. Katika *presentation* ya Dkt. Mpango alitumia neno moja *no gain without pain*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia hotuba ya Rais, wenzetu walisema kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano amekuwa akivunja na kukanyaga sheria katika maamuzi ambayo amekuwa akiyafanya sasa. Mimi niseme, moja ya tatizo kubwa linalokabili Taifa letu ni uwepo wa sheria zinazoruhusu watu kuzitumia kuliibia Taifa hili. Sheria hizi zimewapa fursa watendaji wengi kuiibia nchi yetu. Mmeona wizi mwingi ambao umefanyika katika Taifa hili umehifadhiwa katika sheria. Tunahitaji kiongozi mwenye sifa ya

Rais Magufuli kuzikanyaga hizi sheria ili tuweze kupambana na wizi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yalisemwa hapa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kwamba Rais amepeleka fedha katika sekta ya elimu bila kuleta *mini-budget*. Swali tu la mantiki, tulitaka watoto wasiende shule tusubiri Bunge la Februari tuwaleteeni *mini-budget* mpitishe? Tumeambiwa barabara ya Morocco, fedha zilizokuwa *allocated* kwa ajili ya sherehe za uhuru zimepelekwa pale bila kufanyika utaratibu wa kumpata mkandarasi. Walitaka tutumie miezi sita kumpata mkandarasi ili barabara ile ijengwe. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwaambieni, jambo la kwanza ambalo tunatakiwa kulifanya sasa, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kaka yangu Mwakyembe kaeni mzipitie hizi sheria hovyo mzilete kwenye Bunge la Aprili tuzifute, Sheria ya *PPRA* ni wizi mtupu. Leo kujenga tundu moja la choo mkandarasi anakuletea bajeti ya shilingi milioni 25 na imefuata taratibu za *evaluation* na *process* zote, kile choo kina nini? Kwa hiyo, nimuunge mkono Mheshimiwa Rais katika hatua anazochukua, Taifa letu liko kwenye dharura, linahitaji aina hii ya *leadership* ili *tuweze* kwenda mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, nijikite sasa kwenye hotuba ya Rais. Tumeona *political will* ya Rais ya kutaka kulifanya Taifa hili kuwa la viwanda lakini yapo mambo ya msingi ambayo tunatakiwa tuyafanye kama Waheshimiwa Wabunge na Watanzania. Jambo la kwanza ambalo naiomba Wizara ya Fedha, nia ya Rais haiwezi kufanikiwa kama Wizara ya Fedha haitakaa chini na kufanya *strategic decision* ni maeneo gani ya viwanda tunataka kuwekeza ambayo yatakuwa na matokeo chanya kwa watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashauri na ningeomba Waheshimiwa Wabunge na Wizara ya Fedha tukubaliane, nchi hii tunasema ni nchi ya wakulima ni kweli. Hata hivyo, ukitazama takwimu uchangiaji wa sekta ya kilimo katika pato la Taifa kwa mwaka 2014 umeshuka kwa asilimia kumi na nne. Aidha, Watanzania waliokuwa wamejiajiri katika sekta ya kilimo mwaka 2012 walikuwa asilimia 76 leo ni asilimia 66 maana yake ni kwamba Watanzania wamehama kwenye sekta ya kilimo wameenda kwenye sekta zingine. Hii inamaanisha nini? Maana yake tukifanya maamuzi yasiyokuwa sahihi katika uwekezaji wa viwanda, tukaenda katika maeneo ambayo hayatakuwa na matokeo chanya kwa watu wetu wengi, umaskini wa Watanzania utaendelea kuwepo hata tukiwa na viwanda vyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kwenye suala la viwanda, hatuwezi kufanikiwa kwenye suala la viwanda kama hatujamsaidia Mheshimiwa Profesa Ndalichako katika eneo la elimu kuhakikisha kwamba tunawekeza fedha nyingi kwenye sekta ya elimu ili ku-*improve skills* za vijana wetu waweze kwenda

kusaidia uzalishaji katika viwanda. Tusipohakikisha kwamba elimu yetu inatoa majibu sahihi kuweza kufikia lengo la viwanda, matokeo yake ajira nyingi za viwanda hazitachukuliwa na Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, tukaipa kipaumbele Wizara ya Elimu na kuiagiza Wizara ya Elimu ije na mpango mkakati wa namna gani *technical schools* zetu kama vyuo vya *VETA* vitatoa wanafunzi ili waweze kwenda kuajiriwa katika sekta ya viwanda vya *Agro Based Industries.* Hivi ndivyo viwanda ambavyo vitatuondolea matatizo. *Textiles Industries,* hivi ndivyo viwanda ambavyo vitaajiri vijana wetu wengi. Tunaotoka katika maeneo ambayo pamba inalimwa mmeona wakulima wamepoteza matumaini. Tukiongeza jitihada katika viwanda vya *textiles,* mazao ya pamba yakawa *processed* katika viwanda vyetu, wakulima wetu watakuwa na moyo wa kufanya kazi, watakuwa na soko la uhakika na hii itasaidia sana nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunazungumzia viwanda lakini hakuna jambo la msingi kama *infrastructure* ya reli. Nimeangalia Mpango wa Maendeleo wa mwaka mmoja, Waziri amesema tutajenga reli ya *standard gauge*. Habari ya kujengwa reli imekuwepo kabla mimi sijaja hapa Bungeni, nimekuwa nikiisikia, niwaombe Wabunge, bajeti itakayokuja kama haitatuambia imetenga fedha kiasi gani za kujenga reli ya *standard gauge*, tusikubali kuunga mkono bajeti hiyo. Kama bajeti ya Serikali itakuja bila suala la reli kupewa kipaumbele cha kutosha tusikubali kuunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia suala la uzalishaji wa viwanda, tumsaidie Mheshimiwa Profesa Muhongo. Leo 41% ya uzalishaji wetu wa umeme wanazalisha *Independent Power Producers* na tunanunua umeme kwa shilingi ngapi, ni ghali. Kwa hiyo, tuisaidie Serikali uzalishaji wa gesi uweze kutusaidia kama nchi. Tufanye maamuzi ya lazima, haya mambo ya 100% *owned by private*, anakuja anatumia gesi yetu, sisi hatu-*own stake* katika huu uzalishaji, ameenda kukopa nje hatumsimamii alikokopa, bado tutaununua umeme kwa bei kubwa. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Bashe muda wako umekwisha.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Richard Philip Mbogo.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii. Kwanza nimshukuru Mungu kwa namna ya pekee ambavyo ametujalia mpaka tupo hapa na uhai tulionao.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, naomba niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Nsimbo kutoka Mkoa wa Katavi, kwa jinsi walivyoniamini. Nilivyowaeleza kwamba nitawatumikia, kazi tumekwishaianza, naomba waendelee kuniamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, imesheheni mambo mazuri sana. Kwanza tukiangalia huduma za jamii na matatizo na kero ambazo zinazunguka jamii zote za Watanzania. Mimi namuunga mkono kwa hatua ambazo amechukua kuanza kushughulikia kero zetu, naamini Serikali anayoiongoza itafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwamba Mheshimiwa Rais atafanikiwa kwa sababu amelenga pia kuongeza mapato na kupunguza matumizi. Mtanzania yeyote mfanyabiashara huwa haitaji kupata hasara katika biashara anayoifanya. Siku zote ataangalia mauzo yaongezeke na apunguze gharama. Mheshimiwa Rais wetu ameliangalia hilo ili aweze kuboresha na kupeleka fedha nyingi kwenye miradi. Mimi namuunga mkono mapato yaongezeke na matumizi yapungue na sisi Wabunge tutaendelea kumshauri maeneo mengi ambayo yatakuwa na upotevu wa fedha ili ziweze kuongezeka na wananchi wetu waweze kufaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu la Nsimbo limezungukwa na kero nyingi sana. Kwanza, wananchi wangu zaidi ya 80% au 90% ni wakulima wa mazao ya biashara na mazao ya chakula. Ndiyo maana mkoa wetu ni moja ya mikoa inayotoa chakula kingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna matatizo ya ardhi kuchoka sana, maeneo mengi tumekuwa hatupati mazao ipasavyo. Pia kuna tatizo la pembejeo na tunamwomba Waziri wa Kilimo katika ile ziara yake ya Tabora afike mpaka Mkoa wa Katavi ili aweze kuliangalia suala hili. Tunajua Naibu Waziri alipita lakini ratiba yake ikuruhusu pia kukanyaga na Jimbo la Nsimbo. Wakulima wa tumbaku wanapata taabu sana, kodi ziko nyingi, makato mengi, mikopo unamlipia hata yule ambaye hakuhusu. Kwa hiyo, tunaomba awaangalie sana wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu la Nsimbo ni jipya, kuna kata zimeongezeka na mojawapo ni kata ambazo zilikuwa ni makazi ya wakimbizi lakini Serikali ya Awamu ya Nne ilitoa uraia na mwaka jana wamepiga kura, tumepata Madiwani. Hata hivyo, zile kata zina mahitaji mengi sana. Kwanza, bado ziko kwenye hadhi ya Mkuu wa Makazi, kwa hiyo sheria iliyopo pale ni ya

Mkuu wa Makazi, utendaji wa Halmashauri pale ndani umekuwa hauendi ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Waziri wa TAMISEMI kaka yangu Mheshimiwa Simbachawene, awasiliane na Waziri wa Mambo ya Ndani, kata au maeneo yaliyokuwa makazi ya wakimbizi ya Katumba, Mishamo na Bulyanhulu tuangalie jinsi gani hadhi za makazi ya wakimbizi zinafutwa yabakie kuwa maeneo huru ya raia. Wale raia ambao hawajapata uraia, nimkumbushe Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni aliahidi kwamba suala hili litashughulikiwa haraka ili waweze kupewa uraia.

Kwa hiyo, tunaomba sana ahadi ya Mheshimiwa Rais itekelezwe wale ambao bado wapate uraia na makazi hayo ya wakimbizi hadhi yake ya ukimbizi iondoke ibakie eneo huru.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu lina kata 12 tuna vituo vya afya viwili tu na zahanati ni chache mno, vijiji vingi havina zahanati. Kwa hiyo, taabu ya huduma kwa mama zangu ambao ndio mara nyingi wanahitaji huduma za afya, imekuwa ni shida. Vilevile Jimbo langu la Nsimbo, sekondari ya juu hakuna na sekondari za kawaida ziko chache mno na tuna kata mpya. Kwa hiyo, tunaomba Serikali katika bajeti hii iliangalie kwa jicho zuri kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakumbwa na shida ya miundombinu na Jimbo la pili baada ya Mheshimiwa Rais kufungua kampeni mwaka jana lilikuwa ni la Nsimbo baada ya Jimbo la Mpanda Vijijini. Nilimwomba barabara kutokea Kanoge – Mnyake - Msaginya na aliahidi itatengenezwa kwa fedha za ndani. Nami nitamwomba Waziri ndugu yangu Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa anisaidie liingie kwenye bajeti ya mwaka huu 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mambo mengi, tunashukuru Serikali ya Awamu ya Nne, *alhamdulillah* imetupa majimbo, Halmashauri na pia umeme. Nimshukuru Mheshimiwa Profesa Muhongo kwa umeme wa vijijini, kata nne zimepata umeme lakini pia tupate umeme kwenye kata zilizobakia. Vilevile Halmashauri yangu inahitaji Wakuu wa Idara, kati ya Wakuu wa Idara 19 waliopo ni nane tu wengine wanakaimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais, naomba tuangalie suala la viwanda ambalo lipo hata kwenye Mpango wa Miaka Mitano, tumesahau pia kuangalia viwanda vidogo vidogo. Kuna maeneo mengi ambayo tunahitaji viwanda vidogo vidogo, kama dada yangu Mheshimiwa Hasna alivyochangia jana kuhusu Kigoma kwa lile zao ambalo linatengeneza sabuni, basi tuangalie viwanda vidogo vidogo kulingana na maeneo yetu tulipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nichangie suala la bandari, kuna mpango wa Serikali wa kujenga bandari ya Bagamoyo lakini tujue faida na hasara zitakuwaje katika uchumi wa nchi yetu. Tukiweka mwekezaji maana yake mpaka arudishe gharama yake, tuangalie na bandari tuliyonayo tutakosa mapato kiasi gani? Tunaiomba Serikali iangalie suala hili kwa jicho la karibu zaidi.

Katika hotuba ya Mheshimiwa Rais alizungumzia *Air Tanzania*. *Air Tanzania* kwa muda mrefu imekuwa inaenda kwa ufadhili wa Serikali, ndege moja gharama kubwa za uendeshaji. Serikali imepanga kununua ndege nyingine mbili kwa katika Mpango wake wa Miaka Mitano. Tusiende kihasara, ni bora watumishi waliopo walipwe, waende wakaanze maisha mapya tubakize wafanyakazi wachache ili *Air Tanzania* ifanye kazi kibiashara na kwa faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la kodi kwa wastaafu, mtu amefanya kazi miaka 30, miaka 20 analipia kodi, lakini anakuja kwenye mafao ya kustaafu pia napo anakatwa kodi na hata *TRA* ukiuliza *formula* sahihi hakuna mahali ambapo pamenyooka kuhusiana na kodi hii. Kwa hiyo, tunaomba Serikali iwasamehe wastaafu kodi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Serikali, miundombinu kwenye jimbo langu ni shida na sasa hivi Mto Koga umejaa na kuna watu wamepoteza maisha. Kwa hiyo, tunaomba reli yetu kama ilivyoahidiwa treni ipite wakati wote, fedha za dharura zije, barabara ziweze kupitika, Mkoa wa Katavi tumekuwa kama tuko kisiwani. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali kwa kupitia Wizara mtuangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia ni kuwa ajira ni kitu muhimu kwa watu wote. Kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi tuliahidi kwamba Serikali italeta mikopo *(revolving fund)* ya jumla ya shilingi milioni 50. Kwa hiyo, tunaomba utaratibu uandaliwe haraka, mfuko huo uanzishwe tuupitishe ili watu wetu waweze kupata mikopo na kufanya kazi ambazo zitawasaidia katika kunyanyua uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye ajira jimbo langu lina wachimbaji wadogo wa dhahabu lakini Serikali imewapeleka Kaparamsenga kwenye *copper*. Hiyo haina msaada na sasa hivi kuna mwombaji mpya *Kijani Investment* kwa eneo lililokuwa linamilikiwa na *GBA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali iachie wachimbaji wadogo wadogo eneo hilo, ni kilometa kumi tu kutoka Mpanda Mjini. Bahati nzuri ndugu yangu, kaka yangu, Mheshimiwa Profesa Muhongo barua imekuja ofisini kwako ya Chama cha Wachimbaji wadogo wadogo, wakiliomba hilo eneo wapewe

wao badala ya kampuni mpya ya *Kijani Investment*. Maana wao hawana uwezo wa kwenda kuchimba *copper,* mashapo hayo ya *copper* hawawezi, inahitaji uwekezaji mkubwa sana. Kwa hiyo, tunaomba waachiwe sehemu ambayo wataweza kupata fedha kidogo kwa ajili ya kukidhi mahitaji yao, dhahabu ni rahisi kuliko *copper*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niiombe Serikali, Halmashauri zetu zinapewa *ceilling* ya bajeti lakini Serikali huwa haiangalii mahitaji husika ya kila halmashari. Kwa hiyo, Serikali ifanye upembuzi mzuri ili hizi *ceilling* za bajeti inazotoa iangalie na uhalisia wa mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tumalizie na Mheshimiwa Boniventura Kiswaga. Utatuwia radhi itabidi uongee kwa kifupi kidogo kwa sababu muda wetu umekwisha.

MHE. KISWAGA B. DESTERY: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema zake kwa kuniwezesha kufika ndani ya ukumbi huu na nawashukuru wananchi wa Jimbo langu la Magu kunipa Ubunge ili niweze kuwatumikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naipongeza hotuba ya Mheshimiwa Rais, kwa kadri ambavyo imejikita kuonesha kwamba Watanzania wana mahitaji. Imegusa mahitaji ya kila Mtanzania lakini pia imeonesha huruma kwa Watanzania, naipongeza sana. *(Makofi)*

Sisi Watanzania tumepata kiongozi. Vitabu Vitakatifu vimeandika, ukisoma 2 Timotheo 2:20, unasema; "Nyumbani mwa Bwana kuna vyombo vingi, viko vyombo vya dhababu, vipo vyombo vya miti." Mheshimiwa John Pombe Magufuli ndicho chombo cha dhahabu ambacho Mwenyezi Mungu Watanzania ametuandalia. Naomba tumuunge mkono wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na maji. Jimbo langu la Magu lina matatizo makubwa sana ya maji kama zilivyo wilaya zingine. Sisi wenye nguvu ukirusha jiwe linakwenda moja kwa moja ndani ya maji lakini Wilaya ya Magu haina maji. Tumeahidiwa na viongozi waliopita, Rais wa Awamu ya Tatu, Rais wa Awamu ya Nne mpaka leo Magu haina maji. Bahati nzuri Mheshimiwa John Pombe Magufuli wakati wa kampeni naye ameahidi.

Mimi sina shaka kwa sababu hotuba hii amezungumzia sana suala la maji na sina shaka kwa sababu Waziri wa Fedha ni *type* ileile ya Mheshimiwa Profesa Muhongo kwamba hataki ubabaishaji kwenye makusanyo ya fedha,

nampongeza sana. Ili miradi hii itekelezeke lazima fedha zikusanywe na nawaomba wakaze kamba wasilegeze hata siku moja kwa sababu nchi hii ilikuwa imefikia pabaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua asali ni tamu sana lakini wako watu ambao hawanywi asali lakini kila mmoja anakunywa maji. Hebu tuangalie sasa suala hili, Serikali ifanye kila linalowezekana hata kukopa Benki ya Dunia ili kuweza kutekeleza miradi ya maji iliyoko kwenye nchi hii hasa Wilaya ya Magu. Wilaya yangu vijiji vingi havina maji na Wanamagu wana uvumilivu ukubwa sana na hili ndilo lililonileta Bungeni kwamba maji ndilo hitaji la wananchi wa Magu. Ili nirudi tena hapa Bungeni 2020 lazima maji yapatikane. Waziri wa Maji, Waziri wa Fedha, nisaidie hili ili Mheshimiwa Rais aliposema kwamba tumwachie jambo hili la maji Magu litekelezeke kweli kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo mradi ambao umeanza upembuzi yakinifu leo ni miaka miwili watu wanachakata, wanachakatia wapi? Mheshimiwa Rais alisema hawa watu wanaochakata watachakatia nje, Mtaalamu Mshauri anachukua miaka miwili anafanya upembuzi yanikinifu bila kukamilisha, hii ni kweli? Hii Serikali ya Awamu ya Tano ya Rais John Pombe Magufuli ya 'Hapa Kazi Tu' imwangalie huyu Mtaalamu Mshauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la elimu bure Serikali imeanza vizuri. Mpango wa *capitation* ulikuwepo tangu mwaka 2002 lakini naomba niishauri Serikali kwamba wakati inatoa dola 10 kwa kila mtoto…

NAIBU SPIKA: Naomba umalizie Mheshimiwa.

MHE. KISWAGA B. DESTERY: *Exchange rate* ilikuwa ni Sh1,000 leo ni Sh.2,200. Kwa hiyo, waangalie hali ilivyo sasa ili kumudu uendeshaji wa shule hizi ili ziweze kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja lakini nina mambo mengi ya kuzungumza, kumbe ningeanzia mchana, basi niishie hapo. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. Nimeletewa tena tangazo la Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, ameongeza miwa kwenye ile idadi aliyokuwa ametaja, labda kwa ushauri angeonana tu na maeneo yote yenye wakulima.

Nitataja Waheshimiwa watano ambao tunaweza kuanza nao mchana, Mheshimiwa Joram Hongoli, Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mheshimiwa Kemirembe Lwota, Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige na Mheshimiwa Halima Bulembo.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha kikao hiki mpaka saa kumi jioni.

(Saa 07.00 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 10.00 jioni)

(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)

HOJA ZA SERIKALI

Hoja ya kujadili Hotuba ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

(Majadiliano Yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Halima Bulembo, ameshafika! Mheshimiwa Joram Ismael Hongoli.

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kushukuru kwa kupewa nafasi hii nami kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Rais ya tarehe 20 Novemba, 2015. Nimshukuru kwanza Mwenyezi Mungu kwa yote aliyonijalia mpaka leo hii nikaweza kuwepo mahali hapa. Lakini pili, niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Lupembe kwa imani kubwa waliyoiweka juu yangu mimi wakanichagua na kuwawakilisha katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais ni nzuri sana na kwa kupitia hotuba hii wananchi wa Jimbo langu la Lupembe na wananchi wote wa Tanzania wameifurahia sana, kwani inaonyesha mwelekeo mzuri na matumaini mazuri ya kimaendeleo hasa kiuchumi lakini pia maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yake Mheshimiwa Rais ya tarehe 20 Novemba alieleza sana juu ya viwanda hasa viwanda vidogo vidogo ambavyo vinaajiri watu wengi sana. Viwanda hivi vimekuwa vikiajiri watu wengi na hivi viwanda ni vile viwanda vinavyohusika sana na usindikaji wa mazao mbalimbali kwa ajili ya kuongeza thamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu la Lupembe tuna kiwanda cha muda mrefu sana, Kiwanda cha Chai Igombola ambacho hivi sasa ninavyoongea kwa takribani miaka zaidi ya nane kiwanda hiki kimefungwa, kilifungwa tarehe moja mwezi wa nane mwaka 2008, kutokana na mgogoro uliokuwepo kati ya Wakulima na Mwekezaji. Naomba Serikali ijitahidi au ifanye jitihada za kuhakikisha kwamba kiwanda hiki kinafunguliwa ili wananchi wale wa Lupembe waweze kuuza mazao yao ya chai, lakini pia tuweze kuimarisha uchumi na hatimaye Serikali ikaweza kukusanya kodi kutokana na mishahara ambayo itatokana na wafanyakazi watakaokuwa wameajiriwa pale, lakini pia

iweze kupata tozo kwa maana ya kodi kwenye kiwanda kile na hatimaye kuweza kuinua uchumi wa wananchi wa Lupembe ambao umezorota sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichukue nafasi hii kuelezea kidogo juu ya zao letu la chai. Zao hili limekuwa likilimwa maeneo yangu na ndiyo zao kuu tunalolitegemea sana sisi wana Lupembe. Lupembe ipo Halmshauri ya Wilaya ya Njombe, mnafahamu wote ni Halmashauri ya zamani sana hii, na Lupembe ilikuwa ni miongoni mwa maeneo hapa nchini yanayoongoza kwa ulimaji wa chai. Lakini zao hili la chai limekuwa likiuzwa kwa bei ndogo sana ukilinganisha na bei za uzalishaji wa zao hili. Sasa hivi linauzwa kwa shilingi mia mbili hamsini lakini bei ya uzalishaji, gharama za uzalishaji, ukijumlisha zote za kuuzia, gharama za uzalishaji wa kilo moja ya chai ni shilingi 450/=. Kwa hiyo wakulima hawa wanafanya hiki kilimo kwa hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali iweze kuziangalia kodi mbalimbali ambazo zimeingizwa kwenye zao hili ili ziweze kupungua na hatimaye wakulima wa Lupembe waweze kupata faida kutokana na zao hili la chai.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niweze kuongelea kidogo juu ya elimu, tumesema kwamba Serikali hii sasa kwanza wananchi wangu wamefurahi baada ya Mheshimia Rais kutangaza kwamba sasa elimu ni bure. Kwa hiyo, wananchi wengi waliokuwa wanashindwa kupeleka watoto wao shule sasa wataweza na wameshaanza kupeleka kwa wingi sana. Lakini kupeleka wanafunzi wengi haisaidii kama hatujatengeneza mazingira mazuri kwenye shule hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu moja wapo niiongelee kidogo ni kuhusu walimu hususani madaraja ya walimu, upangaji wa madaraja ya walimu ya mishahara, kumekuwa na tatizo kubwa sana, walimu wamekuwa wakilalamika. Utakuta kwa mfano, mwalimu amefanya kazi miaka saba, nane akiwa na *level* ya *diploma* anaenda kusoma *degree*, anaporudi anapewa daraja lile la "D" halafu anapewa daraja bila kupewa mshahara. Tunaita anapata *dry promotion*, sasa *dry promotion* zimekuwa zikikatisha sana tamaa kwa walimu kufanyakazi. Kwa hiyo, tusipoboresha kwenye upande wa walimu hasa madaraja wanapopata *promotion* ni vizuri yaendane na malipo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachofanyika sasa hivi utakuta kwamba mwalimu anaporudi kutoka chuoni kwenda kufundisha wakati alikuwa amefanya kazi muda mrefu anaenda kuanza ngazi ya mshahara sawasawa na yule kijana au mwanachuo anayeanza kazi. Sasa hii inawakatisha tamaa walimu wengi sana na ndiyo maana utakuta tunasomesha walimu wengi lakini mwisho wa siku walimu wanaamua kuhama kada wanahamia kada nyingine, kwa kuwa wanaona kada hizi za walimu kidogo zinausumbufu na maslahi yake yapo duni. Naomba Serikali iangalie uwezekano wa kurekebisha utaratibu huo,

mimi naamini kwamba ingekuwa ni vizuri kama mwalimu amefanya kazi ameenda kusoma anaporudi basi angalau aongezee ngazi ya mshahara nzuri zaidi kuliko wale wenzake waliobaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilivyo sasa hivi utakuta kwamba wenzake waliobaki ambao hawajaenda kusoma wanakuwa na mshahara mkubwa zaidi, wanapewa daraja zuri zaidi kuliko yule aliyeenda kusoma. Kwa hiyo, kwa kada ya walimu kusoma sasa imekuwa kama ni adhabu. Tunaomba Serikali iweze kurekebisha jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niseme kidogo juu ya huduma ya afya. Jimbo langu la Lupembe ambayo ndiyo Halmashauri ya Wilaya ya Njombe mpaka leo hii haina hata hospitali moja na mpaka leo hii ina kituo cha afya kimoja, Halmashauri nzima, Jimbo zima na zahanati ndogo ndogo na vituo vya afya vingine viwili ambavyo bado vipo kwenye ujenzi. Wananchi wale wanapata shida sana ili waweze kujifungua hasa kwa *operation* kuna baadhi ya wananchi wanatembea kilometa mia moja arobaini na saba kwenda kutafuta Hospitali ya Kibena ili waweze kupata *operation* za uzazi. Naomba Serikali ijaribu kuliona hili jambo la muhimu sana tunaomba tupewe hospitali ya Wilaya lakini pia vituo vyetu hivi vitatu viweze kuboreshwa viwe na huduma ya *operation* kwa maana ya *theatre* ili akina mama wasiteseke kutembea umbali mrefu na wengine kupoteza maisha kwa sababu ya kukosa huduma ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kidogo juu ya wastaafu. Wastaafu waliostaafu kuanzia mwezi wa sita mpaka mwezi Disemba hawajalipwa mafao yao wanataabika huko, wanalalamika na wanailaumu Serikali. Kwa hiyo tunaomba Waziri mwenye dhamana aweze kuchukua jitihada ya kuhakikisha kwamba hawa wastaafu wetu waliofanya kazi muda mrefu, waliojenga Taifa hili wanapata mafao yao haraka ili waendelee kuishi vizuri na kufurahia kustaafu kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongee kidogo juu ya jambo moja kuhusu umeme, Jimbo langu Halmashauri ya Wilaya ya Njombe sehemu kubwa halina umeme. Tuna vijiji 49 lakini vijiji tisa tu ndivyo vyenye umeme. Namuomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na sisi pia atufikirie kule kijijini tuweze kupata huduma ya umeme ili tujisikie na sisi ni miongoni mwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niongee jambo kidogo kuhusu maji. Katika Jimbo langu la Lupembe na ndiyo Halmashauri ya Wilaya ya Njombe vijiji vingi havina maji, mpaka sasa hivi ni vijiji nane tu ndivyo vyenye maji. Sasa kwa hali hii ndugu zangu au Serikali tunaomba mtuangalie na sisi tupate maji kama alivyosema Rais hii Serikali ni Serikali ya kuwatua kina mama ndoo ya maji, basi mtutue na sisi kule Wanalupembe na sisi tujisikie kwamba wake zetu, mama zetu, wanafurahia maisha kwa kutuliwa ndoo za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nisema kidogo juu ya Halmashauri yetu ya Wilaya ya Njombe ipo kwenye Halmashauri nyingine, ipo kwenye Halmashauri ya Mji wa Njombe. Sasa Watendaji wengi na wananchi wengi wanapata shida sana kupata huduma na ile ni Halmashauri Mama ni Halmashauri ya zamani sana. Sasa hivi ukienda hakuna hata gari moja……

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hongoli muda wako umekwisha.

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, ahsante sana na naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Karibu sana. Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla atafuatiwa na Mheshimiwa Kemirembe Lwota.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja hii. Kwanza kabisa na mimi nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwa na afya njema na kuwa mahali hapa leo hii, na kwa moyo wa dhati nichukue fursa hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu kwa hotuba nzuri na zaidi kwa mengi ambayo anawatayarishia Watanzania kupitia hotuba yake.

Mheshimwia Naibu Spika, wananchi wa Tanzania wamemuunga mkono sana Mheshimwia Rais kupitia hotuba yake na kwa hakika Tanzania nzima inampongeza, Afrika inampongeza na dunia inampongeza Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais ameainisha maeneo mengi muhimu kwa maendeleo ya haraka ya nchi yetu. Vilevile ameainisha kero na malalamiko mengi sana ya Watanzania na baada ya kuainisha kupitia hotuba yake akatuletea sisi Wabunge wasaidizi wake ambao anatutarajia tuweze kumsaida katika kutatua kero hizo na malalamiko ya wananchi, alijua mahali pa kupeleka akijua kwamba Wabunge bila kujali kwamba ni wa chama gani wote ndiyo wananchi wanawategemea. Sasa kilichonishangaza mimi na kunisikitisha ni kujiuliza kwamba hivi wananchi wameiopokea na kuipongeza hotuba ya Rais na bila kujali itikadi. Amekwenda kila Jimbo akaainisha kero na malalamiko ya wananchi, sasa hawa wenzetu ambao hawakutaka kusikiliza hizi kero na malalamiko ya wananchi wanamwakilisha nani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningewaona mashujaa kama siku ile wangemsikiliza Mheshimiwa Rais, wakaona hotuba ile inasema nini na basi leo ama jana tulivyoanza kuchangia kwa kuona kwamba haiwafai basi wakatoka. Lakni tukashangaa wanaendelea kunga'nga'nia kujaribu kuchangia jambo ambalo hawakuweza kukubaliana naye. Lakini ya Mungu mengi niachie hapo.

Mheshimwia Naibu Spika, naomba nichangie kidogo sekta ya ardhi. Ardhi yetu imekuwa na thamani kubwa sana na inaendelea kuwa na thamani, tena kwa kasi kubwa sana, na hivyo kadri watu tunavyoongezeka na mifugo na mahitaji ya ardhi, kunakuwa na mahitaji makubwa ambayo ardhi inaendelea kuwa finyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa mfano, kule kwetu Manyara kuna migogoro kila Wilaya na hasa kufuatia uhaba wa ardhi. Ukienda Wilaya ya Kiteto kuna migogoro, ukienda Wilaya ya Mbulu, ukienda Wilaya ya Hanang, ukienda Wilaya ya Babati, Simanjiro kote kuna migogoro kutokana na uhaba wa ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mapendekezo mazuri ya Mheshimwia Rais na maainisho yote ya kwenye *framework* ya mpango wa miaka mitano mimi naomba kutoa mawazo ya ziada. Nchi yetu tumejaliwa kuwa na mapori makubwa sana ambayo mengineyo yana-*potential* kubwa ya kuweza kuzalisha mazao na hasa kutumika kwa ufungaji. Sasa ninaomba kwa sababu wananchi wenyewe hawawezi kuyawezesha hayo mapori ili yaweze kutumika kwa kilimo na ufugaji, naiomba Serikali itenge bajeti ya maksudi kabisa, ili iweze kusaidia kuwezesha haya mapori makubwa ambayo ni *potential* yaweze kutumika kwa ajili ya kilimo na kwa ajili ya ufugaji na zaidi sana kwa ajili ya uwekezaji vilevile kwa sababu tunakwenda kwenye Tanzania ya viwanda.

Mheshimwia Naibu Spika, katika Mkoa wetu wa Manyara pia sasa hivi, kuna wimbi kubwa la wizi wa mifugo, wafugaji wanawaibia wakulima mifugo yao ikiwa ni njia mojawapo ya kuwafukuza wale wakulima ili waweze kuwaachia maeneo hayo waweze kuingiza mifugo yao. Sasa hii ni tabia inayopelekea mauaji, naiomba Serikali iweze kubuni ni namna gani wanaweza wakaikomesha hii tabia ya wizi wa mifugo ambayo pia inapelekea mauaji. Itakapotoa tamko ya kuhakisha kwamba Serikali imetoa tamko kuhakikisha kwamba inatoa adhabu kali kama fundisho wimbi hilo la wizi wa mifugo linaweza likapungua na wananchi watafanya shughuli zao kwa amani na utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ya viwanda tunaiona na kwa hakika mimi nakubaliana nayo, viwanda vitajenga uchumi wetu kwa haraka na kuongeza Pato letu la Taifa. Ninakubaliana na mapendekezo yote yaliyopo kwenye Hotuba ya Rais wetu, lakini vilevile niombe kwamba Mkoa wetu sisi wa Manyara ni maarufu sana kwa kilimo cha mazao hasa vitunguu swaumu. Najua vitunguu swaumu siyo zao lililozoeleka, niwahakikishie lina soko hata nje ya nchi. Ninaiomba Serikali wakati ukifika tuweze kufikiria kuweka kiwanda katika Mkoa wetu wa Manyara hususani Wilaya ya Mbulu ambapo tunalima kwa wingi sana zao hili ambalo kwa sasa hivi soko lake halina uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kidogo kuhusu matumizi ya shilingi milioni 50 alizoahidi Rais wetu. Tuna mifano mingi sana ya fedha za aina hiyo ikiwepo mabilioni ya Kikwete ambayo tuliyasikia kipindi kilichopita, lakini vilevile asilimia 10 ya fedha zinazotengwa na Halmashauri kwa ajili ya vikundi vya wanawake na vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi kwa bahati mbaya hazikuwekewa mfumo mzuri ambao ungeweza kuwafikia walengwa. Ninaiomba Serikali itakapofikia wakati huo wa kutupa shilingi milioni 50 kwa kila kijiji na hasa kwa kuwawezesha wanawake na vijana na makundi mengine. Tuangalie isije ikaenda kwenye mfumo huo huo wa upotevu bali tuiwekee utaratibu mahsusi, bila haraka yoyote kuhakikisha kwamba kunakuwa na taaluma ya kutosha ili fedha hizi ziweze kuwafikia walengwa waweze kufanya kazi iliyokusudiwa na hivyo kufikisha dhamira ya Rais iliyo njema ya kuwawezesha wajasiriamali wadogo waweze kufanya kazi yao kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa na haya machache naunga mkono hoja na naendelea kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu kwa juhudi kubwa anayoiweka katika kuliongoza Taifa letu, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Kemirembe Lwote.

MHE. KEMIREMBE J. LWOTA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kukushukuru wewe kwa kuweza kunipa nafasi hii ya kuchangia, vilevile napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunifikisha hapa siku hii ya leo na kuwashukuru wanawake wote wa Mwanza walionipigia kura kwa wingi kabisa nasema ahsanteni wote na ninawaahidi sitowaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kushukuru na kumpongeza Rais wetu John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri ambayo anaendelea kufanya na hotuba nzuri sana aliyotufungulia Bunge letu hili.

Vilevile napenda kuwapongeza Mawaziri wote walioteuliwa na Mheshimiwa Magufuli, amewaamini na sisi wote tunawaaamini na tunaona kazi mnazozifanya na tunawapongeza tunasema kazeni buti tuko nyuma yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa kuunga mkono asilimia mia moja hotuba ya Mheshimiwa Rais. Mambo aliyeyasema kwenye hotuba yake ni mengi yamehusisha nyanja zote, kwa Mtanzania na kwa maendeleo ya Tanzania yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais ameongelea suala la miundombinu, ameongelea suala la reli na suala barabara. Kwanza kabisa napenda kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri inayofanya kwenye barabara zetu, wote ni mashahidi, barabara zimeunganishwa, Mikoa tofauti mingi imeunganishwa kwa lami na wote tunafahamu. Mheshimiwa Rais alishawahi kutoa mfano humu Bungeni akasema barabara za lami zilizopo Tanzania zingekuwa Burundi wasingepata hata sehemu ya kulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo natoa pongezi sana kwa mambo yanayofanyika na Serikali yetu ya Cha cha Mapinduzi. Napenda nijikite kwenye suala la barabara baada ya mvua za *elnino* zilizoanza kunyesha hivi karibuni mwezi Novemba Mkoa wa Mwanza tulipata matatizo makubwa ya maafa, watu walipoteza maisha. Lakini vilevile barabara zetu zimeharibika sana kwa Majimbo yote mawili ya Mjini, nikiwa na maana ya Jimbo la Ilemela na Nyamagana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uharibifu huo, jitihada zilifanyika kwenye Halmashauri zetu, Halmashauri zikaandika barua TAMISEMI, TAMISEMI wakatuma wataalam wakaja Mkoa wa Mwanza, wakazunguka na ma-*engineer* wetu wa Wilaya zote mbili na wakaona uharibifu zaidi umefanyika kwenye Wilaya ya Ilemela.

Mheshimiwa Spika, utafiti huo ulifanyika mwezi Novemba na baada ya hapo mvua zimeendelea kunyesha sana, na mpaka hivi tunavyoongea mvua zinanyesha na barabara za Mwanza hususani Ilemela zimekatika kabisa. Baada ya wataalam hao kuja, walifanya *emergence plan* kana kwamba barabara za Mwanza hususani za Ilemela zitengewe fedha na zije zitnegenezwe, lakini mpaka sasa hivi ninavyoongea jambo hilo halijafanyika, barabara hizi ambazo zimekatika kabisa zinafanya wananchi wetu wanashindwa kufika mahali wanapotaka kwenda kwa wakati, gharama za usafiri kwa maeneo yanayopitika zimekua juu, akina Mama wajawazito wanashindwa kufika hospitali kwa wakati, wanajifungulia barabani, hali kwakweli ya barabara ni mbaya. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya barabara ambazo zimeharibika sana naweza kuzitaja. Mojawapo ni barabara ya Kirumba – Mwaloni ambayo inaenda kwenye soko letu la samaki la kimataifa. Barabara hii inaingiza fedha nyingi sana kwenye Halmashauri ya Ilemela na Serikali kwa ujumla wake, lakini barabara hii sasa hivi imekatika kabisa, maroli na magari makubwa yanashindwa kupita. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna barabara ya Kiseke *PPF;* barabara ya Busweru - *National* na barabara ya Bwiru.Tunamuomba Mheshimiwa Waziri

wa Ujenzi, Miundombinu kama kuna uwezekano hili suala litatuliwe kwa sababu hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni Waziri alifika Mkoa wa Mwanza akatoa ahadi ya kujenga barabara ya lami inayotoka Sabasaba kwenda Busweru. Barabara hiyo hali ni mbaya na safari hii mpaka barabara imefungwa yaani haitumiki tena, kwa hiyo, tunaomba kwenye bajeti hii inayokuja tutengewe hizo fedha za huu mradi ambao Mheshimiwa Waziri ametupa ahadi na utekelezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kuchangia kwenye masuala ya afya, wote ni mashahidi masuala ya afya wote ni mashahidi hotuba ya Mheshimiwa Rais, aliongolea suala la afya kwenye kurasa za mbele kabisa za hotuba yake na wote ni mashahidi tumemwona baada ya kuapishwa siku chache ya sehemu ambazo amezitembelea ni Muhimbili na amejionea changamoto zilizopo kwenye hospitali zetu za Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zilizopo Muhimbili hazina tofauti sana na changamoto zilizopo Mkoani kwetu Mwanza. Tuna hospitali ya *referral* ya Sekou Toure. Hospitali hii inahudumia watu wengi sana na inatoa huduma nzuri sana na ndiyo maana nadhani watu wanakuwa wengi na wazee, akina mama na watoto wanahudumiwa bure. Napenda kupongeza Serikali kwa jitihada hizi wanazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini changamoto bado ni nyingi vilevile hapo tulipo. Moja ni ufinyu wa bajeti, bajeti inayotakiwa kwenda kwenye hospitali yetu ya Sekou Toure haiendi kwa wakati na ikienda haiendi bajeti kamili. Najua Waziri na Naibu Waziri sasa hivi tumepata ni wachapakazi na nina imani haya mambo tunayoongea hapa yatatekelezeka.

Mheshimiwa naibu Spika, kuna suala la vifaa tiba. Changamoto za vifaa tiba pia ni nyingi pale, hospitali inahudumia watu wengi x-*ray* iliyopo ni moja na ni *x-ray* ambayo imekuwepo tangu hiyo hospitali inaanzishwa. Kwa hiyo tunaomba Mheshimiwa Waziri utusaidie kwa hilo, ni hospitali ambayo inahudumia wakazi wengi sana wa Mwanza na mikoa ya jirani.

Mheshimiwa Spika, suala lingine nilitaka kuongelea ni kuhusu afya ni kuhusu hospitali ya Wilaya ya Ilemela. Hospitali hii tunashukuru sana Serikali kwa sababu inaendelea vizuri, imeshapewa hela *almost 80 percent* ya kazi zinazotakiwa kufanya, kwa hiyo iliyobaki ili hospitali ikamilike tuweze kupata hospitali ya Wilaya ya Ilemela ni fedha ndogo sana. Tunaomba Mheshimiwa Waziri tunapokuja kujadili bajeti utusaidie kutenga hela za hospitali ya Wilaya ya Ilemela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna kituo cha afya cha Buzuruga. Kituo hiki cha afya kinahudumia wakazi wengi sana wa Mwanza kwa sababu kwa upande wa Ilemela hatuna hospitali ya Wilaya, kwa hiyo watu wengi sana wanajikuta wanaenda kwenye hicho kituo cha afya lakini kituo cha afya hiki pia kina changamoto na hatuna wodi ya wanaume. Kwa hiyo, wanaume wanapokuja kuhudumiwa pale hata kama wanaumwa kiasi gani cha kuwa *admitted* hawawezi kuwa *admitted* kwa sababu hatuna wodi, kwa hiyo tunaomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hili na kutupa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la watoto njiti. Suala hili ni changamoto, watoto hawa kwenye hospitali zetu nyingi kwa Mkoa wa Mwanza hawana wodi za watoto njiti, wodi hazipo watoto hawa wakitokea wamepatikana na matatizo hayo wanachanganywa na wodi za kawaida, yaani katika wanawake waliojifungua kawaida watoto, suala hili ni nyeti sana naomba Mheshimiwa Waziri tuliangalie.

Vilevile vifaa vya kuhudumia watoto hawa kama *incubators, suction machines, feeding tubes,* ni vitu ambavyo gharama yake siyo kubwa sana lakini vinakosekana kwenye hospitali zetu.

Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri tunakuomba utuangalie kwenye hilo suala la watoto njiti na pia kama kuna uwezekano *research* ifanyike, tujue hawa watoto wapo kiasi gani na wanapatikana sana kwenye Wilaya gani ya Tanzania ili tuweze kufanya utafiti na kujua ni kitu gani kinapelekea watoto hao wanakuwa njiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige atafuatiwa na Mheshimiwa Venance Mwamoto, atafuata Mheshimiwa Bonnah Kaluwa. Mheshimiwa Maige!

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na mimi nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwanza kuwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Msalala kwa kunirudisha hapa kwa mara nyingine kwa kura nyingi. Imani yao kwangu nina uhakika italipa kwa sababu uwezo wa kuyatimiza niliyowaahidi kwa kushirikiana na Serikali hii ambayo iko vizuri sana ninaamini kwamba ninao.

Mheshimiwa Spika, naomba kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa ushindi mkubwa alioupata, lakini kipekee nimpongeze sana kwa hatua ambazo ameanza kuzichukua katika kurekebisha hali ya maisha ya Watanzania

kupitia mpango wake wa kusaidia kwenye mambo mengi kama ambavyo amekuwa akiahidi.

Mheshimiwa Spika, Mheshiwa Rais, alituomba Watanzania tumuombee na mimi naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba nimeweka mpango wa kuwa ninafunga angalau mara moja kila mwezi kwa ajili ya kumwombea Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali yake. Katika kumuombea nitakuwa pia nikimsaidia kupitia Serikali yake kuainisha maeneo ambayo majipu yapo katika hatua nzuri ili yaweze kushughulikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yake Mheshimiwa Rais aliainisha mambo mengi lakini ukurasa wa nane alisema ifuatavyo naomba ninukuu kwamba; "Suala la madini nalo limelalamikiwa, wanalalamika wenyeji kutofaidika, vilio vya wachimbaji wadogo wadogo kutengewa maeneo ya uchimbaji na kupatiwa mikopo, kutolipa kodi stahiki, usumbufu wa kulipa fidia na kadhalika."

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa leo naomba nijikite kwenye hili eneo, Wilaya ya Kahama tuna migodi miwili, Mgodi wa Bulyanhulu na Mgodi wa Buzwagi. Eneo hili ni chanzo kikubwa sana cha mapato kwa Serikali na ni chanzo kikubwa cha mapato kwa wananchi ambao wanazunguka migodi hiyo. Tumekuwa tukilalamika kila wakati, niipongeze Serikali ya awamu iliyopita ya Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa hatua ambazo ilichukua kurekebisha mikataba. Itakumbukwa aliunda Tume iliyoongozwa na Jaji Mark Bomani, mimi na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge akiwemo Mheshimiwa Waziri Mwakyembe tulikuwa Wajumbe na kupitia Tume hiyo kulifanyika mabadiliko kadhaa ambayo yamepelekea kuongezeka kwa mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba niiombe Serikali, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Pofesa Muhongo kwa hatua ambazo ameanza kuchukua kutusaidia kwenye eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukilalamika kwamba wananchi wa maeneo ya migodi hatunufaiki na madini, kwanza kwa sababu migodi hii hailipi kodi sawasawa kwenye Halmashauri, lakini pili, *procurement* zake nyingi wamekuwa wakinunua vifaa vingi kutoka maeneo ya mbali ya migodi na mbaya zaidi miradi ya ujirani mwema, wamekuwa wakichangia kidogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka mwaka 2014 Mheshimiwa Profesa Muhongo alisimamia mazungumzo baina ya Mgodi na Serikali kwa upande mmoja lakini na sisi wananchi wa maeneo jirani hatimaye Mgodi wa Bulyanhulu, Buzwagi na mingine wakakubali kuanza kulipa ushuru wa huduma kwa Halmashauri kwa asilimia 0.3. Hatua hiyo imesaidia kuongeza mapato ya

Halmashauri lakini kama ambavyo Mheshimiwa Waziri utakumbuka katika mazungumzo yale tulikufahamisha, tunaomba uendelee kutusaidia. Hawa jamaa ni jeuri, na utakumbuka katika mazungumzo kuna baadhi ya mambo waliyakubali lakini utekelezaji wake umekuwa wa kusuasua kwa mfano walisema watakuwa wanalipa hiyo *service levy* kila robo mwaka, sasa hivi inafika mpaka nusu mwaka hawajalipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini baya zaidi, tulisema kwamba kwa mfano Mgodi wa wa Bulyanhulu umeanza uzalishaji mwaka 2000 na toka wakati huo hawajawahi kuzalisha dhahabu ya chini ya thamani ya dola za Kimarekani milioni 500, ukipiga hesabu ya asilimia 0.3 ya dola milioni 500 ni fedha nyingi sana. Kwa hesabu nilizofanya Halmashauri ya Wilaya ya Msasala inapaswa katika kipindi hicho cha miaka 15 iwe imelipwa kutoka Mgodi wa Bulyanhulu dola za Kimarekani zisizopungua milioni 13 hivi sasa wanatulipa milioni 700, milioni 600 ambazo ni kidogo kuliko tunavyotaka.

Mheshimiwa Waziri, naiomba Serikali kusaidia kama ambavyo tulikuwa tumeanzia, mtusaidie tulipwe madeni yetu dola milioni 12 tunazodai Mgodi wa Bulyanhulu ambayo ni 0.3% kutoa dola 200,000 ambazo wamekua wakilipa, ile *difference* ile toka mwaka 2000 ni karibu dola milioni 12, fedha hizo zikilipwa ninaamini kwamba maisha ya wananchi yataboreka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, naomba nimwombe Waziri atusaidie sana katika utekelezaji wa miradi ya ujirani mwema hawa watu wamekuwa hawana imani na Taasisi za Serikali, wamekuwa wakiitekeleza wao wenyewe na kwa mara nyingi wamekuwa wakitekeleza miradi kwa gharama kubwa, kwa mfano, wametujengea kituo cha afya pale Bugalama kwa thamani ya shilingi milioni 850.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zile zingetolewa kwenye Halmashauri, tukajenga sisi kama ambavyo tunajenga miradi mingine milioni 850 tungemaliza kujenga angalau majengo mengi zaidi yenye uwezo wa ku-*accomodate* hata huduma za kihospitali yenye hadhi ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba, Mheshimiwa Waziri atusaidie mazungumzo ambayo bado yanaendelea kati yetu na wawekezaji hawa waweze kuziamini Taasisi za Serikali, waiamini Halmshauri ili wanapotekeleza miradi ya ujirani mwema kwa kiasi kikubwa itekelezwe kwa *modality* ambayo Halmashauri yenyewe itasimamia, na kwa kufanya hivyo tutaweza kupata *value for money*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hivi tatizo la sheria ya manunuzi ambalo tunalilalamikia Serikali, kule mgodini ndiyo liko kubwa zaidi, kwa sababu

unakuta shule ambayo ingeweza kujengwa kwa milioni 50, milioni 80, wao wanasema wamejenga kwa milioni 300, milioni 400. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo katika mazunguzo hayo tumekuwa na kilio cha wananchi waliondolewa kwenye eneo la Mgodi wa Bulyanhulu mwaka 1996. Waliondolewa bila fidia, tumefanya mazungumzo haya kupitia awamu iliyopita na Mawaziri kadhaa, Profesa Muhongo ulianza kuchukua hatua nzuri za kukaa chini kuzungumza na hawa watu niombe katika mazungumzo ambayo umekua nayo, na nipongeze sana jitihada ambazo umekuwa ukizifanya na nimshukuru Mungu kwa kurudishwa kwenye hii Wizara. Kwa sababu *institutional memory* imekuwepo, haya ninayoyasema unayajua, naamini kwamba utatusaidia tuzungumze waweze kulipa fidia kwa wananchi waliokuwa waki-*occupy* lile eneo ambao waliondolewa mwaka 1996 bila fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dakika chache zilizobaki naomba Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi anisikilize vizuri. Kuna tatizo la Mwakata tulipata maafa tarehe 3 Machi, mwaka jana watu 47 wakafa, wananchi kaya zaidi ya 650 zikakosa makazi, Waziri Mkuu akaja, Rais akaja, na mkaahidi kwamba mngesaidia kujenga nyumba mia tatu na kitu. Mpaka leo hii wale watu wanaishi kwenye maturubai, hizi mvua zinazonyesha zinawanyeshea, ni kitu ambacho hakiaminiki kabisa kwa sababu Serikali ilikuwa inaahidi na kwamba tulitegemea jambo hili lingetekelezwa kwa dharura katika kipindi cha mwezi mmoja, miwili na ndiyo maana ya kuwapa maturubai.

Leo, wale watu wanakaa kama wakambizi, nyumba zilizojengwa ni tatu ambazo zimetoka kwa wafadhili wa Mgodi wa Bulyanhulu pamoja na wafadhili wengine. Msaada au ahadi iliyotolewa na Rais kwamba nyumba zile zingejengwa hakuna kilichofanyika hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kasi ambayo Mheshimiwa Rais anayo, ninaomba sana Mheshimiwa Jenista, baada ya hapa hatua inayofuata ni kufuatana na mimi tena twende mapema iwezekanavyo. Twende pale Mwakata, eeh Mheshimiwa Mwamoto anasema na yeye awepo kwenye msafara huo, twende Mwakata ukawaeleze wananchi ni nini na lini nyumba hizo zitajengwa. Wale wananchi wanaishi maisha ya kisikitisha sana kwa sababu hawana nyumba na wanamatumaini ya kujengewa nyumba na Serikali yao, na ninaamini Serikali yetu sikivu itaweza kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ni ahadi ya kupeleka maji kwenye Mji mdogo wa Isaka pamoja na Mji mdogo wa Kagongwa na baadae yaende hadi Tinde. Hii ni ahadi iliyotolewa na Serikali iliyopita toka mwaka 2008, najua limekuwepo tatizo la fedha lakini tumekuwa tukiahidiwa kila wakati nakumbuka kwenye Bunge lililopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, nitazungumza tena siku nyingine. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Venance Mwamoto.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia. Nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kweli kwa kunifanya niwe mzima mpaka leo lakini niwashukuru sana Wananchi wa Kilolo ambao wamenirudisha baada ya miaka kumi kutoka hapa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais iko vizuri na jana wenzetu walipotoka nje, bahati nzuri mimi nilipata bahati ya kuwa wa kwanza kutoka lakini kikubwa kilichofanya watoke ni kwamba hawana sehemu ya kuchangia. Sasa kwenye ile hotuba kama hauna sehemu ya kuchangia itakuwa siyo rahisi ubaki humu ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili wenzetu wanataka kuonekana *Live*. Mimi nilikuwa Mkuu wa Wilaya ya Kibondo, kuna watu walikuwa wanajua kuzungumza humu ndani mnawajua sitaki kuwataja na ilikuwa wakati anachanga unakuta vikundi vimeshajikusanya ukiuliza kuna nini wanakwambia leo jamaa anaongea na anataka kumchana *live* Waziri Mkuu, sasa nafasi hiyo haipo tena.

Kwa hiyo, wenyewe wanataka kuendelea kucheza *live* humu ndani lakini ukiangalia maendeleo kwenye maeneo yao hakuna, na walio wengi ninyi wenyewe mnahakika kabisa hawakurudi waliokuwa wanazungumza sana humu ndani. Wananchi wanataka maendeleo. Wanataka *live* kwenye maendeleo siyo *live* kwenye *TV*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi kwa kweli kwa muda ule ambao umependekezwa ni muda ambao wananchi wengi kweli watakuwa wanaweza kuona kinachofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye suala la maji. Wilaya ya Kilolo, Tarafa ya Mazombe - Ilula kuna tatizo kubwa sana. Mimi nina hakika mwaka 2000/2005 nilipokuwa Mbunge, tulipewa ahadi na Mheshimiwa wakati huo Rais Mkapa suala la maji, bahati nzuri haikuwezekana, wananchi walinihukumu wakanipa likizo, na mwenzangu aliyechukua nafasi yangu aliingia akapewa ahadi nzuri na Rais aliyekuwepo, naye inawezekana ni sababu hiyo hiyo amepewa likizo, sasa juzi alipifika Mheshimiwa Rais kuja kuomba kura tukamwambia sehemu moja nzuri anayotakiwa kwenda ni sehemu ya Ilula ambayo ina tatizo la maji. Aliahidi kwamba suala hilo analichukua, na ana hakika kabisa asilimia 100, akawaambia wananchi kwamba nirudishieni

Mwamoto na nipeni kura, suala la maji limekwisha. Nitawaletea Waziri ambaye anajua matatizo ya maji.

Mheshimiwa Lwenge naomba uandike vizuri hiyo, kwa sababu ili uende kwenu kwenye Jimbo lako ni lazima upite Ilula. Huwezi kunywa maji, huwezi kupita Ilula. Uhakikishe maji yanapatikana na ni ahadi ya Mheshimiwa Rais. Sasa hivi ukienda pale ukimsalimia mtu wa Ilula, maana yake sisi huwa tunasalimiana kule kilugha kamwene, anakwambia maji, ukimwambia kamwene anakwambia maji, ukimwambia kitu chochote anakwambia maji, hapa kazi tu, maji. Sasa dawa yake ni kutoa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ukikaa Ilula ukitaka kupanga chumba unapanga vyumba viwili kama unaanza maisha, unapanga chumba kimoja kwa ajili ya madumu ya maji na chumba kimoja kwa ajili ya kulala wewe. Sasa mimi nawaomba, kwa sababu ni ahadi ya Rais na Mheshimia Lukuvi naomba unisaidie, mimi mdogo wako nipo nisiondoke tena unisaidie maji na maji mengine kwako kule tutakuletea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilula hakuna tatizo la maji, tatizo lake ni mgawanyo wa maji, maji yapo mengi, kuna mito mingi pale lakini unaifikishaje kwa wananchi ndiyo tatizo. Kwa hiyo, mimi naomba, Mheshimiwa Lwenge tuende pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la barabara. Kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, iko wazi kabisa kwamba kila Wilaya barabara itaunganishwa kwa lami mpaka Makao Makuu ya Mkoa, lakini pia na kufanya uwezekano mkubwa na kuunganishwa na Wilaya nyingine.

Wilaya ya Kilolo toka mwaka 2002 mpaka sasa katika kilomita 35, kilomita zilizojengwa kwa lami ni kilomita saba, sasa sielewi ni kwa nini. Kwa hiyo kwa kuwa Profesa Mbarawa nilishazungumza naye, tutaona jinsi ya kutusaidia, lakini ni pamoja na kutuunganisha ile barabara ya *TANROAD* inaishia Idete, tulishaipitisha kwenye mpango wa barabara ya *TANROAD* kwamba iishie sasa Muhanga ili tuunganike na watu wa Morogoro, kwamba itoke Kilolo - Dabaga - Idete - Itonya ifike mpaka Muhanga ili tuende mpaka Mbingu kule Kilombero, Morogoro tuweze kuunganisha nao ili tuweze kufungua uchumi wetu kwa sababu uchumi wa Kilolo unategemea sana Kilimo na ili wananchi wale wapate fedha inabidi wauze mazao yao yale lakini kama barabara zitakuwa ni shida watanyanyaswa, watauza mazao yao kwa bei ambayo haifai.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la pembejeo za kilimo. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo alifika Iringa na tukamwambia matatizo ya pembejeo. Lakini tatizo la Pembejeo Mheshimiwa Waziri wa Kilimo naona unanisikia, naomba hebu washikirishe Wakuu wa Wilaya kwenye suala

hili la usambazaji wa pembejeo na ikiwezekana Wakuu wa Wilaya wasiwe Wenyeviti wa pembejeo kwa sababu wao ndiyo wanatakiwa wasimamie, kwa hiyo linapotokea tatizo hakuna wa kumuuliza! Mkurugenzi yupo mle, Mkuu wa Wilaya yupo mle, wao wasimamie tu mwenendo mzima wa pembejeo kwa sababu kuna ujanja mwingi sana kwenye pembejeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi ndiyo wanapeleka mbegu Kilolo wakati sasa hivi ni wakati wa kupalilia, wanatakiwa wapeleke mbolea ya kukuzia, kwa hiyo kuna matatizo pale, tunaomba utusaide. Lakini pia na bei ya mbolea iko juu sana, tuangalie uwezekano wa kupunguza kama ni kodi, kama mambo mengine basi yapungue.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie pia suala la Mabaraza ya Kata. Mheshimiwa Waziri wa Sheria yupo, TAMISEMI yupo, Utawala Bora yupo, Wizara ya Mambo ya Ndani yupo. Mabaraza ya Kata kuna tatizo, tatizo ambalo lipo wanaoendesha hayo Mabaraza uwezo wao ni mdogo, hawapati mafunzo, lakini kazi ile ni kubwa sana na wamesaidia sana kutatua migogoro.

Kwa hiyo mimi nikuombeni tusaidiane kwenye hilo sambamba na madawati ya jinsia. Mheshimiwa Kitwanga, madawati ya jinsia yamesaidia sana kupunguza kero nyingi sana lakini matatizo ambalo lipo, yale Mabaraza ni vema ofisi zikawa kwa Mkuu wa Wilaya, kwa sababu watu walio wengi Mheshimiwa ukipigwa kibao na mke wako unaona aibu kwenda Polisi lakini ikiwa kwenye Baraza anahisi ni sehemu ya usuluhisho kwa hiyo inakuwa rahisi kwenda na kutoa elimu. Maana yake madawati ya jinsia siyo wanawake peke yake, hata wanaume. *(Makofi)*

Mimi naomba ikiwezekana tuma watu wako waende pale Kibondo wakaone lile Dawati linavyoendeshwa na kesi nyingi pale ni za wanaume kushtaki kwa kupigwa tena. Kwa hiyo unaona jinsi ambavyo elimu imefika kule. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ni suala la ujenzi wa ofisi, Wilaya ya Kilolo toka mwaka 2002 tumekuwa Wilaya lakini Mheshimiwa Kitwanga huna hata jengo moja ambalo limejengwa. Huna Makao Makuu ya Polisi ya Wilaya, huna nyumba ya Polisi Wilaya ya Kilolo. Kwa hiyo mimi naomba, baada ya Bunge hili mimi tutakwenda pamoja na nitachangia na mafuta maana haukuwa mpango wako ili tuende ukaone hali jinsi ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia na suala la hospitali hamna hospitali Wilaya ya Kilolo. Majengo yapo pale lakini mpaka leo hakuna hospitali ya Wilaya na kuna majengo ambayo wananchi wamejitolea wamejenga zahanati lakini hazijaisha, wamejenga vituo vya afya havijaisha, ukiwauliza wanakuambia

bajeti tuliomba lakini tumeletewa bajeti finyu. Kwa hiyo nafikiri Mheshimiwa Kigwangalla tusimsumbue Mheshimiwa Waziri, tuende ukaone hali jinsi ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa muda bado ninao, kuna hili sula la uchangiaji wa elimu ambapo Mheshimiwa Rais amefuta...

Mheshimiwa Naibu Spika, basi naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Muda wako umeisha Mheshimiwa Mwamoto naomba ukae. Mheshimiwa Bonnah Kaluwa.

MHE. BONNAH M. KALUWA: Mheshimiwa Naibu Spika, naitwa Bonnah Kaluwa Mbunge wa Jimbo la Segerea. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunileta hapa katika Bunge lako Tukufu na kuweza kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba pia niwashukuru wananchi wangu au wanachama wenzangu wa Jimbo la Segerea wa Chama cha Mapinduzi ambao waliweza kunipa tiketi ya kuja hapa bila kuwasahau wananchi wa vyama vya siasa kwa jina maarufu vyama vya UKAWA lakini pia wananchi wote wa Jimbo la Segerea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa kwa dhati kumuunga mkono Mheshimiwa Rais John Joseph Pombe Magufuli kwa hotuba yake aliyoitoa siku ya tarehe 20 Novemba, 2015 ilikuwa hotuba nzuri ambayo ililenga kuwatatulia matatizo wananchi wetu.

Napenda nianze kwa kuchaangia katika suala la elimu. Napenda nitoe shukrani zangu za dhati na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Segerea, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuondoa michango mbalimbali ambayo ilikuwepo kwenye shule zetu, kuanzaia shule za msingi mpaka shule za sekondari. Ninaongea hivyo kwa sababu nimekuwa ni mdau wa elimu kwa muda mrefu, tangu nikiwa Diwani nilikuwa nina mfuko ambao ulikuwa unahusika na kulipia watoto ambao wamefaulu lakini hawana uwezo wa kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wengi wameweza kufaidika na hii kauli ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa kwamba watoto wote waende shule na ikiwa shule ni bure na michango mbalimbali kwa sababu walikuwa wanapata shida na watoto wengi waliuwa hawawezi kwenda shuleni au kujiandikisha au wanachelewa kuanza shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kusema hayo naomba sasa nijikite kwenye masuala ya miundombinu ya elimu. Pamoja na Mheshimiwa Rais

kutangaza kwamba elimu itakuwa bure lakini pia kuna changamoto nilikuwa nataka nizishauri kama Mbunge wa Jimbo la Segerea, kwa Jimbo langu ambalo lina shule za msingi 37 ambazo zina matatizo. Pamoja na kwamba shule zetu ni bure kwa sasa, lakini tulikuwa tunamuomba Mheshimiwa Rais aangalie au Mawaziri na watendaji waangalie shule zetu za Jimbo la Segerea zina matatizo makubwa.

Kwanza miundombinu yake siyo mizuri nikiwa na maana kwamba mazingira siyo rafiki kwa watoto ambao wanakwenda shule. Madawati hakuna, watoto wengi wanakaa chini, lakini mifumo mibovu ya vyoo, vyoo ni vibovu, unakuta shule ina watoto 2000 lakini ina matundu ya vyoo mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba shule ni bure lakini tuangalie na matatizo haya ya miundombinu, tunajua ndiyo kwanza tumeanza, changamoto ni nyingi, lakini ninaomba katika bajeti hii ambayo inayokuja, kama tunataka shule zetu ziwe bure na tuweze kutoa viwango vizuri na watoto wetu waweze kufaulu vizuri watoto wa kuanzia shule za msingi, basi tunaomba watutengenezee mazingira rafiki ambayo kwa kawaida watoto wanatakiwa wakae 45 kwenye darasa moja, lakini sasa hivi wanakaa watoto150 kwa hiyo watoto wanarundikana wengi, hata hivyo madarasa yemekuwa ni machakavu sana. Kwa Jiji maarufu kama Dar es salaam, itakuwa ni aibu sana kukuta watoto wanakaa chini. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Waziri aangalie katika Bajeti inayokuja miundombinu ya elimu aiangalie sana katika Jimbo langu ambayo kuna shule nyingi na kuna sehemu zingine kwa sabau sasa hivi tumegawanisha Kata, kuna sehemu zingine hazina hata shule za msingi kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata kama ya Buguruni ambayo ina wananchi wengi karibia 70,000 lakini hawana hata shule ya sekondari wanakwenda kusoma Kata za jirani. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, tunaomba utuangalie sana katika bajeti yako katika miundombinu ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuchangia katika miundombinu ya elimu, naomba nichangie katika masuala ya afya. Jimbo langu la Segerea, kwanza ni Jimbo lenye changamoto nyingi, lina watu wengi, kwa sensa iliyopita tulikuwa tuna watu karibu laki 5 na Jimbo langu la Segrea lina Kata 13, lakini katika Kata 13 tuna zahanati saba, hizi zahanati zote hazina vitendea kazi. Kuna zahanati zingine ambazo hazina hata umeme, wananchi wanakuwa wanapata shida kwa sababu itakapofika saa 12 jioni inabidi ifungwe. Wananchi wengi hawawezi kutibiwa maeneo hayo. Kwa hiyo kutakuwa na mrundikano wa watu wengi ambao wanatoka kwenye Jimbo la Segerea kuelekea hospitali ya Amana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Afya ya mwaka 2010 ilisema kwamba kila Kata inatakiwa kuwa na kituo cha afya na kuangalia kwenye Jimbo langu kwa sababu ya umuhimu wa watu wengi, tunaomba Mheshimiwa Waziri wa afya, atuangalie tupate kituo cha afya kwa sababu mpaka sasa hivi pamoja na kwamba tulikuwa tuna watu 375,000 ambao walijiandikisha kupiga kura lakini Jimbo lenye Kata 13 na lenye watu 375,000 hatuna kituo cha afya. Pamoja na kutokuwa na kituo cha afya, huduma zetu za afya kwenye hizo zahanati ambazo zipo hazikidhi viwango vinavyotolewa. Hakuna madawa, tumesema kwamba watoto kuanzia 0 mpaka miaka mitano wanapata huduma bure lakini wale watoto wakienda wanachokipata pale ni kuandkiwa dawa na kuambiwa muende mkanunue kwa sababu dawa hazipatikani.

Mheshiwa Waziri wa afya, tunaomba utuangalie lakini sambamba na hilo, tunajua kabisa Kata ya Mnyamani tuna mrundikano wa watu wengi lakini pia tuna hospitali moja ambayo pia katika Kata yetu ya Mnyamani kuna Mabwawa ambayo wanayotunzia maji machafu, Mheshimiwa Waziri tunaomba yale mabwawa yaweze kuondoka pale Mnyamani kwa sababu yanaleta hali ya hewa ambayo siyo nzuri kwa sababu yapo karibu na zahanati au na hospitali ambayo ipo kwa wakazi wa Mnyamani na magonjwa mengi ya mlipuko yanatokea Mnyamani kwa sababu mazingira siyo mazuri.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bonnah muda wako umekwisha!

MHE. BONNAH M. KALUWA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Muda wako umekwisha tafadhali naomba ukae, tumsikie Mheshimiwa Halima Bulembo.

MHE. HALIMA A. BULEMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwa majina naitwa Halima Abdallah Bulembo, ni Mbunge wa Viti Maalum kundi la vijana au Mbunge mdogo kuliko wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba kumpongeza Mheshimiwa Rais, katika kipindi alipokuwa akitafuta kura aliahidi kutowaangusha vijana na ukiangalia Baraza lake Mawaziri wengi ni vijana, ukimuangalia kaka yangu Wakili msomi Mavunde ni kijana, kuna Injinia Masauni ni kijana, kuna Dkt. Kigwangalla na kuna Dkt. Possi, tunamuahidi na sisi vijana hatutomuangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, naomba pia kusema kidogo. Nina masikitiko katika suala zima linaloendelea Bungeni, Wabunge wenzetu wa Upinzani kuwa wanatoka. Ningeshauri kale kautaratibu ka posho tungekuwa tunasaini saa 12 jioni tuone pia kama wangekuwa wakitoka? *(Makofi)*.

Baada ya hayo machache, naomba kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake nzuri, ni hotuba yenye kufufua matumaini, ni hotuba yenye kujali wananchi hasa wanyonge, ni hotuba yenye kujali na kuleta nuru na matarajio mapya kwa wananchi na kiukweli Tanzania mpya inaonekana chini ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mimi ni kijana, nitaanza na tatizo sugu la vijana ambalo ni ajira na kaka yangu Mheshimiwa Mavunde naoma unisikilize. Katika hotuba ya Rais, alizungumzia tatizo la ajira kwa vijana. Wote tunafahamu kwamba ajira ni tatizo sugu si kwa Tanzania tu lakini ni kwa dunia nzima. Tatizo hili linahitaji msukumo zaidi wa Kiserikali, Taasisi mbalimbali lakini vilevile linahitaji sisi wenyewe Wabunge tukipata fursa za ajira tuzipeleke kwa vijana, tusisubirie Serikali tu, tukiendelea kusubiria Serikali ifanye kila kitu tutaishia kubaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika suala zima la ajira naomba kuwaambia Watanzania kwamba vijana wengi wanajiajiri na vijana ambao wanakuwa na uwezo wa kujiajiri ni kuanzia umri wa miaka 18 mpaka 35 ambayo ni asilimia 32 ya Watanzania, kwa hiyo vijana ni kundi kubwa. Safari hii kuna utaratibu vijana wengi wamekuwa wakienda Jeshini, ushauri wangu kwa Serikali, nilikuwa naomba katika kila Kambi ya JKT, kuwe na Chuo au Vyuo vya VETA, vijana wanapotoka hapo wapewe mikopo na nyenzo za kazi. Kwa hivi tunaweza tukasaidia kwa namna moja ama nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo naomba kuzungumzia suala la mikopo, niko na vijana bado. Masharti ya mikopo yamekuwa makubwa! Kijana leo anamaliza Chuo Kikuu anataka kujiajiri, anaambiwa ukitaka mkopo leta kiwanja, leta nyumba! Jamani, ndiyo nimemaliza chuo, nyumba naipata wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningeomba Serikali iongee na taasisi za fedha zilegeze masharti kwa vijana wanaokuwa wamemaliza Chuo, ili waweze kujiajiri. Tunaona nchi inaendeshwa kwa watu wengi ambao wamejiajiri, tuwasaidie vijana wafike kule wanakotaka kufika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ninalotaka kuzungumzia ni suala la ushuru. Mheshimiwa Rais aliahidi na aliongea kwa msisitizo mkubwa kwamba, atapunguza na kuondoa ushuru kwa wafanyabiashara wadogo wadogo. Alisema pia, ataondoa *harassment* zinazofanyika na mgambo wa Manispaa na Majiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachofanyika wote tunakijua, wafanyabiashara wadogo bado wananyanyasika, inatia uchungu. Unamkuta

mama lishe kajipangia pale anauza chakula, mgambo anakuja anamwambia kama hutaki nikufukuze nipe 1,000/=! Tangu asubuhi hiyo 1,000/= ndiyo anayoitafuta! Kwa hiyo, kaka yangu Mheshimiwa Simbachawene watu wako hawa uongee nao vizuri, bado wanaendelea kunyanyasa watu wetu na tukumbuke katika nchi yoyote kuna wafanyabiashara wakubwa kama akina Bakhresa, kuna wafanyabiashara wa kati kama akina Shabiby, lakini kuna wafanyabiashara wadogo wadogo! Sasa kwa nini wale wakubwa hawaonewi mnawaonea wadogo, si haki! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alisema kabla ya kuwafukuza wale au kuwaondoa, mwambie mama hapa hustahili kukaa, lakini eneo lako husika ni hili. Unamwambia hapa hufai kukaa, eneo la kukaa halifahamiki, hujampangia! Ni wakati wa Halmashauri za Manispaa na Wilaya ziitikie kwa vitendo hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila Halmshauri ioneshe ni wapi imetenga maeneo kwa hawa watu. Wafanyabiashara wanaishi kwa mashaka, hawana matumaini, wanatapakaa mitaani! Kwa kufanya hivyo tunazidi kumtia aibu Mheshimiwa Rais kuonekana alichokuwa anakizungumza na kuwaahidi wafanyabiashara wadogo wadogo si sahihi. Kwa hiyo, mimi naomba sana Serikali itie mkazo katika masuala haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la mwisho kabisa nataka nimalizie na suala zima la elimu. Naomba kumpongeza Mheshimiwa Rais kwamba ameweza kulitimiza kwa asilimia kubwa, elimu imekuwa bure kuanzia elimu ya msingi mpaka kidato cha nne.

Lakini pia nataka kuzungumzia kuhusu vijana wanaomaliza Chuo Kikuu kwamba kunakuwa na fursa vijana wengi huomba kwenda kusoma nje ya nchi. Lakini fursa hizi kwa uzoefu na kwa utafiti wangu Tanzania ya leo ina Vyuo Vikuu vingi, lakini vijana wengi wanaomaliza Chuo Kikuu huomba zile fursa za kutaka kusoma nje, lakini ambao hupata fursa siku zote wanachukuliwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Mzumbe! Kwa maana bado sitaki kuamini kama ile dhana ambayo ilikuwa inasema mtu akisoma Mzumbe na UDSM ndiyo anakuwa hatari kabisa. Siku hizi kuna wanafunzi ambao wana uwezo mkubwa wapo UDOM, wapo Tumaini, wapo katika kila chuo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba vigezo mnavyovitumia kuwachukua hawa vijana kuwapa nafasi za kusoma nje ya nchi, zifike katika kila chuo, zisiende UDSM na Mzumbe peke yake, tuwape vijana wote haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema machache hayo naomba kushukuru sana, ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Deo Francis Ngalawa, atafuatiwa na Mheshimiwa William Mganga Ngeleja.

MHE. DEO F. NGALAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kukupongeza kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Bunge lako Tukufu. Naitwa Deo Ngalawa, Mbunge wa Ludewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nipende kukishukuru Chama cha Mapinduzi kwa namna kilivyoiandaa Ilani yake. Ilani yake ni Ilani nzuri ambayo imetengeneza mpango mzuri wa mwelekeo wa Taifa ambako linatakiwa kwenda. Katika chaguzi zetu tuliinadi Ilani na wananchi wakatuchagua. Kwa hiyo, napenda kukipongeza chama. Hawa wanaotoka sasa ni kwa sababu hoja zao nyingi zinapwaya, hawana kitu cha kukizungumzia zaidi ya kutengeneza vijembe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napenda kujikita katika hotuba ya Mheshimiwa Rais moja kwa moja. Mheshimiwa Rais katika hotuba yake katika ukurasa wa 12 ameizungumzia reli toka Mtwara – Songea – Mbamba Bay mpaka Liganga. Mimi napenda kumshukuru kwa hilo na tulipokuwa tunaizungumzia hiyo reli ya kutoka Mtwara mpaka Liganga ni kwa maana tunazungumzia suala la makaa ya mawe - Mchuchuma na chuma – Liganga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la makaa ya mawe - Mchuchuma na chuma – Liganga limekuwa ni suala la muda mrefu. Nadhani sasa ni kipindi cha miaka 50 limekuwa likizungumziwa na halina utekelezaji wowote. Nimshukuru Waziri Profesa Muhongo, tarehe 4 na 5 alifika kwenye makaa ya mawe Mchuchuma na vilevile alifika pale chuma – Liganga; alijionea *type* ya wawekezaji ambao tunao na namna gani wanaweza wakaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nisikitike, wana wa Ludewa wana masikitiko makubwa. Wameachia ardhi yao miaka ipatayo 10, ardhi ile haitumiki, hawaitumii kwa maana yao na hakuna utaratibu wowote wa matumaini wa kulipwa fidia katika maeneo ambayo wao wameyaachia.

Sasa nipende kuliambia Bunge lako, wananchi wanataka fidia ya maeneo waliyoyaacha na kibaya zaidi hata ule mpango wa kimkakati wa huyu mwekezaji bado hauonekani!

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na Waziri Muhongo tarehe 5 Mchuchuma, pale Nkoma Ng'ombe na vilevile tulikuwa Liganga pale Mndindi; Serikali imekuwa ikiwakilishwa na *NDC* na wawekezaji ni Wachina, lakini katika majadiliano na maongezi yao wana *contradiction* kubwa. Ile miradi ni

mikubwa, kuna mamilioni ya tani za makaa ya mawe, leo nchi inazungumza kwamba haina umeme! Lakini tunaamini mradi wa makaa ya mawe Mchuchuma ukianza umeme katika Taifa hili inaweza ikawa ni historia.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme utakaozalishwa Liganga una uwezo wa ku-*supply* ndani ya nchi hii katika miaka isiyopungua 150, lakini leo Taifa bado halijachukua hatua madhubuti. Ni miaka mingi, sisi wengine toka tunasoma, kabla hatujazaliwa tunaambiwa kuna makaa ya mawe – Mchuchuma, tunaambiwa kuna chuma – Liganga! Mwekezaji aliyepo ameonesha *incompetence* kubwa mbele ya Waziri Profesa Muhongo! Hakuna maandalizi ya kutosha ya hiyo miradi kuanza!

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi nipende tu kushukuru na kumshukuru Mheshimiwa Profesa Muhongo, Waziri wa Nishati na Madini, aliwaeleza wananchi wetu ukweli kwamba Taifa tunapoamua kuingia mikataba hii iwe ni ya wazi na kusiwepo na uficho wowote.

Mimi ninaamini Waziri usingekuja Ludewa, usingekuja pale Nkoma Ng'ombe – Mchuchuma, usingekuja Liganga bado wananchi wetu wangekuwa wanaendelea tu kudanganywa danganywa na tusingejua *fate* yoyote ambayo inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nipende kuchukua fursa hii kwamba, tupate wawekezaji ambao ni *serious*. Tupate wawekezaji ambao wana uhakika, ili mwisho wa siku watu wetu tuwajengee matumaini, ili nchi iweze kwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukizungumza sana Bungeni kwa nini nchi haiendi, wakati tuna madini ya kutosha, tuna mazao ya kutosha, lakini hatuchukui hatua. Huyu mwekezaji amekuwa akikumbatiwa! Haoneshi dalili yoyote ya namna gani tunaweza kwenda! Fidia hataki kulipa, anaulizwa kama hizo hela anazo anasema hela hana anasubiri kukopa nje ya nchi! *What type of* mwekezaji *is?* Sasa *investor* wa namna hii kweli tunakaa na kumkumbatia namna hii? Mimi nadhani siyo sawa! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Ludewa wanaisubiria Liganga ianze mara moja kwa sababu, imeshakuwa ni hadithi za muda mrefu. Liganga aanze, Mchuchuma aanze, tuachane na hii biashara kwamba hatuna umeme, hatuna umeme, hatuna umeme! Hii inatakiwa kubaki kuwa ni historia. Lakini mimi ninamuamini Waziri Muhongo atalishughulikia hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna barabara ya Itoni – Njombe kuelekea Manda; barabara hii Mheshimiwa Rais ameahidi kwamba iwekwe lami, lakini nashukuru *TANROADS* juzi imetangaza kipande cha kilometa 50

kutoka Lusitu kuelekea Mawengi kwamba kitawekwa lami. Kwa hiyo, tunaomba hili lizingatiwe na lifanyiwe kazi haraka vya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tuna barabara kutoka Mkiu kwenda Madaba na yenyewe Mheshimiwa Rais ameizungumzia kwa kiwango cha lami. Tunaomba lami hiyo iwekwe na wananchi wana matumaini, wana mazao yao mashambani, ila usafiri umekuwa ni shida, pindi hizi lami zikiwa tayari naamini kabisa mazao yatafika kwenye maeneo ya masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tuna suala la miundombinu ya mawasiliano ya simu. Leo hii Tarafa nzima ya Mwambao, Ukisi kule Ziwa Nyasa tunapakana na Malawi, vijiji 15 havina mawasiliano ya simu kabisa! Sasa sijajua Serikali inajipangaje na inawaonaje hawa watu? Hawa watu wako mpakani! Huku tunapakana na Kyela na Dkt. Mwakyembe! Huku tunapakana na Nyasa na *Engineer* Manyanya! Hapa katikati pamekuwa hamna mawasiliano ya aina yoyote! Wananchi wale wameniambia wataanza wao kutafuta hayo mawasiliano. Hatuna mawasiliano ya barabara, hatuna mawasiliano ya simu! Kwenye upande wa barabara wanasema wao wataanza na jembe la mkono. Na ninaiomba Serikali sasa ituunge mkono, ili tuweze kuviunganisha hivi vijiji na waonekane na wao wapo ni sehemu ya nchi hii ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukiahidiwa muda mrefu juu ya daraja la Mto Ruhuhu unaounganisha Wilaya ya Ludewa na Wilaya ya Nyasa. Wananchi wanapata shida na kivuko kile na kivuko kimekuwa hakifanyi kazi. Dada yangu Injinia Manyanya unalifahamu hilo. Tunaomba Serikali ilichukue hilo na lifanyie kazi, ili mwisho wa siku tuweze kwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mambo mengi sisi wana wa Ludewa. Mheshimiwa Rais alipokuja Ludewa alitoa ahadi ya kipande kidogo cha lami cha kilometa 25 kutoka Ludewa mpaka Lupingu. Kwa hiyo, tungeomba ahadi hizo zitekelezwe.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa, muda wako umeisha!

MHE. DEO F. NGALAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MHE. WILLIAM M. NGELEJA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu muweza wa yote kwa yale aliyotujalia.

Pili, nikupongeze wewe Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nakuomba unifikishie salamu za pongezi kwa Mheshimiwa Spika pamoja na Wenyeviti ambao tumewachagua hivi karibuni kwa kazi kubwa mnayoifanya ya

kutuongoza. Naungana na Wabunge wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake ambayo kwa kweli, mimi nailinganisha na tangazo la vita, kwa namna ambavyo ilipangiliwa, lakini kwa namna ambavyo imetoa taswira ya kero za Watanzania na mikakati iliyopo ya namna ya kuzitatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wachangiaji wenzangu wamesema mengi, lakini kama ninavyosema hili ni tangazo la vita kuhusu maadui zetu wale ambao walianza kutajwa tangu enzi za Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, ujinga, umasikini, maradhi, lakini sasa yakaongezeka pia ufisadi, rushwa, uzembe na mambo ambayo yanakwaza maendeleo yetu, sina budi na mimi kupita katika baadhi ya maeneo ambayo Mheshimiwa Rais katika hotuba yake ya kurasa 36 aliyoyataja.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ni kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza sana kwa dhamira yake aliyoionesha na tayari ameshaanza kutenda kwa matendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hili ni tangazo la vita kwa sababu Mheshimiwa Rais baada ya hotuba yake na hata kabla hajaunda Baraza la Mawaziri na kwa nafasi hii pia nawapongeza sana wateule Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri pamoja na watendaji wengine ambao wameteuliwa kumsaidia Mheshimiwa Rais; tayari Mheshimiwa Rais aliingia vitani, alishaanza kufanya kazi na akaanza kutumbua majipu kwa lugha ambayo imezoeleka sasa kwa Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunampongeza sana, lakini kubwa tunazungumzia uwezeshaji wa huduma kwa Watanzania ambao sisi ni mojawapo ya wadau wakubwa sana katika kuwezesha hilo. Lakini tunapozungumzia kuimarisha huduma za Watanzania tunazungumzia uwezo wa makusanyo ya Serikali na matumizi mazuri ya fedha inayopatikana kutoka kwenye makusanyo yanayofanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo kubwa ambalo Mheshimiwa Rais amelifanya na sisi Watanzania wote, tukiwemo sisi Wabunge, ni dhahiri na jambo la msingi kumuunga mkono na kumpongeza ni hili la kuongeza mapato. Kwa muda mfupi tu ambao amekuwepo Ikulu, kama Kiongozi wetu Mkuu wa Taifa, Mheshimiwa Rais amefanikisha kuongeza mapato ya Serikali yanayokusanywa kwa mwezi kwa kiwango ambacho kimetangaziwa Watanzania, kwa mwezi uliopita tuliambiwa makusanyo yalikuwa shilingi trilioni 1.4! Si jambo dogo!

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni kwamba kwa mwendo huu dira ambayo inaonekana sasa, tunajenga uwezo wenyewe wa Taifa kwenda

kusimamia kwa kiwango kikubwa sana kuwezesha utekelezaji wa huduma mbalimbali na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais pamoja na mambo mengine, ametuambia na Watanzania tunakiri kwa matendo anayoyafanya kwamba, anataka kuiona Tanzania ya Viwanda katika kipindi chake cha utumishi wa takribani miaka 10 ijayo, tunaamini itakuwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia viwanda tunazungumzia mambo mengi, lakini mimi hapa ni mwakilishi wa Jimbo la Sengerema ambako ninawashukuru sana wananchi hawa walionituma, nikiunganisha nguvu na wawakilishi wa Majimbo mengine kutoka maeneo mbalimbali ya Tanzania, tunapozungumzia viwanda kwa vyovyote vile tutashuka chini kuzungumzia viwanda vinavyotuhusu katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuungana na wenzangu ambao wamekuwa wakizungumzia umuhimu wa kuwa na viwanda katika Taifa letu na kwa Kanda ya Ziwa na hasa Mkoani Mwanza, Jimbo la Sengerema, viwanda ambavyo navizungumzia hapa ni vile ambavyo Mheshimiwa Rais amekuwa akisisitiza sana, viwanda vya pamba. Nazungumza hapa nikiwa namuona Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, lakini nawaona pia, baadhi ya Mawaziri ambao wanahusika na mambo ambayo yanabeba uchumi wa Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nijielekeze zaidi kwenye maeneo haya, zao la pamba. Ninafahamu, Mheshimiwa Rais kwenye kampeni zake amelisisitiza sana, kufufua viwanda vya kuchambua pamba, lakini na viwanda vingine ambavyo vinategemea mazao ambayo tunayalima katika Kanda ile. Sisisitizi hili katika mtazamo wa Kikanda, nazungumzia yale ambayo wananchi wa Jimbo la Sengerema na Mkoa wa Mwanza na Kanda ya Ziwa wanatarajia kuyaona yaki-*reflect* ile dhamira ya Mheshimiwa Rais katika kujenga uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili katika eneo la viwanda, si pamba tu! La pili, ni hasa mazao ambayo yanatokana na samaki, mazao yanayotokana na mifugo na mazao yanayotokana na kilimo kwa ujumla. Katika hili, naungana na Mheshimiwa Rais, juzi alipokuwa Arusha alisema na mimi nawaomba Waheshimiwa Wabunge eneo hili tumsaidie sana Mheshimiwa Rais pengine kwa kutolea maelekezo au kupitia Azimio kwa kadri itakavyokuwa ama kupitia taratibu za Kamati zetu mbalimbali za Bunge, hili la kulishirikisha Jeshi la Wananchi wa Tanzania katika kuendesha na kusimamia baadhi ya viwanda ambavyo tunaviona vinaweza kutumia rasilimali ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili siyo la kuachia lipite hivi hivi, kwa sababu tunaliweza, tunaweza kulifanya, malighafi iliyopo hapa hapa nchini, nikadhani kwamba ni jambo la msingi Bunge lako Tukufu tujipange tuone namna ambavyo tunaweza kum-*support* Mheshimiwa Rais kutekeleza hiyo azma ya kuweza kuwa na viwanda ambavyo Wanajeshi kwa ujumla wao wanashiriki katika kusukuma hili eneo la viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo napenda kuzungumzia linahusu sekta ya afya. Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, pale Sengerema tuna hospitali ya *mission* ambayo imepewa hadhi ya kuwa hospitali ya Wilaya, na kwa utaratibu wa sera ya afya hiyo hospitali ina hadhi ya Hospitali ya Rufaa ya Kimkoa. Hospitali ile tumekuwa na matatizo ya muda mrefu, nimeyazungumzia sana, lakini kikubwa ambacho ninakizungumzia sasa hivi ni kwamba, ruzuku inayopatikana kwenye hospitali ile haitoshelezi na miaka kadhaa tumekuwa tukiomba na hatujafanikiwa sana katika ombi letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahesabu ya ruzuku yanatokana na vitanda 150 vilivyokuwa vinatajwa kipindi kile wakati Mkataba wa Serikali na wa-*missionary* wenye hospitali hii ulivyofungwa, leo hii ina vitanda zaidi ya 300. Ninachoomba Mheshimiwa Waziri wa Afya, ombi letu liko Wizarani pale, ninakuomba sana ombi letu ulizingatie la kuongezewa ruzuku kutokana na vitanda ambavyo viko pale vinavyohudumia wananchi wa Jimbo na Kanda ile ya Sengerema.

Mheshimiwa Simbachawene, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais inayoshughulika na masuala ya TAMISEMI, Mji wa Sengerema mnaufahamu Jimbo la Sengerema, Wilaya ya Sengerema mnaifahamu, Mji wa Sengerema una hadhi ya Mji Mdogo, lakini kwa miaka minne iliyopita tulileta ombi letu na tulikidhi vigezo wa kuubadili ule mji ufikie Halmashauri ya Mji. Nafahamu Serikali imekuwa ikishughulikia jambo hili, nina wajibu wa kukumbushia hili kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Sengerema, kwamba tunamba ombi letu la kufanya Mamlaka Mji Mdogo wa Sengerema ifikie hadhi ya kuwa Halmashauri ya Mji.

Mheshimiwa Simbachawene kuna lingine tuliongea na wewe la madawati, ombi langu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Sengerema, sisi tulikuwa na Kikao cha *RCC* kule Mkoani, tumezungumza tukasema Wakuu wa Mkoa na Wakuu wa Wilaya wamepewa malengo na Serikali ya kuhakikisha kwamba kila shule ya msingi na sekondari, inakuwa na madawati ya kutosha. Sasa sisi Wilaya ya Sengerema tumebahatika kuwa na msitu wa Serikali shamba la miti linafahamika liko Jimbo la Buchosa na kwa sababu Wakuu wa Wilaya na Mkoa wamepewa mamlaka ya kuomba ridhaa ama kupata vibali kutoka Mkoani, nilikuwa naomba sana tusaidiane pamoja na Mheshimiwa Profesa Maghembe tupate hivyo vibali, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza aelezwe na Wakuu wa Wilaya ili sisi tutengeneze madawati kwa ajili ya kusaidia vijana wetu

wanaosoma katika shule za sekondari na sule za msingi kwa Wilaya na Mkoa wa Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Bunge hili linahitaji kutengeza *action plan*, namna ya kumsaidia Mheshimiwa Rais kuitekeleza hotuba hii ina mambo mengi. Sisemi hili kwa maana ya kwamba hatuiamini Serikali yetu, lakini sisi kama wadau muhimu katika kusukuma gurudumu la maendeleo, na naamini unalifahamu na mkakati naamini wa Kamati ya Uongozi upo, sisi ni muhimu sana tutengeneze *action plan* kwa masuala yanayozungumziwa hapa tuone ni namna gani tunajipanga kumsaidia Mheshimiwa Rais na moja ni hili ambalo tumeshalifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Kamati ya Sheria Ndogo imeundwa ni Kamati mpya, mimi ni mmojawapo ya Wajumbe katika Kamati hiyo, ninaamini kwamba tutakuwa na jukumu la kupitia sheria zote ambazo ni kero kwa wananchi na hasa zinawezesha kutoa ushuru ambao ni kero kwa wananchi katika Halmashauri zote za nchi yetu. Lakini tukishakuwa na *action plan* katika Bunge hili tutaisaidia sana Serikali kuikumbusha kutekeleza yale ambayo yamesemwa katika hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nashukuru sana, nakupongeza sana, naungana na wenzangu kwa mara nyingine tena kuunga mkono hoja, kuunga hotuba hii nzuri ambayo ni tangazo la vita kwa ajili ya kuondoa na kupunguza umasikini wa Taifa letu. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante, Waheshimiwa Wabunge, muda tuliobaki nao ni mdogo sana, nitawataja Wabunge wafuatao ambao watachangia lakini naomba kwa kadri inavyowezekana watumie muda mfupi kuliko dakika kumi, tafadhali. Mheshimiwa Hawa Ghasia ataanza, Mheshimiwa Amina Mollel, atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Michael, Mheshimiwa Stanslaus Mabula, Mheshimiwa Emmanuel Kasaka, mwisho atakuwa Mheshimiwa Neema Mgaya. Mheshimiwa Hawa Ghasia, tafadhali!

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, na nimshukuru Mwenyenzi mungu ambaye ameniwezesha afya njema na kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu bila kuwasahau wananchi wa Mtwara Vijijini ambao wameniwezesha kurudi kwa mara ya tatu katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa katika Bunge hili ambayo kwa kweli imegusa katika kila suala. Mimi kwa kifupi kama ambavyo umeshauri, ningependa nizungumzie maeneo machache.

Eneo la kwanza ningependa kuzungumzia suala la viwanda, ambalo Mheshimiwa Rais amesisitiza wakati wote kwamba Serikali yake itakuwa ni Serikali ya viwanda. Naunga mkona sana suala hilo, na napendekeza suala la wapi viwanda vijengwe, tuangalie vigezo vya kiuchumi zaidi. Mwenyenzi Mungu ameiumba nchi yetu kila eneo lipo zao au ipo rasilimali au malighafi ambazo amewajalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na Mkoa wangu ambao Mwenyenzi Mungu ameujalia gesi nyingi, ameujalia zao la korosho, bila kusahau bandari ambayo ni ya asili yenye kina kirefu. Kwa hiyo, naunga mkono Wizara ya Fedha na Uchumi ambayo kupitia Mpango wa Taifa wa miaka miwili, mapendekezo waliyoyatoa miaka mitano ijayo ambayo wamependekeza kuendeleza maeneo ya viwanda eneo la Mtwara likiwa ni mojawapo. Ningependekeza na ningeishauri Serikali kwamba suala la uendelezaji wa viwanda liende sambamba na uendelezaji wa miundombinu ambayo itawezesha viwanda vile kufanya kazi kwa ufanisi, ikiwemo reli ya kutoka Mtwara hadi Songea kwenda Liganga na Mchuchuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, reli ile itawezesha sana kubeba malighafi kutoka Liganga na Mchuchuma kuja Mtwara na vilevile kusafirisha bidhaa ambazo zitazalishwa katika viwanda ambavyo vitakuwepo kule Mtwara. Mtwara imejaliwa gesi na sasa hivi bomba la gesi limejengwa hadi Dar es salaam, lakini bei ya gesi ni sawa Mtwara na Dar es Salaam. Wakati ukiangalia bei ya mafuta ni tofauti, Dar es Salaam tofauti na Mtwara, tofauti na Kigoma na tofauti na eneo lingine. Kwa kuweka bei ya gesi sawa Mtwara na Dar es Salaam au Mikoa mingine ndiyo kusema unataka kuua uwekezaji wa Mkoa wa Mtwara. Kwa sababu hakutakuwa na motisha yeyote mtu kwenda kuweka kiwanda Mtwara wakati bei ya gesi popote anapohitaji ataipata kwa bei ile ile. Kwa hiyo, nimuombe Waziri wa Nishati aliangalie suala hilo la bei ya gesi.

Mheshimiwa Naibu Waziri, suala lingine ambalo nataka pia nilizungumzie ni suala zima la uendelezaji wa bandari ya Mtwara na uwanja wa ndege wa Mtwara. Uchimbaji mkubwa wa gesi unafanyika baharini na wafanyakazi wanapelekwa kule kwa helkopta na kurudishwa kwa helkopta na wakati mwingine kama ilivyo katika eneo lolote la kazi wakati mwingine zinatokea ajali kule. Sasa ikitokea usiku ni suala gumu sana kuwaleta wale majeruhi huku nchi kavu kwa sababu uwanja wa ndege wa Mtwara hauna taa. Ukiachia taa ule uwanja ulijengwa mwaka1965, hata mzungumzaji nikiwa sijazaliwa, lakini mpaka sasa hivi tunavyozungumza hakuna ukarabati wa maana uliyofanyika katika uwanja ule, kwa hiyo, niombe Serikali iufanyie ukarabati uwanja ule uendane na uwekezaji ambao uko kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia suala zima la viwanda vya korosho na suala zima la ukamilishaji wa hospitali ya Rufaa katika Mkoa ule. Pia suala la maji, viwanda vyote vinahitaji maji, wananchi wanahitaji maji, lakini shughuli za binadamu nyingi zinahitaji maji. Ningependa kurudia tena kwamba suala la uwekezaji wa viwanda uende sambamba na uwekezaji wa miundombinu ambayo inabeba au inawezesha viwanda vile kufanya kazi ikiwemo umeme, barabara, reli, bandari, hospitali kwa sababu wafanyakazi pia wanahitaji kuwa na afya ili waweze kutumika vyema.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hotuba ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

MHE. AMINA S. MOLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia mawili matatu katika hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa John Joseph Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kunijalia afya njema lakini pia familia yangu, pamoja na wote wa UWT walioniwezesha kufika hapa.

Baada ya kusema hayo naomba nianze kwa kuchangia kwanza kabisa kwa kumpongeza Rais, kwa kuteuliwa kwake, lakini nimpongeze sana kwa kazi nzuri aliyoifanya kwa sababu katika kipindi cha miezi mitatu siku 100 ndizo hizo ambazo hivi sasa zinaelekea kutimia, tumeona mengi ambayo ameweza kuyafanya kwa kipindi kufupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kubwa kabisa kwa niaba ya watu wenye ulemavu kwa kweli nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jitihada za kutambua kundi hili kuliwezesha katika sekta mbalimbali. Tumeshuhudia kwa mara ya kwanza katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunaye mwakilishi na vilevile masuala ya watu wenye ulemavu kuyahamishia katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Hiki kilikuwa ni kilio cha watu wenye ulemavu kwa kweli tunamshukuru sana kwa hili. Vilevile tunamshukuru sana kwa kutupa Mawaziri hawa na nina imani kabisa kama waswahili asemavyo uchungu wa mwana aujuae mzazi, ninaamini kabisa Mheshimiwa Jenista Mhagama atakuwa msaada mkubwa kwa kweli, kwetu sisi katika kundi hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kwa moja nianze kuchangia baada ya shukrani hizi kwa sababu ningekuwa mchoyo wa fadhila. Mheshimiwa Rais katika hotuba yake aligusia masuala ya watu wenye ulemavu na kama nilivyosema awali ameanza kuonyesha kwa vitendo. Tunafahamu tunapozungumzia umasikini katika nchi hii watu wenye ulemavu ndilo kundi

linaloongoza kwa umaskini, na hata unapokutana na watoto wenye ulemavu wengi wao pia wametoka katika familia maskini. Kwa hiyo, suala la elimu ni muhimu sana, kwa kundi hili, ukimuwezesha kupata elimu kwanza mtu huyu anaweza kujitegemea yeye mwenyewe, lakini pia hata unapomwezesha katika nyenzo mbalimbali inakuwa ni msaada mkubwa kwake yeye ili kuweza kujitafutia riziki kwake yeye, lakini pia katika familia yake kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa nchini Tanzania ni 4% tu ya watoto wenye ulemavu ndiyo wanaopata elimu, na tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwamba amefanya elimu kuwa bure, tunaamini kabisa mojawapo ya vikwazo ambavyo wazazi wengi walikuwa wanaona taabu kuwapeleka watoto wao shule, kama ana watoto wawili mwenye ulemavu na asiye na ulemavu anaona ni afadhali ampeleke asiye na ulemavu na huyo mwenye ulemavu abaki nyumbani. Kwa hiyo tunaamini kabisa kwamba hivi sasa wazazi wengi watawapeleka watoto wao shule ili waweze kupata elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naiomba Serikali ichukue hatua kali, sheria ifuate mkondo kwa wale wazazi ambao mpaka hivi sasa bado wanawaficha watoto wenye ulemavu nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii mzazi wangu angenificha mimi tusingekuwa na Amina hapa Bungeni, tusingekuwa na akina Mheshimiwa Ikupa, tusingekuwa na Waheshimiwa wengine wote kama wazazi wetu wangetuficha. Lakini walitambua thamani ya sisi ndiyo maana leo hii tuko hapa. Kwa hivyo, ninaamini kabisa kukiwepo na sheria ambayo itawabana wazazi wote wanaowaficha watoto wao majumbani na kuwakosesha haki yao ya msingi ya kupata elimu ninaamini kabisa watoto hawa wataweza kufika mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala hili la elimu, hivi sasa elimu katika shule za msingi na sekondari ni bure, lakini tunafahamu kwamba wanafunzi wanaokwenda Vyuo Vikuu kuna mikopo. Hivi kuna utaratibu gani mzuri ambao unaandaliwa kwa wanafunzi hao wenye ulemavu ili waweze kupata elimu? Kwa sababu wengine hawapati hizo asilimia za mikopo. Kwa hiyo, niishauri Serikali yangu na ninaamini kabisa mwanzo mzuri tumekwisha uona, ianze kutoa ruzuku kwa wanafunzi wenye ulemavu, wanaokwenda Vyuo Vikuu, sekondari na hata *form five* na *six*, ili basi waweze kujikimu, lakini pia ule mzingo ambao wengine ni walemavu na familia zao ni masikini zaidi wataweza kwenda shule. Ombi langu ni hilo kwa Serikali.

Mheshimwia Naibu Spika, lakini pia mimi ni mwanataaluma, nimetoka katika taaluma ya habari. Hawa waandishi huko wanakotoka wengi wao mishahara yao ni midogo na mimi nimuombe sana kaka yangu Mheshimiwa Nape, nakuomba sana kuhakikisha kwamba waajiri wengi kunakuwepo na utaratibu mzuri ambao utawawezesha Waandishi wa Habari waweze kuifurahia

kazi yao. Wananchi wanafaidika kwa sababu ya hawa Waandishi wa Habari. Tukiwa katika misafara, wakiwa katika shughuli zozote za kitaifa muda wote wako *busy* kufanya kazi zao, lakini waajiri wengi hawatambui thamani ya Waandishi wa Habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ombi kwa Serikali, tuwaangalie sasa ili waandishi hawa waweze kufurahia taaluma yao, waweze kuifanya kazi yao ipasavyo kwa kuboresha maslahi yao, lakini vilevile kwa sababu wanakumbana na changamoto nyingi wanapofanya kazi, tuangalie utaratibu pia wa kuwaandalia bima, kwa sababu waandishi wengi na hata katika matukio mengi wao ndiyo wanaokuwa waathirika wa kwanza. Kukiwa na matukio ya milipuko mabomu, tukio lolote lile wao ndiyo wa kwanza kwa sababu mwajiri ili aweze kupata taarifa lazima huyu mwandishi awepo pale.

Kwa hiyo, kaka yangu Mheshimiwa Nape, ninakuomba sana uangalie ni kwa jinsi gani tutaweza kuboresha maisha mazuri kwa hawa Waandishi wa Habari.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Molel muda umekwisha.

MHE. AMINA S. MOLEL: Mheshimiwa Naibu Spika ahsante, naunga mkono hoja

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Esther Michael!

MHE. ESTHER M. MMASI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii, awali ya yote ninamshukuru Mwenyenzi Mungu kwa nafasi hii aliyonipatia na pia wananchi wangu kutoka Kilimanjaro akina mama wale kwa upendo wao ninawashukuru sana, niombi langu kwa Mwenyenzi Mungu aweze kuniongoza kwa hekima za Kimungu niweze kuutumikia utumishi wangu huu kwa moyo wa uadilifu, kwa moyo wa kujitoa na kujituma, nitamsihi sana Mwenyenzi Mungu anisimamie katika utumishi wangu huu mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada yakusema hayo, nimesimama mbele yako kumpongeza Mheshimiwa wetu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, kwa hotuba yake nzuri. Hotuba yake ilivaa kiatu cha Mtanzania mwenye kipato cha hali ya chini, kiatu chake kilivaa kila aina ya mtu ambaye alikuwa na uhitaji na imani yake katika Serikali yetu hii ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanza tu kuchangia moja kwa moja katika hotuba hii mimi nitapenda kujikita kwenye mambo mawili kama siyo matatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikaanza na kwenye suala la ajira, ni kweli kwenye ukurasa ule wa 15, Mheshimiwa Rais alianza kuonyesha kwamba na alikiri pale kwamba ni kweli Tanzania suala la ajira bado ni changamoto kubwa na ukiangalia takwimu zinasema ingawa uchumi umekuwa kwa asilimia 7.1 lakini asilimia 28 ya Watanzania bado ni maskini. Lakini katika kutatua changamoto hii Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli alielekeza hisia zake na alielekeza weledi wake kwa kusema kwamba njia mojawapo ya kujitoa kwenye umaskini ni pamoja na kuwa na viwanda na akasema pale tukiwa na uchumi unaotegemea viwanda pengine tutazalisha ajira za asilimia kama 40 hivi. Sasa katika hili mimi nitapenda kuchangia changamoto ambazo tuko nazo na ndiyo imekuwa kama ajenda ya dunia lakini pia imekuwa ni ajenda ya Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanza na suala la ajira. Katika suala hili la viwanda Mheshimiwa Dkt. Joseph Pombe Magufuli, alianza kwa kuonyesha kwamba ni vema sana uchumi wa Tanzania ukalenga ule ubepari wa Kitaifa na tukatoka kwenye ubepari mamboleo. Ubepari mamboleo ni uchumi ule unaokuzwa au unaojengwa kwa uchuuzi, yaani hautumii malighafi ya ndani wewe unaagiza malighafi kutoka nje unalisha viwanda vya ndani, na kwa kufanya hivi kutoka kwenye ubepari mamboleo kwenda kwenye ubepari wa Kitaifa ndiyo njia pekee ya kujenga uchumi wa Tanzania na uchumi wa viwanda ulioimarika na kasema kwamba pamoja na viwanda hivi aliweka umuhimu wa kukuza sekta ya uvuvi, kilimo na ufugaji na katika hotuba yake pia alipokuwa anaongea na wafanyabiashara alionyeshwa kusikitika kwake na akasema inasikitisha sana kuona Tanzania ndiyo nchi pekee yenye mifugo mingi ikianza na Ethiopia Tanzania ikiwa ya pili lakini hatuna viwanda vya samli, hatuna viwanda vya ngozi, leo hii hatuna viwanda vya uvuvi alionyeshwa kusikitishwa.

Sasa katika mchango wangu katika sekta hizi tatu ni upi? Mimi nitapenda kusema kwamba ukianza na suala zima la kilimo ni kwamba ifike sasa Serikali yetu iweze kutambua changamoto kubwa ambazo tuko nazo.

Moja, ikiwa ni vikwazo vya kisheria, ukiangalia hasa sheria hii ya Vyama vya Ushirika, mathalani mimi ninayetoka Kilimanjaro, leo siwezi kulima kahawa na nikawa na *direct control* na ile kahawa. Watu wengi walikuwa *discourage* waka-*prone* zile kahawa ambalo ni zao kuu la uchumi na tunajua kabisa mchango wa zao kuu kama hili. Kwa hiyo, hii inakatisha tamaa, ifike sasa tutoke kwenye sheria kandamizi, sheria za kikoloni ambazo haziwezi kumsaidia Mtanzania wa leo. *(Makofi)*

Lakini pia katika suala zima la ajira, mimi ninafikiri ifike sasa Tanzania ichukue hatua madhubuti, mimi niliangalia juzi bajeti ya Kenya ya mwaka 2014/2015 ni bajeti ya juzi tu, niliona pale wenzetu walivyojidhatiti katika suala la

ajira, kuna mfuko pale wa vijana, lakini mfuko huu kwa Tanzania yetu ya leo mfuko huu umefichwa katika Baraza la Taifa la Uwekezaji. Mimi ninashauri, kwa ombi ninaomba sana Wizara husika iweze kutoa mfuko ule pale ulipo, uwe ni mfuko wa kujitegemea vijana wetu waweze kupata ajira kupitia mfuko ule. Kwa nchi ya Kenya waliweza kutenga shilingi trilioni 8.1 sawa na pesa za Kitanzania shilingi bilioni 32.4, kwa pesa za Kitanzania hizi ni hatua madhubuti katika kumsaidia Mtanzania.

Lakini pili, nikija haswa kwenye suala la hili la ajira nafikiri sasa ifike muda ofisi husika au Wizara husika iweze kutumia tafiti zinazofanyika Tanzania. Mathalani, katika taasisi za umma kuna *convocation office* kule wanafanya *tracer studies* nyingi na kuonyesha na kubaini kijana huyu anayemaliza leo kesho atakuwa wapi na anafanya nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Wizara husika ni kwamba tafiti ziingizwe kwenye matumizi, *donors* wengi wanatoa pesa nyingi ziende kwenye tafiti lakini haziingizwi kwenye matumizi.

Mathalani tunaenda kwenye uchumi wa viwanda tusipojikita kwa kuangalia suala la *research and development* siamini kama tutafika. Juzi watu wengi walikuwa wanajiuliza hapa tutalindaje viwanda vyetu, jibu ni kwamba tutahitaji kutupa jicho letu kwenye upande wa pili, suala la *research and development* tulipe uzito wa hali ya juu. Walimu wanakesha maofisini wanafanya tafiti, lakini tafiti zile zimebaki kuwa kwenye makabati. Ninaomba ofisi husika iweze kutoa uzito wa pekee kwenye suala *research and development*, tukifanya hivi tutalinda uchumi wetu wa Tanzania, tutalinda viwanda vyetu vya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye suala la elimu, ninashukuru Mheshimiwa Rais alionyesha umuhimu kwamba elimu iwe bure, lakini changamoto nikianza pale mimi nilipopita mathalani Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, nimefanya *research* nimetembea na *data* nitakazozitoa ni *data* ambazo nimezitoa *field,* ninaongea kwa masikitiko makubwa, ninaongea nikiumia na nimeguswa sana. Mathalani Chuo Kikuu cha Dar es Salaam chuo kikubwa kama kile hakina *hostel* kwa wanafunzi, wanafunzi wanauwawa, wanafunzi wanapigwa risasi, mwaka jana tarehe 15 Desemba kijana mwaka wa nne wa *CoET* alipigwa risasi akiwa anasoma *Yombo five,* lakini pia mwaka 2013, ninakumbuka ilikuwa tarehe 23 Aprili, kijana Henry Chuo cha Uhasibu Arusha alipigwa risasi akiwa anasoma, akiwa anatoka bwenini…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Michael muda wako umekwisha. Mheshimiwa Stanslaus Mabula, hayupo? Haya kama hayupo…

MBUNGE FULANI: Yupo.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kulikuwa na itilafu ya mitambo kidogo, naitwa Stanslaus Mabula, Mbunge wa Jimbo la Nyamagana. *(Makofi/Vigelele)*

MBUNGE FULANI: Kiboko ya Wenje hii.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye ametupa fursa ya kuwepo hapa ndani, lakini nitumie nafasi hii pia kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Nyamagana kwa kufanya maamuzi sahihi kuwakataa watalii na kuleta wachapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maandiko matakatifu Hosea 4:6 inasema watu wangu wanaangamia kwa kukosa maarifa. Kwa hiyo, nataka nikuthibitishie maandiko haya yako watu yanawahusu moja kwa moja. Kwa hiyo, tuliobaki humu tusiwe na shaka kwa sababu sisi tuna maarifa, tunayo kazi ya kulitumika Taifa na Watanzania. Mara zote nimekuwa ninasema tumeanza na Mungu, tutamaliza na Mungu na ndivyo itakavyokuwa. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Kweli kabisa.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuchangia kwanza nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake iliyokuwa imejaa na kusheheni mahitaji ya Watanzania. Watanzania wengi wakati wote tumekuwa na subira lakini tumekaa tayari kutegemea hiki ambacho Mheshimiwa Rais sasa anakifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda moja kwa moja kwenye kuchangia hotuba hii yako masuala ya msingi ya kuzungumza juu ya Jimbo langu la Nyamagana lakini juu ya Taifa zima kwa ujumla. Nianze na sekta ya afya. Mheshimiwa Rais amezungumza sana juu ya kuanzisha zahanati kwenye kila kijiji, kituo cha afya kwenye kila Kata, lakini kuhakikisha kila Wilaya ina hospitali na Mkoa una hospitali ya rufaa na Kanda zinazo hospitali za rufaa kwa ajili ya kuhudumia Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo ninalotoka mimi la Nyamagana linazo hospitali 12 peke yake kwa maana ya zahanati, lakini siyo Nyamagana tu, ninaamini yako maeneo mengi sana. Kihalisia tunapozungumza kumhudumia mwananchi kwenye sekta ya afya, kuanzia ngazi ya Kijiji, ngazi ya Kata na ngazi

ya Wilaya, tunapozungumza kuanzisha hospitali hizi ili zikamilike hospitali yako mambo mengi yanayohitajika, unazungumzia habari ya majengo, watumishi wenye nia njema na thabiti ya kuwatumikia Watanzania, unazungumzia vifaa tiba zikiwemo dawa ili kuhakikisha vyombo hivi na nyumba hizi zinapokuwa tayari Watanzania wenye matumaini na Serikali hii waweze kupata mahitaji yao, tukiamini afya ni suala msingi ambalo linaweza kuwa ni chombo peke yake kwa mwanadamu kinachomfanya awe na uhakika wa kupumua wakati anapopata matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini Nyamagana inabeba Hospitali ya Rufaa ya Bugando, hospitali hii ni kimbilio la wakazi zaidi ya milioni 14 wa Kanda ya Ziwa, lakini iko *based* kwenye Jimbo la Nyamagana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watumishi wanalalamikiwa sana, lakini inawezekana watumishi wanalalamikiwa sana sisi kama Serikali hatujafanya wajibu wetu. Niiombe Serikali ya Awamu ya Tano hospitali yenye vitanda zaidi ya 950 inayotegemewa na watu zaidi ya milioni 14 inaomba bajeti ya takribani bilioni saba kwa mwaka mpaka leo tuko zaidi ya miezi sita imepata milioni 106 peke yake, wananchi wataendelea kulalamika, watumishi wataonekana hawana maana kwa sababu hawatoi huduma zilizobora. Bili ya maji peke yake na umeme kwa mwezi ni zaidi ya milioni 60. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuombe sana tuangalie masuala haya kimsingi ili tuweze kutoa huduma. Nyamagana ni Jimbo peke yake lenye kilomita za mraba 256 kilomita 71 zikiwa ni maji lakini hatuna maji ya uhakika ya bomba kwa wananchi wa Jimbo la Nyamagana. Hili ni tatizo na lazima liangaliwe kwa undani. Liko suala la elimu limeshazungumza sana na mimi naunga mkono na wale waliolizungumza. *(Makofi)*

Suala la miundombinu pia limezungumzwa ziko barabara ambazo hazipitiki, Nyamagana Mheshimiwa Rais wakati amepita ameahidi kuimarisha barabara zinazosimamiwa na *TANROAD* na zile ambazo alifikiri kwa ahadi yake zitatekelezeka, kutoka Buhongwa kupitia Lwanima, Kata ya Sahwa, Kishiri kuunganisha na Igoma, Fumagira kuunganisha na Wilaya za Misungwi na Magu. Lakini kutoka Nyakato kupita Busweru kwenda Kabusungu, kwenda kutokea Bugombe, Igombe na kuunganisha na Kata nyingine, hii barabara ili iweze kupitika kwa mama yangu Mheshimiwa Angelina kwa sababu haya ni majibu pacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la miundombinu naomba niseme kwamba liko tatizo kubwa, Serikali hii imejipambanua kukusanya mapato ni lazima tuhakikishe tunapata vyanzo vya mapato. Mwanza ni kituo kikubwa ambacho kinaunganisha mikoa ya Kanda ya Ziwa, nchi za Afrika Mashariki na Kati na Maziwa Makuu hakina *airport* ya maana ambayo inaweza kuongeza

mapato kwa asilimia kubwa. Tuone umuhimu wa kujenga *airport* ya maana, *Internation Airport* ambayo itasaidia mtalii anayekwenda Ngorongoro kutokea Arusha akipita kule atokee Serengeti aje aondokee Mwanza, akishukukia Mwanza apite Serengeti aende Ngorongoro aondokee Arusha. Lakini bandari tunaunganisha mikoa zaidi ya sita hakuna bandari ya maana Mwanza hili na lenyewe liangaliwe kwa maana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, juu ya ukusanyaji wa mapato. Nimuombe Waziri wa TAMISEMI, hakuna siku itakaa Halmashauri hizi ziweze kujitegemea asilimia 50 mpaka 100 maana yake ni kwamba uwezo huo ni mdogo sana lazima tujipange kukusanya mapato.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mabula muda wako umekwisha.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana naunga mkono hoja asilimia mia. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka!

MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Naibu Spika, jina langu kamili naitwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hotuba nzuri ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli. Naomba ili kule mbele ya safari nisije nikasahau kuunga hoja, kabla sijaanza kuchangia niseme naunga mkono hoja asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kutoa rai kwanza kwa ndugu zetu kwa Waandishi wa Habari haya wanayofanya ndugu zetu hawa wapinzani nilikuwa naona leo magazeti mengi yameandika kimenuka, na lugha kama hizo naomba waandike pia kwamba hawa wenzetu pamoja na kwamba kimenuka wanaondoka wakiwa wamesaini pesa za walipa kodi ili wananchi waweze kuwaelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia nisirudie ya wenzangu kwa sababu Mkoa wa Tabora tuna kitu ambacho ni *common interest* kama Kiwanda cha Tumbaku na wenzangu walishaongelea. Lakini naomba niongelee Kiwanda cha Nyuzi katika hotuba ambayo ni ya Mheshimiwa Rais. Kiwanda kile tulikwenda kukikagua na Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya kama mwezi mmoja umepita, Kiwanda cha Nyuzi Tabora sasa hivi ni *godown*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kubinafsishwa tulikwenda ili wakakifungue lakini tukaambiwa mimi na DC kwamba kiwanda kile funguo zake maana yake tuliambiwa kwamba ile mitambo ya mle ndani ilishauzwa kama vyuma chakavu, tukataka tushuhudie lakini tukaambiwa kwamba funguo

ziko India. Sasa kwamba mwekezaji kaondoka na funguo kwenda India hili ni jambo ambalo Mheshimiwa Mwijage, Waziri wa Viwanda na Biashara tuna tatizo hilo, kiwanda kile kimfungwa funguo ziko India. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kama Mbunge wa Tabora Mjini niweze kuongelea suala la hospitali yetu ya Mkoa ambayo ndiyo ya Rufaa ya Kitete. Pale kama alivyoainisha Mheshimiwa mmoja aliongelea suala la Kitete, hospitali ya Kitete ina changamoto nyingi na ndiyo hospitali tunayoitegemea kama ya rufaa. Kweli ina tatizo kubwa la wataalam, Madaktari Bingwa pale wanahitajika madaktari kama nane, nilitembelea ile hospitali kama mwezi mmoja pia umepita, niliongea na Mganga Mkuu, kuna Daktari Bingwa mmoja tu katika Madaktari Bingwa nane wanaohitajika katika hospitali. Lakini niliuliza kwani kuna changamoto gani, nikaambiwa suala ni kwamba hawapendi kukaa pale Tabora kwa sababu ya mazingira, nilimuuliza Mganga Mkuu unadhani ni mazingira gani akaniambia hawapendi kukaa Tabora kwa sababu kwanza maslahi ni kidogo, hawawezi pia kupata nafasi za kufanya kazi zile za ziada *part time* kama wanavyoweza kufanya Madaktari wengine wa Miji mikubwa kama Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya na Arusha. Kwa hiyo, ningeomba Wizara iweze kuangalia kwa makusudi ili kuweza kuboresha zile huduma lakini pia kuboresha maslahi ili hao wataalam watakapopatikana waweze kukaa kama hospitali yetu ya Kitete bila kuona kwamba wamesahauliwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna matatizo pia ya Wauguzi wako wachache sana hospitali yetu ya rufaa na wale wachache ambao wanafanya kazi, nichukue nafasi hii kuwapongeza kwamba wanafanya kazi katika mazingira ambayo maslahi siyo mazuri, lakini inapofika suala la muda wao wa ziada manesi wale wanafanya kazi nzuri Madokta lakini muda wao wa ziada amekuwa haupati pesa kutoka Serikalini kwa ajili ya kulipa zile *overtime*, kwa hiyo, hii inakatisha tamaa, naomba Wizara husika muweze kuliangalia jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye suala la maji nitakwenda haraka haraka kwa sababu ya muda, Tabora tuna bwawa la Igombe linatoa maji lakini tuna bwawa pia la Kazima ambalo sasa limejaa tope, lakini bado kuna maji ambayo yanaweza kutosha hata vijiji vya jirani au kata za jirani kama Manoleo, Itonjanda na Ifucha ambazo zinazunguka lile bwawa. Lakini bwawa lile limeachwa tu kiasi ambacho sasa halihudumii zile sehemu ambazo zina matatizo ya maji.

Mimi ningeishauri Serikali kwamba katika kipindi hiki ambacho bado tunasubiri maji ya Ziwa Victoria waweze kuchukua njia angalau kutoa lile tope, maji yale ni mengi kuliko tunajenga bwawa jipya, tuna bwawa jipya linajengwa sehemu za Inara, Kata ya Ndevelwa, bwawa lile hata maji ya safari hii lile bwawa lilikuwa linakamilika lakini sasa linavuja maji hayakai, na limegharimu

zaidi ya shilingi bilioni moja na kitu. Lakini Idara yetu ya maji pale TUWASA bili nyingi hazilipwi na hasa na taasisi za Serikali na ile TUWASA pale Tabora ni moja ya taasisi ambazo zinajitegemea hazipata ruzuku yoyote. Ile taasisi inadai zaidi ya shilngi bilioni 1.3 na wadeni wakubwa ni pamoja na taasisi za Serikali lakini pamoja na shule mbalimbali. Kwa hiyo, naomba Wizara ya Maji muweze kuliangalia hili kwamba tunafanyaje, kwa sababu sasa suala la maji limekuwa ni tatizo kubwa Tabora.

Lakini pia naomba niongelee suala la wenzetu hawa askari na hasa polisi kwa kweli hali za askari wetu hasa polisi kwenye kambi zao zile nyumba zao kwa kweli hata ukiziangalia hazilingani na Jeshi la Wananchi, JWTZ sasa hivi ukiangalia nyumba zao angalau zinavutia. Naomba Wizara inayohusika basi tuwakumbuke na ndugu zetu wa polisi kuwawekea mazingira mazuri wanapokaa pamoja na maslahi yao ili kuweza kufanya kazi zao kwa ufanisi.

Mwisho naomba niongelee kuhusu reli, wenzetu walishaongelea. Kuhusu reli kwanza kabla sijaongea kwa sababu sijajua kama nitafika huko mimi nina *interest*, tumeambiwa tu-*declare interest* kama unayo kwenye shirika. Mimi nimekuwa ni mfanyabiashara mmoja wa reli, lakini kuna kitu kimoja kinanishangaza kuhusu reli, kila siku ni Godegode. Kila tunaposikia treni haiendi ni Godegode, sasa pale Godegode kuna nini? Kama imewezekana kujenga daraja la Malagalasi kubwa kiasi kile, kila siku kambi ya reli ni Godegode, naomba Wizara husika tuangalie pale Godegode kuna nini, isije ikawa ni mradi…

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwakasaka muda wako umekwisha!

MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA: Ahsante naomba kuunga hoja mkono asilimia mia moja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Sawa, Mheshimiwa Neema Mgaya.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi tena ya kuweza kurudi ndani ya Bunge hili Tukufu. Lakini vilevile niwashukuru wapiga kura wangu akina mama wa Mkoa wa Njombe kwa kuniamini na kunichagua kuwa mwakilishi wao, ahsanteni sana akina mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza, Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuwa taa ya ulimwengu. Hivi sasa Mataifa mbalimbali yamekuwa yakimzungumzia kwa utendaji wake wa kazi mzuri. Gazeti la *New York Times* nchini Marekani limemzungumzia na kumwelezea vizuri katika suala zima la uadilifu na utekelezaji wa sera aliokuwanao tangu

alipokuwa Waziri kwa kipindi cha miaka 20. Pongezi sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna gazeti lingine nchini Uingereza linaitwa *London Times,* limeelezea jinsi wananchi wanavyomshauri Malkia Elizabeth kuwa siku ya yake ya kuzaliwa iwe siku ya usafi nchini Uingereza. Hii yote ni kwa sababu ya utendaji mzuri wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, ndiyo maana watu sasa hivi wanatamani ku-*copy* mambo yake. Hongera sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la elimu. Naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuweza kutukeleza ahadi yake katika suala zima la elimu, kwa maana ya kwamba ada kuanzia shule ya msingi hadi kidato cha nne imefutwa. Ni kweli sasa hivi wanafunzi wa shule ya msingi hadi kidato cha nne hawalipi ada tena. Vilevile ahadi yake ya kutoa vitabu kuanzia shule ya msingi mpaka kidato cha nne pia imetekelezeka. Hongera sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali na kuijulisha kwamba dhana hii ya kufutwa kwa ada bado haijaeleweka kwa wananchi. Hivyo basi, naishauri Serikali ishuke chini kwa wananchi ili iwaeleweshe vizuri dhana nzima ya elimu bure, kwa maana ya ufutwaji wa ada kutokea shule ya msingi mpaka kidato cha nne, lakini vilevile na Serikali kuchangia vitabu kuanzia shule ya msingi mpaka kidato cha nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la huduma ya afya. Nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipoendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais wangu kwa sababu hivi sasa tumeona ameweza kutatua kero mbalimbali katika Wizara ya Afya kwa muda mfupi sana aliokuwa madarakani. Kero kubwa ya *CT-Scan* katika hospitali ya Muhimbili imetekelezeka. Wananchi wanapata kipimo hiki cha *CT-Scan* ndani ya Hospitali ya Muhimbili ukilinganisha na zamani walikuwa wanaenda kupima kipimo hiki nje ya hospitali kwa gharama kubwa. Hongera sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tumeona uanzishwaji wa maduka ya madawa ya *MSD* ndani ya hospitali ya Muhimbili na kule Mwanza. Hivi sasa wananchi wa Jiji la Dar es Salaam ambao wanakwenda kupata matibabu pale Muhimbili na wananchi wa Jiji la Mwanza wanapata dawa kwa bei nafuu. Hongera sana Mheshimiwa Rais kwa kutekeleza hilo ndani ya muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeanza kuona mabadiliko ya wafanyakazi katika hospitali, lakini vilevile na vituo vya afya. Hii inapelekea zile ziara za kushtukiza katika hospitali hizi na vituo vya afya.

Rai yangu kwa Serikali, naomba sasa Serikali ishuke, iende kwenye mikoa mingine ili iweze kutatua kero ambazo zinawakabili wananchi wa mikoa mingine katika hospitali. Mfano kule kwetu Njombe, hospitali yetu ya Njombe sasa hivi imekuwa ni chakavu sana; haina dawa za kutosha, haina wahudumu wa kutosha wala hospitali hii haina vipimo, ukizingatia kwamba hospitali hii ya Njombe sasa hivi tunaitegemea kama hospitali ya Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Halmashauri ya Njombe Mji wanatibiwa pale, wananchi wa Halmashauri ya Wanging'ombe wote wanatibiwa pale. Namwomba Waziri, Dada yangu Mheshimiwa Ummy Mwalimu, tukitoka kwenye Bunge hapa mje kuona jinsi ilivyochakaa, dawa hakuna, hatuna Madaktari wa kutosha na vipimo hakuna. Nawaomba mje kuangalia changamoto hii ili muweze kututatulia, kwa sababu sisi mkoa wetu wa Njombe ni mkoa mpya, tunahitaji kupata, hospitali ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kumwomba Mheshimiwa Simbachawene kwamba katika mkoa wetu wa Njombe, tuna Wilaya mpya ya Wanging'ombe, Wilaya hii haina hospitali ya Serikali. Wananchi wa Wanging'ombe…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mgaya, muda wako umekwisha. Mheshimiwa Kiteto Koshuma, dakika tano, Mheshimiwa Edwin Sannda dakika tano, atamalizia Mheshimiwa Malembeka kutoka Zanzibar.

MHE. KITETO Z. KOSHUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa jina naitwa Kiteto Zawadi Koshuma, ni Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Mwanza.

Mheshimiwa Spka, kwanza kabisa, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, japokuwa muda ni mdogo lakini nitachangia kwa kiasi fulani. Kwanza naomba niwashukuru wanawake wa Mkoa wa Mwanza ambao wameweza kuniamini ili kuwawakilisha katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba niongelee kuhusiana na hotuba ya Rais ambayo ilikuwa nzuri sana na imeweza kugusa nyoyo za Watanzania na kuweza kuwaonyesha Watanzania kwamba Tanzania sasa tunaweza tukawa na matumaini na Tanzania yetu na tukaishi kwa amani na mategemeo makubwa sana kutoka katika nchi ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hotuba ya Mheshimiwa Rais kabla sijaendelea ili muda usije ukaniishia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuongelea kuhusiana na mama lishe kitu ambacho kilimgusa sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, alipowaongelea mama lishe alisema Serikali sasa imefikia wakati iwatambue pamoja na shughuli zao wanazofanya. Mama lishe wamekuwa wakidharaulika sana, kama ambavyo Wabunge wengine wametangulia kusema.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikazie kwamba Waziri husika wa TAMISEMI atusaidie kwa kuwasiliana na Halmashauri zinazohusika ili ziweze kuwashirikisha kuhusu ni maeneo gani ambayo ni rafiki kwao kuweza kufanya shughuli zao za mama lishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua mchango mkubwa ambao mama lishe wanao katika jamii yetu. Wengi wetu tunakula chakula kwa hawa mama lishe, lakini pia hawa mama lishe ambao wanatupatia chakula, wanajisaidia na wao kupata kipato, ambapo wanaweza wakatatua matatizo mbalimbali. Kama tunavyojua katika familia, mama pekee ndio mtu ambaye anajua kwamba watoto wamekula nini au baba amekula nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, naomba Serikali sasa ifikie hatua ya kuwatambua hawa mama lishe na kufahamu kazi ambazo wanazifanya kwamba zinachangia katika pato la Taifa na kukuza uchumi wa Taifa, hasa ukiangalia katika kauli mbiu ya Rais ambayo inasema Hapa Kazi Tu na sasa hivi ni kazi tu, hivyo tuwatambue hao mama lishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais pia aliguswa sana tatizo la bodaboda. Bodaboda ni vijana wetu ambao, badala ya kutangatanga na kuwaibia watu kwenye mifuko yao wameamua kujiajiri kwa kupitia pikipiki ili waweze kujipatia kipato na hatimaye kutatua matatizo yao. Bodaboda hawa wamekuwa wakipata matatizo ya kuhamishwa kwenye vituo vyao ambavyo wanapaki kwa ajili ya kupata abiria.

Naiomba Serikali yangu ambayo ni sikivu, Serikali ya Chama cha Mapinduzi, iwasikilize hawa watu wa bodaboda, wawawekee vituo ambavyo na wao pia kwao ni rafiki ambapo wanaweza kupata abiria. Hii ni kwa sababu, nimegundua katika Halmashauri nyingi wanapangiwa vituo ambavyo siyo rafiki kwao. Boda boda hupangiwa sehemu ambayo hawezi kupata abiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba sana Serikali yangu sikivu, itusaidie, mshuke kwenye Halmashauri ili muweze kuzishauri kwamba wanapotaka kuwapangia vituo hawa watu wa bodaboda, basi waweze kuwashirikisha ili wao pia wawepo katika kuchangia maamuzi kwamba ni wapi

tukae ili kuweza kupata abiria na hivyo basi kuweza kusaidia katika shughuli zao mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nichangie upande wa viwanda suala ambalo Mheshimiwa Rais amelipa kipaumbele sana. Suala hili kama ambavyo wengi wametangulia kusema kwamba bila viwanda Tanzania haitaweza kuendelea, lakini sasa viwanda hivi vitaendeleaje kama hatutaweza kuwashirikisha watu ambao tayari wanahusika na viwanda?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika Mkoa ninaotoka, Mkoa wa Mwanza ni Mkoa maarufu sana ambao samaki wa aina ya sato wanapatikana, lakini ni viwanda vichache sana ambavyo viko pale, kama vile *Vic Fish, TFP* na viwanda vingine lakini ni vichache sana.

Naiomba Serikali yangu inapokuwa inaleta mpango kazi wake, basi iangalie huu Mkoa wa Mwanza na kuufanya kuwa mkoa wenye viwanda. Kwa sababu gani nasema hivyo? Mwanza tunapata samaki…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. KITETO Z. KOSHUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie sentensi yangu. Pale Mwanza pia kuna Kiwanda cha Ngozi...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa muda tafadhali! *(Kicheko)*

MHE. KITETO Z. KOSHUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Edwin Sannda, una dakika tano. Mheshimiwa Malembeka ajiandae.

MHE. EDWIN M. SANNDA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa jina naitwa Edwin Sannda, wengi huwa wakisikia hili jina wanashtuka kidogo; lakini msishtuke, Sannda hii ni nzuri tu, siyo kama ile ya kuzikia. Ni Mbunge wa Jimbo la Kondoa Mjini. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nachukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwepo hapa, lakini pia nikishukuru chama changu kwa kupitisha jina hatimaye likaenda kupigiwa kura. Nawashukuru wadau wangu wote, familia, ndugu jamaa na marafiki na hatimaye wapiga kura wa Jimbo la Kondoa Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kwa moja napenda kuchangia kwenye hotuba ya Rais. Kwanza kabisa naipongeza; imekaa vizuri, imegusa nyanja zote, lakini pia nawapongeza kwa wale waliotupa Mpango wa miaka mitano wa Maendeleo, wameakisi moja kwa moja hotuba ya Rais, wamegusa kila nyanja, nawapongeza sana. Pia yule aliyewasilisha ule mpango ni pacha wangu, kwa hiyo naye nampongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nichangie pale kwa maana ya vitu vikubwa vinne. Mpango mzuri, lakini huwa tatizo letu linakwenda kwenye utekelezaji *(execution)*. Nawaomba hasa wale Wizara ya Fedha na Mipango na Serikali nzima kwa ujumla, suala la utekelezaji ndiyo liwe msingi mkubwa wa kuangalia *(execution)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, yameongelewa mengi sana kuhusiana na *government efficiency* na *effectiveness* (ufanisi wa Serikali), lakini kila tunapoongelea ufanisi wa Serikali, tunazungumzia kupunguza gharama na kubana matumizi. Napenda pale kwenye suala la *efficiency* ya Serikali tuongezee suala la *delivery time,* kukamilisha miradi, kufikisha huduma na yenyewe mwisho wa siku inaingia kwenye gharama. Tukiweza kufanikisha eneo hili napo tutakuwa tumefanya vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mbali na *delivery* pia suala la ubora. Tunatengeneza vitu, tunakamilisha miradi chini ya viwango, hatimaye tunahitaji kufanya marekebisho muda siyo mrefu, ambayo pia ni gharama tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwenye *government efficiency,* labda tungeangalia sehemu tatu, gharama inavyozungumziwa ya kwanza, *delivery time,* pamoja na *quality* ya huduma zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu cha tatu ningependa kuzungumzia suala la ubunifu kidogo. Kila mmoja aliyesimama kati yetu hapa anavutia kwake, tatizo liko hili, huduma zinahitajika hizi lakini mwisho wa siku ni lazima tujue ni namna gani tutatoka nje ya *box* tuwe wabunifu kuongeza kipato chetu. Tukiwa na kipato kikubwa kabisa kama nchi, ina maana hizi huduma zote zitafika, siyo tunagombea zile rasilimali chache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nafikiri, tujaribu kuangalia kama inawezekana, maana na sisi wenyewe ndio tunaotunga sheria, tukawekeza kwenye baadhi ya sekta. Hawa wawekezaji wakubwa wanaokuja au sekta ambazo tutaziona ni nzuri kabisa zitatuletea tija, mbali na kodi tunayopata, vyanzo vya kawaida vya mapato ya Serikali, lakini tuwe na hisa tuwekeze ili tuwe tunapata magawio yaongeze katika Pato zima la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri Wizara ya Fedha pamoja na nyingine, hebu tuangalie eneo hili, kama litahitaji sheria ya kubadilishwa au kutungwa, siyo kwamba tunaenda kufanya biashara *per se* lakini angalau tuwe na uwekezaji na sisi tuongeze vyanzo vya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ninalotaka kuongea ni suala la…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. EDWIN M. SANNDA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Malembeka.

MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Ninaitwa Angelina Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Kaskazini, Unguja.

Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufika hapa. Nashukuru Chama changu cha Mapinduzi na Jumuiya zake zote tatu kwa kazi nzuri iliyoifanya ya kufanya kampeni nchi nzima na kutuwezesha Wabunge wa Viti Maalum kuingia humu ndani, sambamba na Wabunge wa CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono kwa nguvu zangu zote hotuba ya Mheshimiwa Rais Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wamechangia mengi kuhusiana na michezo, wanahabari, elimu, afya, maji, reli, umeme, kilimo uvuvi, rushwa, barabara, utawala bora, biashara, ukusanyaji wa mapato na mengineyo yote nayaunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wangu katika hotuba ya Mheshimiwa Rais, napenda kuchangia ukurasa wa 35 *paragraph* ya pili na ukurasa wa 36 *paragraph* ya pili; kwa ridhaa yako naomba niyarudie maneno yale. Ukurasa wa 35, *paragraph* ya pili inasema; "Mheshimiwa Spika, tunaitwa Waheshimiwa kwa heshima ya dhamana tuliyopewa na Bunge hili Tukufu, tutunze heshima hiyo ili tuzidi kuheshimiwa." Mwisho wa kunukuu.

Ukurasa wa 36 unasema; "Mheshimiwa Spika, nimejitahidi kuzungumza kwa uchache, lakini napenda kukushukuru sana tena, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa viongozi wote, tuliokaribishwa kuingia katika ukumbi huu na kuhudhuria yaliyojitokeza na mmeona kuna kazi kubwa, kwa sababu bado kuna watoto wengi, mwendelee kuwavumilia na kuwafundisha na Watanzania wamewaona." Mwisho wa kunukuu na baada ya hapo kilifuata kicheko na makofi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ni maneno makali ambayo Mheshimiwa Rais ameongea kwa unyenyekevu mkubwa. Yale maneno ukiyaangalia kwa haraka unaona yanachekesha, lakini maneno hayo ni makali. Humu ndani hakuna watoto! Kuna watu wazima, Waheshimiwa Wabunge, wenye umri mkubwa na wenye busara; lakini kutokana na sababu za wachache humu ndani watu wote tunaonekana watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, humu ndani tumeshindwa kuonesha nidhamu kati ya Wabunge na Wabunge, tumeshindwa kuonesha nidhamu baina ya viongozi wetu wa nchi, tumeshindwa kuonesha nidhamu kwa viongozi wetu wa vyama, tumeshindwa kuonesha nidhamu baina ya Wabunge na viongozi wetu wa Bunge tuliowachagua, lakini pia tumeshindwa kuonesha nidhamu kwa wananchi waliotuchagua.

Mheshimiwa Naibu Spika, humu ndani wanasema siyo shwari. Mimi nasema humu ndani ni shwari, isipokuwa siyo shwari kwa wale wa upinzani. Wamekuwa wakilalamika kwamba Chama cha Mapinduzi tunakula pesa, tunamaliza hela ya Serikali, tunamaliza hela ya umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe utakuwa shahidi, wanakuja hapa, wanasaini, wanachukua hela ya wananchi, wanaondoka. Hivi ni nani alienda kuomba kura akisema naomba mnichague nikamzomee Rais? Ni nani alienda kuomba kura akasema, nipe kura yako niende nikamzomee Spika? Ni nani aliyeomba kura akasema, ninaomba kura yako niende nikamzomee Mwanasheria Mkuu wa Serikali? Ni nani aliyeomba kura akasema ninaomba kura yako ili niende nikawazomee Wabunge? Ni nani aliomba kura akasema naomba nichague ili nikisaini posho nitoke? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalidhalilisha Bunge! Tunakula pesa za wananchi bila sababu. Kama kweli wana uchungu wakae ndani ya ukumbi huu waongee, wachangie hoja, tuzijibu, tushindane kwa hoja, siyo kwa kuzomeana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme, wamekaa wanalalamika, Zanzibar siyo shwari. Mimi natoka Zanzibar, Kitope, Kichungwani, Mkoa wa Kaskazini Unguja, Jimbo la Mahonda. Sijatemewa mate, sijapigwa makofi na niko salama, isipokuwa wao kwao siyo shwari, ndiyo maana kutwa wanazomea.

Mheshimiwa Naibu Spika, humu ndani kuna watu wana heshima zao, watu wakubwa sana; tuna watoto wa Marais ambao wako humu ndani, wameingia kihalali kama Wabunge, hawezi kukubali baba zao wanatukanwa tunawaangalia. Kuna watu humu sisi ni shemeji zetu, wajomba zetu, watoto

wetu, wakwe zetu, wanatukana humu ndani tunawaangalia. Uvumilivu una mwisho wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siku zote huwa wanasema nyoka wa kijani haumi, mimi ninakuhakikishia siku akiuma hana dawa! *(Makofi/Kicheko)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikuhakikishie, kama mtu anasema hataki… *(Kicheko/Makofi/Kelele)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba ya Rais. *(Kicheko/Makofi/Vigelegele)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba tuendelee na ratiba.

Ratiba tuliyonayo sasa, Mawaziri kadhaa watatoa ufafanuzi wa hoja zilizojitokeza, lakini pia pale ambapo wanaona kulikuwa na maswali, watayajibu lakini hawataweza kujibu hoja zote, wala hawataweza kujibu maswali yote, lakini yale machache ambayo wanaona wanaweza kuyajibu leo, basi watayajibu; na haya wanayoyajibu leo hayakuondolei haki yako ya kuuliza maswali siku ambazo zinaendelea katika Kipindi cha Maswali na Majibu, lakini pia kuendelea kupeleka maswali kwa vipindi vinavyokuja.

Waheshimiwa Wabunge, nimelazimika kutoa ufafanuzi kidogo kuhusu upangaji wa majina ya wachangiaji. Wapo Wabunge ambao ni wazoefu humu lakini wapo pia Wabunge ambao ni wageni. Wabunge wazoefu wanajua wakikosa nafasi sasa wataipata tena baadaye, kwa sababu hiki ni kipindi tu kimojawapo cha vipindi vya Bunge au Mikutano ya Bunge. Kwa hiyo, kama hukupata fursa safari hii, utapata katika vikao vijavyo.

Pia unaweza kuwa hukupata fursa ya kuuliza swali; swali lako bado linafanyiwa kazi, wakishamaliza kulifanyia kazi, basi litakuja; ama mengine yatajibiwa kwa maandishi. Vilevile kama hukupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, hiki siyo kipindi pekee cha Maswali ya Nyongeza, viko vingi vinakuja, huko mbele utapata fursa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lingine ni kuhusu majina. Majina kwa kawaida ukishatangaza Bungeni kwamba sasa hoja imetolewa kila mtu anajaza na yote yanajazwa kwa wakati mmoja; kwa hiyo, Sekretarieti inachukua yale majina, inakwenda kuyaweka pamoja. Kwa hiyo, hutegemea jina lako limeangukia wapi. Hakuna kusema labda wewe umeonewa jina lako likawa la mwisho. Hakuna anayeonewa, ni majina yote yanakuja wakati mmoja na siku moja.

Kwa hiyo, inabidi yapangwe; na katika kupangwa unaweza ukajikuta uko sehemu ambayo hukufikiwa kuchangia.

Waheshimiwa Wabunge, hiki ni kipindi tu kimojawapo, vipindi vingi vinakuja na mtapata fursa na sekretarieti iko hapa inaangalia ni akina nani wameshapata fursa ya kuongea sasa. Kesho tunaendelea kujadili kuhusu mpango, utapata fursa. Kwa hiyo, kama hukupata kuchangia hotuba ya Rais, utapata fursa ya kuchangia Mpango ambao unaelezea yale ambayo yako kwenye hotuba ya Rais ya namna ya kuyafanya.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuyasema hayo, tutachukua muda kiasi kwa ajili ya kuwasikiliza Mawaziri halafu baadaye Waziri Mkuu ama mtu aliyetayarishwa kwa niaba yake atatoa hoja ya kufunga mjadala huu. Kwa kuanzia, tutaanza na Mheshimiwa Januari Makamba, yeye atatumia dakika 10, Mawaziri wengine wote watatumia dakika tano tano. Mheshimiwa Waziri Makamba!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa fursa hii. Naanza moja kwa moja kwa kutoa pongezi kwa hotuba nzuri aliyoitoa Rais wetu mpendwa, hotuba ambayo imetoa dira na mwelekeo wa Tanzania mpya. Kwa kauli ya hotuba ile na vitendo vilivyofuatia baada yake, tunaanza kuiona kabisa safari ya kupata Taifa jipya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, safari hii haitakuwa nyepesi, itakuwa ngumu, tutajaribiwa njiani, tutakejeliwa, tutakebehiwa, tutatiwa mashaka kuhusu mwenendo wetu, kuhusu mwelekeo wetu, lakini napenda kuwasihi Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwamba tumuunge mkono Mheshimiwa Rais. Unapotaka kutengeneza keki ya mayai au chapati za mayai ni lazima upasue mayai. *(Makofi)*

Mheshimwa Naibu Spika, zamani kulikuwa na dawa zimeandikwa *shake well before use,* lazima utikise ndipo unywe dawa, ndipo ifanye kazi. Kwa hiyo, mitikisiko hii inayotokea ni sehemu ya kujenga Taifa jipya na wala watu wasipate mashaka wala wasiwasi kwamba nchi yetu inaelekea katika mwelekeo ambao sio wenyewe. Tulifika mahali tulihitaji Rais wa aina hii na tumempata na tumuunge mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumze kuhusu Zanzibar. Uchaguzi ni mchakato wa kikatiba na ni mchakato wa kisheria. Wakati tulipoamua kuingia kwenye Mfumo wa Vyama Vingi, tulibadilisha Katiba yetu, tukatengeneza taasisi zitakazotusaidia kuendesha uchaguzi wa ushindani na sheria ambazo zitatusaidia kuendesha siasa ya ushindani.

Kwa upande wa Zanzibar, Katiba ya Zanzibar Ibara ya 119 iliweka Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ambayo ilipewa majukumu na mamlaka ya namna ya kufanya na ikapewa uhuru mkubwa. Vilevile ikatungwa Sheria Na. 11 ya mwaka 1984 na ikabadilishwa mara kadhaa ili kukidhi mahitaji ya siasa ya ushindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar Kifungu cha 5(a) kinasema kwamba; "Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ina jukumu la usimamizi wa jumla wa mwenendo wa uchaguzi." Maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba Tume imepewa nguvu na Mamlaka ya Kikatiba na Kisheria kufuta matokeo ya uchaguzi pale inapojiridhisha kwamba sababu na kasoro zilizojitokeza kwenye uchaguzi haziwezi kutoa matokeo yanayoakisi utashi wa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mamlaka ya Tume kuhusu kufuta uchaguzi wa Zanzibar hayana mashaka yoyote; hayana mashaka ndani ya Katiba, wala ndani ya sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ilitoa sababu nane za kufuta matokeo. Sababu mojawapo ikiwa ni malalamiko ya vyama vya siasa; ikiwa ni mgombea mmoja kujitangaza kwamba ameshinda ambapo ni kinyume kabisa na sheria, jambo ambalo lingeweza kupelekea machafuko na mtafaruku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ilikaa katika Mkutano wake wa tarehe 28 Oktoba, 2015 na kupitisha uamuzi wa kufuta matokeo yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Katiba ya Zanzibar upo utaratibu wa Tume kufanya maamuzi. Ibara ya 119(10), kwamba Tume itakapokaa maamuzi yake ni halali anapokuwepo Mwenyekiti au Makamu na wajumbe wengine wanne. Vilevile Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar inatamka kwamba kanuni, maelezo na matangazo yote ambayo Tume ina mamlaka ya kutunga au kutoa, yatahesabika kwamba yametungwa kisheria kama yamewekwa sahihi na Mwenyekiti wa Tume au Mkurugenzi wa Uchaguzi. *(Makofi)*

Tangazo lililotolewa na Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi wa Zanzibar kufuta matokeo kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar ni tangazo halali kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile baada ya hapo tangazo lile, kama invyohitajika kwenye Katiba, liliwekwa kwenye Gazeti la Serikali kama hati ya kisheria namba 130 kwenye *GN* Namba 6587 ya tarehe 6 Novemba, 2015. Kwa hiyo, mjadala wa mamlaka ya Tume ya Uchaguzi kuhusu kufuta matokeo yale haupaswi kuwepo kwa sababu mamlaka yale inayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 21 Januari , 2016 Tume iliamua na kutangaza tarehe ya kurudiwa kwa uchaguzi. Kama Katiba inavyoelekeza katika Ibara ya 119 (10) kwamba maamuzi ya Tume ili yafanyike, ni lazima akidi itimie na lazima wengi wakubaliane na uamuzi ule.

Katika kikao cha Tume cha tarehe 21 mwezi wa Kwanza cha kuamua kutangaza kurudiwa kwa uchaguzi, akidi ilitimia na wengi walikubaliana na uamuzi ule. Kwa hiyo, uamuzi ule ni halali kisheria na Kikatiba. Katiba ya Zanzibar inasema kwamba hakuna mwenye mamlaka, hata Mahakama ya kuhoji au kuchunguza maamuzi yanayotolewa na Tume kuhusu uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wote tunajua kwamba uamuzi ule ulikuwa halali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu lazima iendelee kuwa nchi ya amani, ni lazima iendelee kuwa nchi ya utulivu na msingi wa amani na utulivu ni kuheshimu Katiba na sheria ambazo tumezitunga sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine linalozungumzwa ni kwamba kama matokeo ya uchaguzi ulioendeshwa na Tume Zanzibar yamekubalika na kwamba kama tuna Wabunge kutoka Zanzibar humu, iweje basi uchaguzi wa Zanzibar uharibike na matokeo yafutwe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, chaguzi zile ni mbili tofauti, zimefanyika kwa Katiba mbili tofauti, Tume mbili tofauti, sheria mbili tofauti, madaftari mawili tofauti, utaratibu wa kuhesabu kura tofauti, wasimamizi tofauti, hata wino kuna wino wa *NEC* na wino wa *ZEC*. Kwa hiyo, haishangazi wala haistaajabishi kwamba uchaguzi mmoja ukaharibika mwingine ukawa halali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachounganisha chaguzi hizi mbili ni kitu kimoja tu ni kwamba zilifanyika siku moja, lakini chaguzi hizi ni tofauti. Hoja kwamba kama uchaguzi huu ulikwenda sawa na mwingine siyo sawa, haina mashiko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwasihi wenzetu ambao wameamua kutafuta suluhu hii kwa nje ya Katiba na nje ya sheria, wanakosea na kwamba hakuna miongoni mwetu ambaye ana uwezo wala mamlaka ya kuiamrisha Tume ifanye kingine nje ya Katiba na nje ya sheria. Viongozi wa nchi yetu akiwemo Rais wetu, wamefanya jitihada kubwa na za kutosha kuhakikisha kwamba nchi yetu inaendele kuwa ya amani na kwamba maamuzi haya ya Tume ambayo hatuna mamlaka nayo, hayapelekei katika vurugu na mtafaruku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wajibu wa kulinda amani na umoja wa nchi yetu ni wajibu wa viongozi wa kisiasa. Maamuzi ambayo viongozi wa kisiasa wa Zanzibar watayachukua, kama yatakuwa ni maamuzi ya kusababisha vurugu na fujo na mtafaruku, basi damu ya Watanzania itakuwa mikononi mwao.

Sisi kwa upande wa Chama cha Mapinduzi na kwa upande wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wajibu wetu ni kuhakikisha kwamba nchi yetu ianendelea kuwa ya amani, utulivu na usalama. Tunao wajibu wa kuheshimu maamuzi ya Tume na hicho ndicho tutakachofanya. Hatuna mamlaka ya kuiamrisha Tume ifanye vinginevyo kinyume na utaratibu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niliona niseme hayo. Yapo mengine yamezungumzwa yakiwemo masuala ya bomoa bomoa, tutayazungumza wakati wa michango ya kuchagia kwenye Mpango. Nashukuru sana kwa nafasi hii. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Tutamsikiliza Mheshimiwa George Simbachawene atafuatiwa na Mheshimiwa William Lukuvi.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE - WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kwanza kabisa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu mizuri ambayo kusema ukweli imezidi kuongezea yale ambayo Mheshimiwa Rais aliyasema siku ya hotuba yake. Kwa hiyo, tumeendelea kupata mambo mengi zaidi ambayo yatatusaidia kuyafanyia kazi. Mmesema mengi katika sekta ya afya, kilimo, mambo ya utawala, utumishi, ukusanyaji wa mapato na mambo mengi sana mmeyasema ambayo yanaangukia katika Wizara yangu ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuwahakikishia kwamba yote haya tunayafahamu. Tanzania mpya ya Magufuli inayokuja, ni ya watu kufanya kazi. Tunataka tuwahakikishie kwamba Mheshimiwa Rais anaendelea kuisuka Serikali na mtambue kwamba Serikali bado haijakamilika. Bado tunahitaji Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, lakini tutakwenda mbali zaidi; tunataka kusuka vizuri sana Wakurugenzi mpaka Wakuu wa Idara. Tunataka tuwachuje, wawe na *vetting* nzuri kabisa na siyo kuokotana tu. Tunataka Tanzania mpya, tukisema kuanzia juu Hapa Kazi Tu basi ni Hapa Kazi Tu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mengi yaliyosemwa hapa liko moja ambalo limejitokeza sana juu ya elimu bila malipo. Elimu bila malipo limesemwa na Wabunge wengi na ni kwa sababu halifahamiki. Serikali imeamua hata wakati bajeti haijafika, lakini kupitia kwenye wigo ule ule wa bajeti ya mwaka 2015/2016 kunyofoa katika utoaji wa huduma ya elimu, katika *vote* ya Wizara ya

TAMISEMI kuhakikisha kwamba tunapata shilingi bilioni 131.88 kwa ajili ya kuanza kutoa elimu bila malipo kwa watoto wetu wa kuanzia chekechea hadi kidato cha nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mwezi tumepanga kupeleka shilingi bilioni 18.777 ambazo zimegawanyika katika maeneo manne. Kwanza ni fedha kwa ajili ya mitihani ya kidato cha nneambayo Serikali italipa moja kwa moja Baraza la Mitihani. Kwa hiyo, watoto wote kuanzia darasa la nne, *form two,* lakini kidato cha nnewenyewe watalipiwa na Serikali. Pili, ni fedha kwa ajili ya fidia ya ada, badala ya ile ada ya shilingi 20,000/= na shilingi 70,000/= Serikali inalipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, fedha ya uendeshaji wa shule za msingi na sekondari, hizi zote Serikali italipa. Fedha kwa ajili ya chakula shilingi 1,500/= kwa kila mtoto wa shule maalum za msingi na kila mtoto wa shule za bweni za sekondari. Sasa kwa zile shule za bweni za sekondari, kwa zile shule za *hostels* ambazo zimejengwa na jamii hili limeleta mkanganganyiko kidogo, kwamba zile shule za bweni ambazo zimejengwa na jamii kupitia mipango yao wenyewe, kupitia wadau wengine wa maendeleo, hizi si *hostels* zinazotambulika na Serikali. Tunafahamu zipo, lakini siyo zile ambazo Serikali inapeleka fedha kwa ajili ya chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutambue kwamba shule hizo ni karibu shule 3,252 zenye watoto karibu 1,334,280, ni wengi sana. Kwa hiyo, huwezi ukakurupuka ukaja na mpango wa kuwalisha wale; tumeona tuanze na hawa wa bweni lakini baadaye kama itawezekana, tunaweza tukaenda huko, lakini siyo jambo ambalo sisi katika fungu hili la sasa, tumeliwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukue nafasi hii kuwaomba wadau, wazazi na Halmashauri husika maana ndiyo wadau muhimu katika mamlaka zile. Kama zilianzisha shule hizi za bweni, basi zijue utaratibu ziliokuwa zinautumia, ziendelee nao, lakini utaratibu huo sasa usiwe unatoka katika maagizo ya Wakuu wa Shule kuwaagiza wazazi wawalazimishe kuhakikisha kwamba watoto wao wana chakula, wanaleta bwenini. Sisi tumesema hizi shule siyo za bweni ni za kutwa. Kwa hiyo, tunaamini mtoto atakaa nyumbani na atakuja kusoma shuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kumekuwa kuna jitihada ya kuwafanya wakae shuleni, ni jitihada ya nyongeza tu na hivyo jukumu lile linabakia bado kwa utaratibu ule ule wa wazazi na wadau na pengine mamlaka zao zilizoamua ziwepo hizo shule, lakini siyo jukumu la Serikali kwa sasa mpaka hapo baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona nielezee hili kama sehemu ya jambo lililoletwa mkanganyiko mkubwa. Ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Geore Simbachawene. Namwita Mheshimiwa Wiliam Lukuvi, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake nzuri; na uzuri huu unajionesha pia kutokana na michango ya Waheshimiwa Wabunge na wananchi ambao sio Wabunge. Tunasoma kwenye magazeti, tunaona kila mtu amefurahia hotuba yake, lakini hata utendaji wa wa awali kabisa ya Serikali yake ya Awamu ya Tano. Kwa hiyo, nampongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Ismani kwa kunirudisha tena hapa Bungeni. Nataka kuwaahidi tu kwamba kama nilivyozoea nitawatumikia na nadhani bado wana imani na mimi nitaendelea na nafasi yangu ile ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi niliyopewa na Mheshimiwa Rais ni kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Nataka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba nimewasikiliza sana, yote yaliyosemwa mkifungua ukurasa wa 41 mpaka 46 mmezungumza katika maeneo hayo. Maeneo yote mliozungumza yako kwenye ilani, nataka kuwaahidi kwa sababu muda hautoshi, kwamba tunawawekea utaratibu wa kuyatekeleza katika miaka mitano hii. Kwa sababu tuko pamoja tumeshaunda na Kamati tutashirikiana katika kuhakikisha kwamba yote yaliyopangwa katika Ilani ya Uchaguzi wa Chama chetu yanatekelezwa katika kipindi hiki cha miaka mitano kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mambo ya muda mfupi ambayo tumeamua kuyafanya na juzi mliniuliza. Moja kubwa mmezungumza ni habari ya migogoro, hili ni jambo la muda mfupi, liko kwenye ilani lakini halitaji miaka mitano. Tumekubaliana na rafiki yangu hapa kwamba mtuandikie migogoro; najua kuna migogoro ya mipaka ya vijiji kama nilivyosema, mipaka kati ya vijiji na hifadhi mbalimbali za misitu, wanyama na nini, mipaka kati ya Wilaya na Mikoa. Tukishapata hiyo orodha tutapanga utaratibu. Yale yanayohusu Wizara yangu na Wizara ya Maliasili tutaunda timu ya pamoja na bila kumsahau mwenzetu mwenye ardhi, Serikali za Mitaa ili kuhakikisa kwamba tunapitia migogoro yote na kuipatia majibu. Kwa hiyo, ni jambo ambalo tutaanza nalo sasa, haliitaji bajeti kubwa, ni lazima tuondoe hii migogoro kwa sababu imedumu na imewatesa sana wananchi, hilo tutalifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Wizara yangu sasa hivi tunafanya *audit* ya ardhi. Wako watu tuliyowapa mashamba makubwa lakini hawayatumii vizuri, vilevile wapo watu tumewapa mashamba makubwa, wameweka rehani na bahati nzuri mtu yeyote akiweka rehani *mortgage,* mimi najua kwa sababu lazima *mortgage* zile zinasajiliwa kwangu. Wameweka matirilioni za fedha lakini tunataka kujua kwenye mashamba yao hizo trilioni za fedha wameweka?

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya mashamba ambayo nimeshayapitia nimegundua pamoja na mamilioni ya fedha waliyochukua, mashamba yao yako vilevile kama walivyoyachukua. Kwa hiyo, tunataka tujue hizi fedha wamepeleka wapi? Kwa hiyo, tunafanya *audit* kwa watu waliochukua mashamba makubwa kwa maana ya kwamba kama wameshindwa, sheria iko wazi, tutawanyang'anya, tutawapa wananchi wenye shida au tuawapa wawekezaji wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunataka tujue, wale walio *mortgage* fedha hizo wamepeleka wapi? Kwa sababu sasa iko tabia ya watu kuchua mashamba makubwa sana, tena watu wa aina fulani tu, wanachukua mashamba kila mahali, lakini hawawekezi, wala hawayatumii. Sasa wanachukua kama rehani ili wapate pesa, waende kujenga magorofa kigamboni kwa Mheshimiwa Ndugulile. Hiyo hatutakubali. Tunataka ukichukua fedha, lazima uwekeze katika mashamba yale yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hizi ni hatua za muda mfupi, kuondoa kero ya migogoro ya ardhi inayosababishwa na mipaka ambayo sisi watu wa Serikali tunaweza kufanya; lakini ya muda mrefu iko kwenye ilani. Lengo la Serikali katika Ilani ya Miaka Mitano ni kupima kila kipande cha ardhi. Tunaanza mpango huu mwezi ujao kwa Wilaya mbili ya Kilombero na Ulanga. Tunapima kila pande cha ardhi, lazima kiwe na mwenyewe na kumilikishwa kwa hati. Tunafanya Wilaya mbili za majaribio, Ulanga na Kilombero tunaanza mwezi ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo letu tungependa hatua kwa hatua ardhi yote ya Tanzania ipimwe na ikipendeza zaidi, kila mwananchi awe na fursa ya kumiliki ardhi yake kwa hati ili aweze kuitunza, lakini na Serikali iweze kupata mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, yako malengo ya muda mrefu. Nilitaka tu niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge mliosema mengi, tutatembea sana, tutawakuta huko huko, lakini nataka muwahakikishie wananchi kwamba ile migogoro mikubwa ambayo imewakera kwa muda mrefu, tutaisimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Profesa Ndalichako!

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi nichangie hoja hii iliyoko mble yetu.

Kwanza kabisa, napenda kuanza kutoa shukrani za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa John Joseph Pombe Magufuli kwa imani kubwa kabisa aliyoonyesha kwangu kwa kuniteua kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Tanzania na kuniteua kuwa Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Rais kwamba nitaifanya kazi aliyonipa kwa moyo wa dhati kabisa na nitawatumikia wananchi, Watanzania wenzangu katika sekta hii ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingi zimezungumzwa katika Wizara yangu, lakini kwa sababu ya muda nitazungumzia tu chache. Napenda kuanza kuzungumzia suala la elimu bila malipo ambalo mwenzangu wa TAMISEMI amelizungumzia, lakini ningependa kuongezea tu jambo dogo katika kutoa ufafanuzi kwa sababu umejitokeza mkanganyiko kwamba Serikali inabagua baadhi ya watoto; wengine wanapewa chakula na wengine hawapewi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu kusema kwamba usajili wa shule uko wa aina mbili na Wizara yangu ndiyo inayofanya usajili wa shule. Tuna shule za kutwa na shule za bweni. Shule za bweni zina vigezo vyake. Tunatambua kama alivyosema Waziri wa TAMISEMI kwamba kuna baadhi ya shule za kutwa ambazo zimewekewa *hostel* kwa sababu maalumu. Sasa zile haziko katika utaratibu wa sasa wa wanafunzi kupatiwa chakula kwa sababu usajili wake ni shule za kutwa na sio shule za bweni. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nami narudia kuwaomba Wakurugenzi wote wa Halmashauri, kama kuna shule ambayo ilisajiliwa kama shule ya kutwa lakini inakidhi vigezo; kwa sababu vigezo vipo ili shule iweze kuwa ya bweni. Ina vitu vingi ambavyo wanapaswa kuzingatia. Basi kama wamekidhi vile vigezo, waje Wizarani tuwabadilishie usajili. Ili waweze kupata chakula, lazima iwe ni shule ya bweni na siyo vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa shule ya kutwa kwa sababu inahesabika kwamba mwanafuni anakuja shuleni na kurudi nyumbani, kwa hiyo, lile jukumu la chakula bado ni jukumu la mzazi kwa sababu mwanafunzi anaishi nyumbani kwa mujibu wa usajili shule husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimeona hilo jambo pamoja na maelezo mazuri ambayo aliyasema, nizungumzie kwa sababu ni suala la kisera.

Kwa hiyo, shule iliyosajiliwa kama shule ya bweni inapata chakula, shule iliyosajiliwa kama ya kutwa katika mwongozo ambao tumeutoa mzazi ataendelea kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuzungumzia kidogo suala ambalo limejitokeza kuhusiana na malalamiko kwamba ada kubwa. Hii imejitokeza hata katika hotuba ya Mheshimiwa Rais kwamba mojawapo ya kero ni ada kubwa zinazotozwa na shule binafsi. Naomba tu niseme kwamba Wizara yangu tayari inalifanyia kazi suala hilo na tunajaribu kuja na ada elekezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba hili suala la ada elekezi linahitaji kufanyiwa kazi kwa kina na kuangalia vizuri shule zetu, kwa sababu shule ziko katika makundi mbalimbali. Unaweza kukuta zile huduma au *facilities* ambazo zinapatikana shuleni zinatofautiana sana. Kuna shule nyingine mpaka zina *swimming pool,* zimejengwa kwa terazo, nyingine zimejengwa kwa *tiles* au kwa *marble,* sasa unapokuwa unatoa ada elekezi, ni lazima pia uzingatie kwamba mwanafunzi anasoma katika aina gani ya shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo shule nyingine za binafsi ambazo hazina hata sakafu. Kwa hiyo, huwezi kuja na ada elekezi ukasema tu kwamba ni shilingi kadhaa. Ni lazima haya mambo yote uyaangalie. Hata chakula wanachopewa wanafunzi kinatofautiana. Baadhi ya shule wanapewa mpaka *sausage*, wanakula pilau na wengine wanakula ugali na maharage kila siku. Huwezi ukaja na ada elekezi ambayo ni *uniform. (Makofi)*

Kwa hiyo, Wizara yangu lazima iliangalie hili jambo kwa umakini mkubwa sana. Tutaangalia mpaka mishahara wanayolipwa walimu. Kuna baadhi ya shule zinawaonea walimu inawapa mishahara kidogo.

Kwa hiyo, naomba Watanzania tuwe na subira, Wizara yangu inalifanyia kazi hili jambo, lakini siyo jambo ambalo linahitaji kufanya kazi kwa haraka. Tutakapokuwa tayari, tutakuja kuwapa majibu. Tutakapokubaliana, kwa sababu tunafanya kwa kina na tuna mtaalam mshauri, tutaweka *class* za shule kwa vigezo mbalimbali ambavyo tutavitambua, basi tutakapokuwa tumekamilisha, naomba tukubaliane na hiyo ada. Nashukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Tutamsikia Mheshimiwa *Engineer* Lwenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwigulu Nchemba.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Awali ya yote naomba niwashukuru wananchi wa Wanging'ombe kwa kunipa kura nyingi sana nikawa Mbunge wa Bunge hili. Pia namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuniteua kuwa Waziri wa Maji na

Umwagiliaji. Naomba niwaahidi Watanzania pamoja na Mheshimiwa Rais kwamba nitaifanya kazi hii kwa bidii zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi kila aliyesimama hapa amezungumza tatizo la maji kwenye eneo lake. Sitaweza kuyajibu yote, lakini nitatoa bango kitita cha kuelezea utekelezaji wa awamu ya kwanza ya programu ya maji ambayo imegusa kila Halmashauri, kila Wilaya, kila Mkoa, mji Mkuu wa Mkoa, Mji wa Wilaya; ni miradi mingi sana.

Katika awamu ya kwanza tumekuwa na miradi 1,888 na miradi 1,200 imekamilika, bado miradi 700 na kitu inaendelea na iko kwenye hatua mbali mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niwashukuru Wabunge. Bunge lililopita mliidhinisha tuanzishe Mfuko wa Maji ambapo tuliamua kabisa kwamba tuanze kwa shilingi 50 ya lita ya mafuta, tukapata shilingi bilioni 90. Sasa naomba sana, tutakapoingia kwenye *Phase II* ya programu ambapo tumeainisha miradi mingi yenye thamani ya bilioni 3.3 *US Dollar* ambayo ni sawa sawa na trilioni sita, ndani ya miaka mitano, tutatimiza ahadi ya Mheshimiwa Rais aliyoiongelea kwenye hotuba yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo pia ni Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ambapo tunasema kwamba sasa imefika mahali tufikishe upatikanaji wa maji vijijini asilimia 85 na mijini asilimia 95. Katika miaka kumi ijayo tunataka tuseme asilimia 100 kwa vijijini na mjini lazima wapate maji, kulingana na programu ambayo tumeiandaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakapofika kwenye bajeti tunaomba sana Waheshimiwa Wabunge mtuunge mkono ili fedha za ndani ziweze kutekeleza jambo hili. Wafadhili wameshaahidi zaidi ya shilingi bilioni 1.4 kwamba watachangia kwenye hiyo shilingi bilioni 3.3 *Us Dollar*. Nusu tayari wameshaahidi. Kwa hiyo, ina maana kwamba Serikali lazima tutafute nusu nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ili kila mtu apate huo mradi wake, tunahitaji tupate mapato mengi ya ndani ili tuweze kutekeleza miradi hii. Kwa hiyo, naomba sana tutakapofikia mahali hapo, Waheshimiwa Wabunge, mtuunge mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme machache katika miradi ambayo inaendelea hivi sasa. Kwanza kulikuwa na mradi wa kutoa maji katika bomba la Kashwasa kupeleka Tabora - Igunga na Nzega pamoja na vijiji 89 vitakavyonufaika. Tumeshapata fedha kutoka Serikali ya India, sasa hivi tunatafuta mkandarasi, tunafanya kitu kinaitwa *pre-qualification*. Wataanza

kuleta *tender* zao. Tunategemea ikifika Julai, Mkandarasi atakuwa ameanza kazi ya kujenga mradi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na kilio cha wananchi wengi wanaoishi kando kando ya Ziwa ya Victoria kwamba maji yale yaweze kupatikana. Tayari tumeshaanza miradi mingi ya kutoa maji ndani ya Ziwa Victoria kupeleka kwenye miji yote inayozunguka Ziwa Victoria. Kwa hiyo, mradi unaendelea na kazi nyingi zitaanza kuanzia mwezi wa saba mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mradi pia wa kutoa maji kutoka Mto Ruvuma kupeleka Manispaa ya Mtwara na Mikindani. Tumeshakamilisha usanifu, bomba kubwa litajengwa kilometa 60 na vijiji karibu zaidi ya 29 ambavyo viko kando ya bomba lile vitapatiwa maji. Tunakamilisha mazungumzo na Serikali ya China kwa ajili ya kuweza kupata ufadhili pamoja na Serikali ili tuweze kukamilisha mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuna mradi mwingine ambao utaongeza upatikanaji wa maji katika Mji wa Dar es Salaam. Tumekuwa na kilio na ahadi kwa muda mrefu. Sasa tumefika mahali kwamba mradi ule wa upanuzi wa Ruvu Chini utakamilika mwezi wa pili; na upanuzi wa mradi wa Ruvu Juu utakamilika mwezi wa tatu. Kwa hiyo, tukifika mwezi wa tatu matanki yote ya maji ambayo tuliyajenga kwa muda mrefu, yatakuwa yameshajaa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi tunayoendeleanayo sasa ni kusambaza maji yawafikie wananchi, kwa sababu kwenye sera ya maji tunasema upatikanaji wa maji uwe mita 400 hasa kwa wananchi walioko vijijini. Kwa wale wanaokaa mijini, tunataka tuwaunganishie maji kwenye nyumba zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kazi hii inaendelea na kwenye programu hii nina hakika kabisa tutaanza na maeneo kama ya Kimara, Kibamba, Kiluvya, kwenda mpaka Mlandizi, maeneo yale yote tutayasambazia maji baada ya kupatika wingi wa maji ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa eneo hili la Temeke na maeneo mengine ya upande huu pili kama Mkuranga, tuna uchimbaji wa visima Kimbiji na Mpera. Tumeshakamilisha visima nane na sasa hivi tutaingia kwenye awamu ya pili ya kujenga miundombinu ili tuhakikishe kwamba tunapata maji ya kutosha kwa wananchi wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda; na kwa sababu nimesema nitaleta bango kitita kwa utekelezaji wa mambo yote haya, naomba tukubaliane kwa leo kwamba mtapata *report* na mtatusaidia katika kujenga hoja katika kufanya miradi maeneo mengine ambayo yamebaki. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, atafuatiwa na Mheshimiwa Charles Kitwanga na Mheshimiwa Angellah Kairuki, ajiandae.

WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nami nitoe shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Rais kwa kunipa fursa hii na kwa wananchi wangu kwa kunirejesha tena Bungeni tena kwa kura za kishindo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ajili ya muda, sitaenda kwa kina kati ya yale ambayo nilikuwa nimekusudia kuyasema kufuatana na mpango wa Wizara, lakini pia kufuatana na hoja zilizotolewa na Wabunge. Nitafanya hivyo wakati nitakapokuwa nachangia kwenye mpango tutakapojadili baada ya ajenda hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa leo niwaambie tu Waheshimiwa Wabunge, kama mnataka mali mtaipata shambani. Naawaambia Waheshimiwa, vijana wenzangu, wahitimu wa Vyuo pamoja na Watanzania kwa ujumla kama mnataka mali mtaipata shambani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka kumekuwa na wimbi kubwa la vijana kutoka vijijini kwenda mijini. Leo niwaambie, ni wakati wa vijana kutoka mijini kwenda vijijini. Huko ndiko utajiri uliko na huko ndiko mali iliko. Mashambani kuna ufugaji, kuna uvuvi na kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu katika miaka mitano ya Rais aliyepewa dhamana na Watanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kitakuwa ni kipindi cha kuweka mabadiliko katika sekta nzima ya kilimo na kuipa hadhi inayostahili ambayo kila wakati tumekuwa tukisema ndiyo uti wa mgongo na ndiyo inayotoa ajira kwa asilimia kubwa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wameongelea matatizo mengi. Moja, wameongelea upande wa wafugaji. Nitaenda kwa undani, lakini tunalopanga kama Wizara, tunapanga ni kuondoa utaratibu wa wafugaji kuzunguka na mifugo na hivyo kuleta ugomvi kati ya wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, namna ambavyo tunapanga kwenda kulifanya jambo hili, tunataka kufanya kama ambavyo katika Taifa kuna Ranchi zilizobainishwa miaka na miaka, kuna hifadhi ya mapori yaliyobainishwa miaka na miaka, tunakwenda kubainisha na maeneo ya wafugaji katika maeneo hayo tutakwenda kuweka miundombinu inayostahili ya mahitaji ya huduma za mifugo ili kuondoa tatizo la wafugaji kuzunguka zunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye jambo hili tunao uwezo wa kushirikiana hata na wafugaji wenyewe kuweka miundombinu, iwapo tu watakuwa wameambiwa kwamba hili ndilo eneo na wakagawiwa kama vitalu na kuweza kufanya shughuli hizo za kuweka miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua fedha wanazodaiwa bahati mbaya na baadhi ya watumishi ambao sio waaminifu, wakazitoa kwa namna ya rushwa, ni nyingi kuliko fedha ambazo zingeweza kutumika kuendeleza miundombinu na wafugaji wakawa katika eneo salama, la uhakika na ambalo hata lingeweza kutupa takwimu ambazo zingewezesha hata mwekezaji anayetaka kuwekeza kwenye maziwa akajua katika ukanda huu kuna mifugo ya aina hii na inaweza ikatoa maziwa kwa kiwango kile.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilivyo sasa ni ngumu sana kwa Mheshimiwa Mwijage kumshawishi mtu kuweka kiwanda cha maziwa kwa watu wanaohama kwa sababu haijulikani kama mpaka wiki ijayo watakuwa katika eneo hilo. Nitaenda kwa undani wake tutakapokuwa tunajadili Mpango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa pembejeo, Waheshimiwa Wabunge wameongea kwa uchungu sana. Na mimi katika kuzunguka katika kipindi kifupi, nimegundua utoaji wa pembejeo, ruzuku ambayo Serikali imekuwa ikitoa, uwianio wa fedha ambayo imetumika kwa takwimu na faida ambayo imetokana na utoaji wa ruzuku wa aina hiyo, haviendani.

Kwa hiyo, fedha imekuwa ikipotea kwa namna mbili; moja, ni kwa baadhi ya Maafisa pamoja na Mawakala wasio waaminifu kucheza *deal.* Wanapeleka mbegu, wanapeleka mbolea, wanapeleka mifuko ya kuonesha tu, baada ya hapo wanawapatia wananchi wengine ambao wameshapanda, wanawapatia kama ni 2,000 au 5,000, wanaondoka na mifuko ya mbolea na mifuko ya mbegu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara na Serikali kwa ujumla tunaangalia uwezekano wa kuwa na utaratibu mpya ambao utatoa majawabu ya kudumu ya tatizo hilo la upotevu wa ruzuku inayotelewa na Serikali. Tunaangalia uwezekano wa kuangalia kwenye makato, kwenye vitu vinavyosababisha bei ya mbolea inakuwa ya juu, tuweze kushughulika na bei hiyo na mbolea inayopatika iwe ya bei sawasawa na ya ruzuku na iweze kupatikana kwa wakulima wote badala ya wachache ambao wamekuwa wakilengwa kwa aina hii ya ruzuku. Nitalifafanua kwa kirefu wakati wa Mpango. *(Makofi)*

Jambo lingine ambalo ambalo Waheshimiwa Wabunge wameliongelea na lilimkera sana Mheshimiwa Rais wakati anazunguka na aliwaahidi Watanzania kwamba litafanyiwa kazi, ni jambo la makato mengi kwenye

mazao ya wakulima. Tutalifanyia kazi, na niwaahidi tutakapokuja kujadili Mpango, nitaleta hayo mapendekezo na hatua ambazo Wizara inapanga kuzichukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata wewe nikukumbushe, kama mnataka mali mtaipata shambani. Ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Sawa Mheshimiwa Mwigulu, nitakuja niombe kitalu na mimi. Mheshimiwa Charles Kitangwa! *(Makofi)*

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI: Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuniteua kuwa Waziri wa Mambo ya ndani. Nawashukuru sana wananchi wa Misungwi kwa kuendelea kuniamini na kupata asilimia themanini na kitu, haikuwa jambo dogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezitoa. Naanza tu kwa kusema, upande mmoja una haki lakini upande mwingine lazima kuwe na wajibu. Ukidai haki, timiza wajibu wako. Ndugu zetu kwa mfano, kama jana walikuwa wakidai haki, lakini hawakutimiza wajibu wao kwa kufanya fujo na ndiyo sababu Wizara yangu iko pale kuhakikisha kwamba nchi yetu inaendelea kuwa tulivu na salama. Hilo tutalifanya kwa nguvu zetu zote kwa sababu hatuwezi kufanya biashara, wala shughuli zozote katika mazingira ya ambayo hayana utulivu na siyo salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie mambo machache tu ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyazungumzia tukianzia na malalamiko mengi hasa *oparetion* ya bodaboda yaani ya pikipiki.

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na wananchi wote, mtakumbuka kwamba hivi karibuni limejitokeza wimbi kubwa la uhalifu unaosababishwa na watu wanaoendesha pikipiki. Kwa hiyo, hapa hatuzungumzii bodaboda peke yake, tunazungumzia pikipiki zote.

Kwa hiyo, *oparetion* tunayoifanya sasa hivi ni ya kujaribu kuhakiki na kuona kama pikipiki zote zinamilikiwa kihalali na watu gani na kuhakikisha kwamba kila mmoja anayepita katika eneo linalotakiwa, anapita kwa kufuata Sheria za Usalama Barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili ni jambo la usalama zaidi ili tuweze kuishi katika mazingira salama na wananchi wasiwe na wasiwasi, vilevile watu wote walio na pikipiki za kawaida au bodaboda wasiwe na wasiwasi, hili ni kwa nia njema na kuhakikisha kwamba nchi yetu inaendelea kuwa salama na tulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo limezungumziwa, ni la wakimbizi. Ni kweli wakimbizi kwa miaka ya nyuma walifikia kwenye 800,000, lakini walipungua sana na sasa hivi hali inaanza kurudia tena. Kwa sasa hivi tuna wakimbizi kwa mfano tuna Wakongo 63,000; tuna Warundi wapya ambao wameingia 124,000; tuna wakimbizi kama 199 wengine kutoka hata nchi kama Syria, lakini bado wanakuja kwetu, lakini tuna wakimbizi wengi tu, Warundi wapya ambao wamekuja tena sasa hivi ni 124,637.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kinachotupa nia ya kujipanga upya sasa hivi ni kwamba baadhi ya wakimbizi wanaokuja wametoka katika maeneo ya majeshi. Wanapofika katika maeneo ya wakimbizi wanaanza kufanya *recruitment* ya askari. Hili tumeliona na tumejipanga na tunahakikisha kwamba halitaendelea. Nchi yetu haiwezi kuwa chanzo cha askari wanaokwenda kufanya vurugu katika nchi za majirani zetu. Nihakikishe tu kama alivyosema Mheshimiwa Rais katika hotuba yake kwamba, wale watakaokuwa wanahitaji Uraia, utaratibu utafuatwa kulingana na sheria zetu na tutaweza kuwapatia uraia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo limezungumziwa na watu wengi, ni hili la maisha mazuri ya askari polisi wetu. Kitu cha kwanza wamezungumzia…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI: Kitu cha kwanza ambacho wamezungumzia ni nyumba. Niseme tu kwa sababu ya muda, kwamba tuna mpango wa kujenga nyumba mpya 3,500 kila mwaka kwa ajili ya polisi wetu. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kitwanga. Namwita Mheshimiwa Angellah Kairuki, atafuatiwa na Mheshimiwa Ummy Mwalimu, halafu atafuata Mheshimiwa Profesa Muhongo.

MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI - WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA): Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge wengine waliochangia hoja hii. Napenda kuchukua fursa hii kuchangia machache yaliyojitokeza katika hotuba ya Mheshimiwa Rais, lakini vile vile kwa michango ambayo Waheshimiwa Wabunge wameitoa kupitia hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba kwa ufinyu wa muda, nitajaribu kujibu masuala machache na nitajikita zaidi katika suala la

kupambana na rushwa, lakini vilevile katika masuala mazima ya Utumishi, hususan madeni mbalimbali ya watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kupitia TAKUKURU kwa namna ambavyo ameweza kuonesha utashi na kuonesha njia yake katika kupambana na tatizo la rushwa. Kupitia TAKUKURU, nimhakikishie Mheshimiwa Rais na wananchi wote wa Tanzania kwamba tutaunga mkono azma yake hii, tayari ameshatuonesha njia, kwa kweli ameipa TAKUKURU silaha iliyo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba kwa sisi TAKUKURU tutahakikisha hatutaacha jiwe lolote ambalo halitageuzwa. Yeyote atakayejishughulisha na vitendo vya rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma atachukuliwa hatua stahiki. Hatutaona haya, hatutamwonea aibu mtu yeyote atakaye jikita na vitendo hivi, hatutaangalia cheo cha mtumishi yeyote wa umma alichonacho Serikalini, ili mradi amejikita katika vitendo hivi viovu, basi atapata malipo yake stahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuliunga hili mkono, tumejaribu kushauriana na wenzetu wa TAMISEMI, kuangalia ni kwa namna gani sasa tunaweza kuziba mianya mbalimbali ya ubadhirifu wa fedha katika Halmashauri. Katika miaka mitano iliyopita, tayari tumeshachukua hatua na kesi mbalimbali zimefika Mahakamani. Watumishi takribani 6,794 wamefikishwa Mahakamani na wengine wamekuwa katika hatua mbalimbali za mashauri hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa tumepeleka Waratibu mbalimbali wa Kanda wa TAKUKURU ambao watakagua kila Mradi wa Maendeleo ili kihakikisha kwamba fedha inayokwenda katika miradi, basi ni fedha ile ambayo kweli imepangiwa matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa 2014/2015 kupitia Waratibu hawa wa Kanda wa TAKUKURU, tumeweza kuiokolea Serikali fedha takriban Shilingi bilioni saba. Kwa mwaka huu wa fedha tutajitahidi kuongoza kasi zaidi ili tuweze kuokoa fedha nyingi zaidi za miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu Waheshimiwa Wabunge na vilevile wananchi mbalimbali kwa ujumla wenye miradi ya maendeleo katika Halmashauri, waweze kutoa ushirikiano wa dhati kabisa kwa Waratibu hawa wa TAKUKURU wa Kanda, lakini pia kwa Ofisi nzima za TAKUKURU katika maeneo hayo ili tuweze kuchukua hatua stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nijikite sasa katika suala zima la Utumishi, hususan suala zima la madeni ya watumishi katika malimbikizo ya mishahara.

Tunatambua deni ni kubwa, lakini sisi kama Ofisi ya Rais Utumisi wa Umma tumejitahidi, tumeshalipa takriban shilingi bilioni 27.9 kwa walimu mbalimbali. Vilevile kwa mwaka huu wa fedha peke yake tumeshalipa takriban shilingi bilioni 7.9 ambayo ni malimbikizo ya mishahara kwa watumishi mbalimbali takriban 8,793.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaelewa mzigo walionao watumishi wa umma na niwahakikishie kwamba, mimi kama Waziri ninayesimamia masuala ya watumishi, lakini vile vile Mbunge wa Wafanyakazi, kwa kweli nitaangalia kwa kadri inavyowezekana kwa kushirikiana na Serikali yangu, kuona ni kwa namna gani sasa madeni haya yanapungua kama siyo kumalizika kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu kwa wenzangu watumishi, nyaraka mbalimbali za madai wanazowasilisha, basi ziwe ni nyaraka ambazo ni za kweli, nyaraka ambazo tutakapofanya uhakiki zisipoteze muda. Wapo watumishi ambao wamekuwa sio waaminifu. Unakuta kuna madai makubwa, baadaye tukifanya uhakiki, gharama inakuja kupungua. Vilevile kwa kufanya hivyo, unamcheleweshea yule ambaye anastahiki kulipwa malipo yake kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana ushirikiano wa watumishi wenzangu wa umma, tujitahidi tupeleke madai hayo kwa wakati, lakini vilevile kwa Halmashauri zetu, madai ambayo yanatakiwa kulipwa na Halmashauri zile, basi wayalipe kwa wakati na wasisababishe mzigo kwa watumishi wetu wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilijitokeza hoja mbalimbali kwa upungufu wa watumishi, niseme tu kwamba nakubaliana nao; lakini changamoto kubwa ambayo tunaipata kupitia Serikali, yako mahitaji makubwa kweli ya watumishi wa umma katika sekta mbalimbali, lakini ukiangalia hivi sasa *wage bill* yetu au malipo ambayo tunalipa kwenye mishahara ya watumishi wa umma ni takriban asilimia 51.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba kwa watumishi wa afya mwaka huu, 2016 tutaajiliri takribani watumishi 10,873, vile vile tutaajiri walimu 28,975 na watumishi kwa ujumla wa sekta ya umma watakuwa 71,496.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, mengine tutaongea wakati wa kuchangia Mpango. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ummy Mwalimu, ajiandae na Mheshimiwa, Profesa Muhongo atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Maghembe.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nakushukuru, lakini nianze na kukishukuru

Chama changu cha Mapinduzi na Wanawake wa UWT wa Mkoa wa Tanga kwa kunipa heshima hii ya kurudi tena katika Bunge hili.

Pia kwa heshima na unyenyekevu mkubwa, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa imani yake kubwa sana kwangu, namwahidi tutachapa kazi, kama kauli mbiu ya Serikali inavyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesikiliza michango, maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge na tunawashukuru wote ambao wamechangia katika eneo hili. Lengo ni kutaka kuboresha utoaji wa huduma za afya, lakini pia kuhakikisha tunajenga jamii ya Watanzania inayojali na kuheshimu usawa wa jinsia, haki za wanawake, haki za watoto na haki za wazee. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge na niwathibitishie katika hatua hii kwamba tutafanyia kazi maoni yenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, nitajikita katika masuala makuu mawili ambayo yameongelewa sana na Waheshimiwa Wabunge wote. Kama walivyosema wenzangu, wakati wa kuchangia Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Mpango wa Maendeleo wa 2016/2017 tutatoa mwelekeo wa vipaumbele vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala kubwa ambalo limechangiwa na Waheshimiwa Wabunge, lakini pia limejitokeza kwa sauti kubwa wakati wa Hotuba ya Mheshimiwa Rais ni suala la upatikanaji wa dawa katika vituo vya umma vya kutolea huduma za afya katika Zahanati, Vituo vya Afya, Hospitali za Wilaya na Hospitali za Rufaa za Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Bunge lako nataka kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwamba tumedhamiria kuhakikisha tunapunguza tatizo la ukosefu wa dawa katika hospitali zetu. Tayari tumeshaanza kuchukua hatua na kwa sasa hivi uwezo wetu wa kutoa dawa ni asilimia 70 na tunakusudia tufikie asilimia 95. Hii tutawezaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza dawa ambazo zinafika kwa wananchi, nyingi zinapotea mtaani katika mikono ambayo siyo salama. Kwa hiyo, kubwa ambalo tumelifanya na tutaendelea kulifanya ni kudhibiti upotevu wa dawa za Serikali na vifaa tiba. Sasa hivi tumeshaweka nembo katika dawa zote za Serikali ambazo ni muhimu. Asilimia 80 ya dawa za Serikali sasa hivi tayari zina nembo.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, tuendelee kuhamasisha wananchi wetu, watakapoona dawa ya Serikali ambayo ipo katika duka la dawa ambalo halistahili, watujulishe na wachukue hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo tumelifanya ni kuimarisha mfumo wa usambazaji, ununuzi na uhifadhi wa dawa. Hili ambalo tumelifanya

tumeshaagiza *MSD* kuhakikisha dawa hazishushwi katika kituo chohote cha afya cha Umma bila kuwepo kwa Kamati ya Afya ya Kituo husika.

Waheshimiwa Wabunge, sisi sote ni Madiwani, tuhakikishe Kamati za Afya za Zahanati, za Vitua vya Afya za Wilaya zinatimiza wajibu wao wa kuhakikisha tunadhibiti dawa na vifaa tiba vya Serikali.

Jambo lingine ambalo ningependa kulisisitiza, mpango wetu wa muda mrefu ni kuhakikisha tunanunua dawa kutoka kwa wazalishaji, badala ya kununua dawa kutoka kwa wafanyabiashara na hili linawezekana sana. Kauli mbiu ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kwamba tunabana matumizi. Kwa hiyo, tunaamini tutakaponunua dawa kutoka kwa wazalishaji, tutaweza kupata dawa nyingi, lakini pia kwa bei nafuu na hivyo kuweza kutatua tatizo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hili, tutaongeza bajeti ya kununua dawa, vifaa na vifaa tiba. Waheshimiwa Wabunge, wameongelea suala la ukosefu wa *X-Ray*, *Ultra-Sound*, *CT-Scan* na *MRI*. Tayari tumeshachukua hatua, sasa hivi Muhimbili hamna shida tena katika vifaa hivyo vikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao mpango pale Wizarani wa kuhakikisha katika kila Hospitali ya Rufaa ya Mkoa tunaiwezesha katika eneo zima la uchunguzi, maana yake, ni vifaa vyote ambavyo vinahitajika katika kufanya uchunguzi. Tayari tumeshapeleka mapendekezo yetu kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, tuone ni jinsi gani tutaweza kusonga mbele.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, duh!

Meshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni suala la miundombinu. Nikuhakikishie kwamba tutafanya kazi na wenzetu wa TAMISEMI kuhakikisha kwamba tunajenga zahanati katika kila kijiji, vituo vya afya katika kila Kata na Hospitali za Wilaya. Niwaambie Waheshimiwa Wabunge, hili kwa kweli, sisi la kwetu itakuwa tu ni kuweka vibali. Kwa hiyo, wale Wabunge wote ambao wamejenga vituo vya afya...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ummy, tafadhali weka nukta!

WAZIRI WA AFYA MAENDELEO YA JAMII JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize kwa kusema, kama mwanamke, afya ya mama na mtoto ni kipaumbele cha Serikali ya Awamu ya Tano. Tutahakikisha

tunapunguza vifo vya wanawake wajawazito na watoto chini ya miaka mitano. Hilo ni la kipaumbele, tutaongea kwenye Mpango wa Maendeleo. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Profesa Muhongo!

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mheshimiwa Rais kuwa na imani na mimi. Vilevile ndugu zangu wa Jimbo la Musoma Vijijini ambao waliamua niwe mwakilishi wao mzuri, tumeanza kujenga uchumi kwa kasi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais ni agizo na Wizara ya Nishati na Madini imeanza kutekeleza kwa vitendo. Niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango mizuri na wengi ambao wamechangia watakubaliana name kwamba wengine nimeanza kutatua kero zao. Kwa hiyo, wengi wanaomba umeme. Nawathibitishia Watanzania kwamba unakuja umeme mwingi, wa uhakika na wa bei nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wachimbaji wadogo wanatafuta maeneo, na watapewa na vilevile ruzuku itaendelea kupatikana. Tulianza na dola 50,000, tumefika dola 100,000 na tunataka tupate wachimbaji wadogo wanaoweza hata kufika kwenye ruzuku ya dola 1,000,000 au 5,000,000 hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, agizo la Mheshimiwa Rais, ni suala la kuondoa umaskini ambao unaendana na kujenga uchumi imara. Ni lazima uchumi wetu ukue kwa zaidi ya asilimia 10 na kufanya hivyo ni kila Mtanzania atumie umeme mwingi, aliyepo shambani na aliyeko kwenye viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hivi wastani wa matumizi ya umeme wetu, kila mtu hapa, hata tuliokaa humu ni *unit* 9 kwa mwezi. Kazi niliyopewa ni kuwatoa kwenye *unit* 9 kwa mwezi, kwenda kwenye *unit* 250 kwa mwezi. Hiyo ndiyo inayoitwa nchi ya kipato cha kati. Tukifanya hivyo, uchumi utakua kwa zaidi ya asilimia10 kutoka asilimia 7 za sasa hivi. Tukiendelea na asilimia 7 na asilimia 8 umasikini hautatoka.

Kwa hiyo, Wizara ya Nishati na Madini inataka ilete umeme mwingi. Tuna vijiji 15,809; asilimia 33 tu ya vijiji hivi ndiyo vyenye umeme. Kwa miaka miwili inayokuja, ni lazima tufike angalau asilimia angalau 67, theluthi mbili ya vijiji hivyo vipate umeme. Sasa hivi ni asilimia 40 ya Watanzania wote wanaopata umeme. Tukitaka kuingia nchi ya kipato cha kati, ikifika mwaka 2025 angalau asilimia 75 ya Watanzania na ikifika mwaka 2030 kwa sababu Tanzania ndiyo iliwakilisha Afrika kwenye mambo ya nishati duniani, ni lazima tuwe zaidi ya asilimia 90 ya Watanzania wanaotumia umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tutafanyaje sasa? Ni kutumia ni vyanzo vyote vya umeme ambavyo tunavyo. Kwa sasa hivi gesi ni karibu

asilimia 50, maji asilimia 35 na umeme wa mafuta karibu asilimia 15. Ni lazima tuachane na umeme wa mafuta, uwe umekaa pale kama tahadhari yetu tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tutazalisha umeme mwingi kutokana na gesi asilia, makaa ya mawe na maji. Halafu ndiyo tunakuja nishati jadidifu yaani jua, upepo na mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kwasababu hesabu hizi lazima ziendane na muda. Leo hii Watanzania tuko milioni 53.5; tutakavyokuwa tunapiga kura mwaka 2020 tutakuwa karibu milioni 65; na tutakapofika mwaka 2025, tukiwa nchi isiyokuwa na maskini na mtu anaamua anachotaka kula, kama mimi napenda muhogo basi tutakuwa karibu watu milioni 80 na uchumi hapa ndugu yangu inabidi Pato la Taifa liwe zaidi ya shilingi bilioni 240 mwaka 2025. Kwa hiyo, niwahakikishie Watanzania umeme wa uhakikia ni lazima. Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Namwita Profesa Maghembe, ajiandae Dkt. Mwakyembe atafuatiwa na Mheshimiwa Charles Mwijage.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na ninapenda kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa hotuba nzuri iliyotoa malengo thabiti ambayo yamenukuliwa duniani kote kama hotuba ya mfano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuniamini na kunipa dhamana ya kuiongoza Sekta ya Maliasili na Utalii. Wasemaji wengi wameeleza changamoto zilizopo katika sekta hii, lakini kwanza nilikuwa nataka niwahakikishie ndugu zangu kwamba Sekta ya Maliasili ukiondoa misitu inachangia uchumi wetu kwa asilimia 17, lakini ukiongeza misitu mchango wake unafika asilimia 23 ya uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchango huo, sekta hii ndiyo ya kwanza kutupatia fedha za kigeni kwa kuchangia asilimia 25 ya fedha zote za kigeni.

Pamoja na mchango huu, sekta hii ndiyo inahakikisha tunapata maji, inahakikisha mvua zinakuwa za kuaminika, inahakikisha tunapata watalii wengi sana kutoka maeneo yote duniani. Sekta hii pamoja na changamoto zilizopo, ina ubora katika nchi yetu kuliko nchi zote za Kiafrika, na ni ya pili duniani kote ukiacha Brazil kwa ubora dunia nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hiyo ni muhimu tupambane sana na changamoto ambazo zinaikabili; ya kwanza ikiwa ujangili. Hili tunapambana nalo kwa kuwafanyia utafiti majangili. Hivi sasa wamebadilisha sana njia zao za

kuwaua wanyama ambao wanawahitaji katika mapori yetu. Tembo wanauawa kwa kupewa sumu na wanyama wengine wanapewa sumu tena kwa aina ambayo kwa kweli ni ya kusikitisha sana. Na sisi tunabadilisha mwendo wetu wa kushughulika nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tunafanya majaribio ya ndege ambazo hazina marubani, kwanza kuhakikisha kwamba zinaondoa migogoro kati ya wananchi wenye mashamba na mapori ya akiba na mapori tengefu, lakini pia kuhakikisha kwamba tunaona shughuli za binadamu pamoja na majangili katika maeneo ambayo yana maliasili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumechukua hatua pia ya kuongeza wafanyakazi ambao wanashughulikia ulinzi wa wanyamapori kutoka askari 1,506 mwaka 2014 na sasa wamefikia askari 2,064. Aidha, tumeongeza vitendea kazi kwa sehemu kubwa sana na tumelitengeneza Shirika la *Tower* ambalo kazi yake itakuwa kulinda maliasili zetu kwa karibu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ni kubwa sana na Waheshimiwa Wabunge mmelisema kwa uchungu mkubwa ni uharibifu unaofanywa na wanyamapori katika mashamba na katika maeneo tunakoishi. Tutashirikiana na Wizara ya Ardhi, Wizara ya Mazingira na Wizara ya Kilimo na Mifugo ili kuhakikisha kwamba migogoro hii inaondoka mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

Aidha, tunachukua hatua mbalimbali za kuhakikisha kwamba mapato yetu kutoka kwenye maliasili zetu yanaongezeka. Kuacha sasa, wizi ule mdogo mdogo unaotendeka ndani, malengo yetu ni kuongeza watalii kutoka 1,100,000 hivi sasa na kufika 3,000,000 mwisho wa mwaka 2018 tukilenga kwamba utalii sasa utupatie asilimia 40 ya mapato yote ya Taifa letu. Ndugu zangu naomba tulinde maliasili zetu. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Dkt. Mwakyembe!

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naanza kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuniamini kuwa mmoja wa wasaidizi wake. Vilevile natumia fursa hii kuwapongeza sana wapigakura wa Kyela kwa uamuzi wao wa busara wa kubaki njia kuu, kwa sababu madhara ya michepuko yanaonekana wazi, viti vitupu hapa! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wamarekani wanasema hotuba ya Mmarekani mwenzao mmoja mweusi, Martin Luther King Junior aliyoitoa mwaka 1963, ndiyo hotuba bora kupita zote katika historia ya Taifa hilo ya miaka 229. Hiyo hotuba ilimgusa kila Mmarekani anayeipenda nchi yake. Na mimi naweza kudiriki kusema, ukiachia hotuba za Mwasisi wa Taifa hili, Baba wa Taifa Mwalimu Julius

Kambarage Nyerere, hotuba aliyoitoa Rais wetu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alipokuwa anazindua Bunge hili tarehe 20 Novemba, nayo ni hotuba bora kupita zote iliyogusa mioyo ya Watanzania wote wenye nia njema na nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba yenyewe ukiiangalia ni fupi tu, ina aya 160. Nimejaribu kufanya utundu tu hapa kuangalia, maana imerekodiwa kama *Hansard*. Rais wetu alipigiwa makofi na vigelegele mara 137 yaani ni zaidi ya 86! Nilipokuwa najaribu ku-*check history,* Martin Luther King Junior, alipigiwa vigelegele mara ngapi; ilikuwa kama asilimia 75. Kwa hiyo, imevunja rekodi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii imewaweka mahali pabaya sana wenzetu wa upinzani waliozoea kupinga kila kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la hotuba hii, ukijaribu kuipinga, wananchi huko nje wanakuona wa hovyo. Ndiyo maana wakaona watafute kisingizio cha hoja tu ya *TBC,* Waingereza wanasema ni *red hearing*, unatafuta hiyo ili usiwepo kwenye mjadala, maana ukiwepo, utasifia tu hii hotuba! Ndiyo shida hiyo! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawahakikishia Watanzania, hatujavunja sheria yoyote, Madaraka, Mamlaka ya Bunge, Kanuni za Bunge, hatujavunja. Mmoja alisema tumevunja Katiba ya Ibara ya 18. Sasa mimi ni Mwanasheria, Mwanakatiba. Ibara ya 18(d) inasema nini? "Kila mtu anayo haki kupewa taarifa." Sawa, tunakubali. Inasema, "wakati wote." Siyo wakati tu UKAWA wanapoongea ndipo kuna haki ya kupewa taarifa, *no*. Ni wakati wote! Ndiyo maana Waziri wetu wa Habari hapa ameipeleka kwenye *prime time*, usiku, Watanzania wengi waone. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri sisi Bunge tuna wajibu kuomba radhi Watanzania kwa fedha yao walipa kodi tunavyoichezea hapa. Tunatakiwa tufanye kazi, siyo mchezo mchezo huu! Hii radhi ya mdomo sasa hivi kwa kweli imepitwa na wakati! Naomba nisome Ibara ya 23; sisi ndio watunga sheria ni lazima tuonyeshe mfano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 23 (1) inasema, "Kila mtu bila kuwepo ubaguzi wa aina yoyote, anayo haki ya kupata ujira unaolingana na kazi yake." Kama umekuja tu hapa kufanya fujo, hujapata pesa kihalali unayolipwa posho. Inabidi kiti chako sasa kiamue, watu ambao wamekuja hapa kufanya mzaha, wasivunje Katiba ya nchi. Huku ni kuvunja Katiba ya nchi, nakuomba sana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kusema tu kwamba kuna watu wameongelea kuhusu vitu viwili hapa ambavyo vingine nitaviongelea wakati wa Mpango. Kuna suala la Mahakama Maalum ya Mafisadi. Naomba niwahakikishie Watanzania, Kiongozi wa Serikali wa awamu ya tano akitoa tamko, akitoa agizo, hilo lazima litekelezwe. Kwa hiyo, hivi sasa tumefikia hatua nzuri, tutawatangazia Watanzania kuhusu suala hilo ambalo amelitamka Mheshimiwa Rais na sisi tunalitekeleza. Hilo lazima waelewe. *(Makofi)*

Mheshimwia Naibu Spika, la pili, kuna wengine wamegusia kuhusu suala la Katiba Mpya, sasa sijui niseme nini zaidi ya kuwakumbusha Watanzania kwamba kwanza Watanzania wakumbuke, Rais wetu hajakaa mwaka mzima kama Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni mwezi wa pili tu na siku 23, hawezi kuyafanya yote katika kipindi cha miezi miwili na siku 23. Maana wengine wanamwangalia hata Waziri Mkuu hapa, inakuwa kama amekaa miezi tisa. Jamani ni miezi miwili tu na siku 23. Tuwaombee kwa Mungu, tuwasaidie kuweza kutimiza malengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alisema kwenye hotuba hii, "nimeachiwa kiporo, nitakitekeleza." Hivi jamani leo hii tuanze kusema, kwanini asianze hiyo? Sasa ukianza hayo…

(Hapa kengele ililiia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Aah, kakengele nako haka! Basi tutakuja huko baadaye tutamalizia mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tutamsikiliza Mheshimiwa Charles Mwijage.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Awali ya yote, nachukua fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza wananchi wa Wilaya ya Muleba Kaskazini, Jimbo la Muleba Kaskazini kwa kunichagua, lakini zaidi namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuwa na imani na mimi kunikabidhi Sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Sekta ambayo ndiyo inabeba kazi kubwa ya sehemu ya kwanza ya Awamu ya Tano ya Serikali yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhima ya sehemu ya kwanza ya Awamu ya Tano ni kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya uchumi na maendeleo ya watu. Ndiyo kazi ambayo tumepewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama walivyochangia Waheshimiwa Wabunge, viwanda vitajengeka, lakini nani atajenga? Wabunge tuna nafasi ya mbele, kila Mtanzania ana jukumu na injini kubwa ya kujenga viwanda ni sekta binafsi.

Niwahakikishie, Serikali ya Mheshimiwa Rais amesema itaweka mazingira bora na hiyo ni moja ya kazi ambayo amenikabidhi mimi. Ukisoma taarifa ya *Doing Business 2016,* Tanzania tumewekwa mahali pabaya, hali siyo nzuri. Bado njoo kesho zipo. Hiyo ni kazi ambayo nitaisimamia na mimi ni tarishi mkuu. Nitatembea Wizara zote, Idara zote, kuhakikisha kwamba wafanyabiashara, wawekezaji, wenye viwanda, wanatendewa sawa na kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tunakwenda kwenye viwanda? Kwa nini tunatoka kwenye uchumi wa uchuuzi? Sifa moja kubwa, viwanda vinatoa ajira kubwa sana. Tuna matatizo na vijana kwa sababu hatuwapatii ajira na Mheshimiwa Rais ameshatoa maelekezo. Nimepewa *matrix* mezani kwangu, nimeambiwa kila Mkoa kiwanda gani kiende; kila siku natafua wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna maeneo matatu tunayolenga; kuna viwanda vilivyopo sasa nchini, tutahakikisha vinafanya kazi na nitaondoa vikwazo vyote kama tarishi mkuu. Vile vile kuna wawekezaji wa ndani na nje wanaotaka kuwekeza, mimi ni mtumishi wenu, nitahakikisha nawatendea zaidi mnavyopenda ili muweze kuwekeza ili kutengeneza ajira nyingi, lakini nisiwafiche, muweze kuchangia kwa kutulipa kodi ili tuweze kupata maendeleo ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namba tatu, kuna suala ambalo Mheshimiwa Rais amelizungumza kwenye hotuba yake kuhusu viwanda vilivyobinafsishwa. Kuna watu wanasema Mwijage ametoa maelekezo miezi sita sijui wafanye nini. Siyo miezi sita, amri ilishatolewa ya *Treasury Registrar,* wote mliopewa viwanda mwende mjisalimishe, ueleze hicho kiwanda unakifanyia nini. Niwaeleze, watu wasiwe na mtazamo hasi, siyo kweli kwamba viwanda vyetu vinafanya vibaya, hapana!

Mheshimiwa Naibu Spika, *Breweries* ilibinafsishwa, inalipa shilingi bilioni 400 kwa mwaka kama ushuru. *Mbeya Cement* inalipa shilingi bilioni 38 kwa miaka mitano, inafanya vizuri, inakwenda kuzalisha tani milioni moja ifikapo mwisho wa mwaka; na mwezi ujao nakwenda kufungua kinu kipya cha kuongeza usalishaji. *Twiga Cement* inafanya vizuri, lakini *Moro Polister* ilikuwa inazalisha kilometa 16 za urefu wa nguo leo inazalisha kilometa 60. Fikiria kilometa 60 ya nguo. Kwa

hiyo, tusiangalie upande hasi na upande chanya upo. Aidha, kuna mazingira yasiyokuwa sawia kwa wawekezaji wa ndani, wanazidiwa na vitu vinavyotoka nje. Nitahakikisha kwamba mnatendewa haki ili tuweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema Tanzania halitakuwa dampo la taka, *substandard products* hazitaingia nchini na nitasimamia. Nimemwambia *Manager* wa *TBS* ukae *standby* mimi na wewe tunafanya kazi sahani moja. Ndugu zangu tutahakikisha vipyeo vinakuwa sawia. Mtu analeta mzigo umejaa kwenye meli, anasema nimeleta nusu, amharibie kazi Mzee Mpango. Nitakusaidia kufanya kazi hiyo Mzee Mpango, kwa sababu ndiyo kazi niliyoanzanayo. *(Makofi)*

Mtu analeta *finishing product* anasema siyo *finished product* kusudi ampige magoli Mzee Mpango. Mjukuu wangu nitahakikisha mambo yanakuendea vizuri, kwa sababu hiyo ndiyo kazi ya taaluma yangu. Tutahakikisha uwanja wa ushindani upo sawa kusudi watu wafanye biashara. Watanzania wengi wameshindwa kufanya biashara kwa sababu uwanja wa ushindani haukuwa sawia.

Kwa hiyo, ndugu zangu Watanzania nitawaletea *matrix,* yule anayejua nini faida ya kwao ya kiwanda, aje aniambie. Shemeji yangu nikwambie, usiwe na wasiwasi, kiwanda cha mbolea kinajengwa Mtwara na wawekezaji wanagombania Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwatoe mashaka, watu wanaosema Bagamoyo isijengwe Bandari, Bagamoyo siyo Bandari, ni *Bagamoyo Special Economic Zone*. Ni zaidi ya Bandari! Kuna mji unajengwa Bandari *square kilometer* 100. Nimekwenda pale na nimewaagiza, Bandari mtengeneze kitu kinaitwa *wet port* kusudi meli zitakazokwenda kuvua, zikija zing'oe pale Bagamoyo tuweze kufanya vitu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia zaidi kwenye Mpango. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa kanuni ya 28(5) nitaisoma, inasema, "Iwapo shughuli zilizopangwa kwa siku hiyo zimemalizika kabla ya saa moja na dakika arobaini na tano, Spika ataliahirisha Bunge bila kuhoji. Lakini iwapo zimesalia dakika kumi kabla ya kufikia muda wa kuahirisha kikao na Bunge au Kamati ya Bunge zima au Kamati ya Matumizi bado haijamaliza shughuli zake, Spika anaweza kuongeza muda usiozidi dakika thelathini bila kulihoji Bunge au Kamati ya Bunge Zima au Kamati ya Matumizi ili kukamilisha shughuli zilizobaki."

Waheshimiwa Wabunge, naongeza dakika thelathini ili kuweza kumalizia shughuli zilizobaki. *(Makofi)*

Tutaendelea na Mheshimiwa Jenista, tutamaliza na Mheshimiwa Mpango kabla hatujamkaribisha Mheshimiwa Waziri Mkuu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU): Mheshimiwa Naibu Spika, nami naanza kwa kushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nachukua nafasi hii pia kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kunipa kazi ya kumsaidia na hasa kumsadia Waziri Mkuu ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Naomba nimhakikishie nitakuwa mtumishi mwema.

Vilevile nawashukuru pia wapigakura wa Jimbo la Peramiho, nawaambia Hapa ni Kazi Tu, wasibabaishwe na kelele za mpangaji wakati sisi wenye nyumba tupo, tunaendelea kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu Mheshimiwa Rais wetu ametupa kazi kadhaa za kufanya. Naomba nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu na hasa kwa kuonyesha kwa vitendo anajali makundi maalum na hasa ya walemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wetu amelidhihirisha hilo kwa matendo. Chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu Mheshimiwa Rais amemteua Naibu Waziri anayeonyesha kama ni kielelezo cha watu wenye ulemavu katika nchi yetu ya Tanzania wanaweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kwanza kuwapongeza Wabunge wote kutoka katika kundi hilo na Watanzania wote kutoka katika kundi hilo ambao wameonyesha umahiri mkubwa katika kutoa mchango wao kwenye maendeleo ya Taifa letu bila kusita na kuonyesha kwamba kundi hili ni kundi muhimu katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2010 tumetunga Sheria Na.1 ya kuhakikisha kwamba tunakwenda kusimama katika maneno ya Mkataba wa Kimataifa ambao unatoa haki za binadamu na hasa kwa kundi la watu wenye ulemavu. Mkataba huo tuliuridhia mwaka 2008, mwaka 2010 tumetunga sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia hotuba ya Rais inatukumbusha, watu wenye ulemevu wana haki sawa na Watanzania wote. Kwa niaba ya Serikali na kwa maagizo ya hotuba ya Rais, tutakwenda kusimamia wapate haki sawa kwenye elimu, wapate haki sawa kwenye afya, wapate haki sawa kwenye ajira, wapate haki sawa kwenye masuala yote ya uchumi. Hiyo ni kazi tumepewa katika hotuba hii ya Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka kuondoa kila dhana ya unyanyapaa. Kumekuwa na tabia imezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge kwamba wapo watoto wenye ulemavu wanafungiwa na hata jamii zetu zimekuwa zikiwachukulia watoto wenye ulemavu, kwa mfano wenzetu wenye ulemavu wa u-*albino* wafungiwe mahali fulani kwa ajili ya ulinzi na usalama. Katika mipango tulionayo sasa, tumeanza kuona ni namna gani watu hawa walindwe lakini watolewe nje wakawe na wao ni *part* ya jamii ya Watanzania katika kuleta maendeleo na kupatiwa maendeleo endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi nyingine kubwa ambayo tumepewa pamoja na kusimamia sera, maafa na mambo mengine yote, matatizo ya dawa za kulevya na UKIMWI, naomba niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge kwamba kazi hiyo tunaifanya sawia. Tutapambana na dawa za kulevya, hakuna kurudi nyuma, tutaendelea kupambana na ugonjwa wa UKIMWI hakuna kurudi nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bunge lililopita tulishatunga sheria, tutazisimamia na ole wao watakaoendeleza biashara ya dawa za kulevya, sheria ile itafanya kazi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepewa kazi nyingine kubwa ya kuhakikisha kwamba tunaongeza ajira katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, katika hotuba yake ametuagiza, katika kuhakikisha Watanzania wanaondokana na tatizo la ajira mpango huu wa kuwezesha sekta ya viwanda, ifanye kazi ya kutosha kati ya Wizara yetu lakini na Wizara ya Viwanda na Biashara kuhakikisha huu mpango wa sekta kubwa ya viwanda vidogo, vya kati na viwanda vikubwa, iweze kuchukua asilimia 40 ya nguvu kazi ya Taifa. Waheshimiwa Wabunge, tutafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaendelea kuimarisha mifuko tuliyonayo sasa. Waheshimiwa Wabunge mmesema vijana wetu wanamaliza vyuo, hawana mikopo, vijana wana uwezo wa kuongeza stadi walizonazo ili kuchangia pato la Taifa na kujiajiri, wanashindwa kupata uwezo wa kufanya hivyo. Tumejipanga kuimarisha mifuko hiyo, iwape vijana wetu mikopo yenye riba nafuu na Waheshimiwa Wabunge tunaendelea kuwasiliana, tutaleta mipango hapa Bungeni muiunge mkono, tunataka kuonyesha mwaka 2020 haya yanawezakana; na tuwawezeshe vijana wetu kuweza kuajiriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutatekeleza mikakati mingine ambayo tayari iko ndani ya Wizara, kwa mfano kukuza ajira kwa vitendo na tutashirikiana na Halmashauri zetu kuhakikisha tunafanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Tutakapopata muda, tutatoa maelezo ya kina. Nachukua nafasi hii kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais na ninampongeza sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Mpango umewekwa wa mwisho kwa sababu maalum. Nadhani unaelewa sababu maalum, maana yote yaliyosemwa hapa, yanakuhusu.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza na mimi napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu kwa heshima na dhamana kubwa ambayo amenipatia ya kuwatumikia Watanzania katika nafasi ya Waziri wa Fedha na Mipango. Napenda kumuahidi na kupitia Bunge hili kuwaahidi Watanzania wote kwamba nitaitumikia nchi yangu kwa uwezo wangu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisikiliza hotuba ya Mheshimiwa Rais, nimeisoma na naomba kwanza niseme mambo matano kwa faida ya Watanzania ambao hawajaisoma hii hotuba na wengine pengine hawakuisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kwamba Tanzania mpya itajengwa na sisi Watanzania wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kila Mtanzania ni lazima afanye kazi kwa bidii na kujituma *(selflessness)* na hili ndilo linatuwezesha kugeuza maisha ya dhiki kuwa kama Mbinguni, yaani *change of hell into paradise,* lakini ni lazima tujitume, tutoke jasho ili kukuza uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, rushwa, ufisadi, ubadhirifu na matumizi mabaya ya mali na rasilimali zote za umma ni lazima tuvipige vita kwa nguvu zetu zote bila kuoneana haya. Kwa nafasi ambayo Mheshimiwa Rais amenitunukia, ni lazima mapato ya ndani ya kodi na yasiyo ya kodi, ni lazima yakusanywe kikamilifu kwa mujibu wa sheria. Hatutawachekea wakwepa kodi wala watumishi wa Mamlaka ya Ukusanyaji Mapato *(TRA),* wala Wizara na Idara za Serikali zinazokusanya maduhuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwetu sisi kama Wizara ya Fedha na Mipango, hawa ni nyoka, ni sawa na kucheza na *cobra*. Hatutakubali, tunawathamini sana wafanyabiashara wakubwa kwa wadogo, lakini watii Sheria za Kodi na sheria nyingine za nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la nne, ni lazima kuwa na hofu ya Mungu katika kuwatumikia wananchi. Ni lazima tuwe na uchungu na maisha duni ya Watanzania walio wengi vijijini na mijini. Hawa hawana uhakika wa chakula,

wanakula mchunga ndiyo mboga yao bila fursa ya kuchagua; wanakunywa maji yasiyo salama, watoto wao wanakaa chini shuleni na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la tano, amani na mshikamano katika nchi yetu, hii ni nguzo kuu ya maendeleo na ni lazima ilindwe kwa nguvu zote. Hivyo ni lazima kuzuia na kuzima ninachoita *chaos of democracy* kama tukio la jana na leo asubuhi hapa Bungeni. *This is true costly to our country and we cannot afford it. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nisemee hoja mbili, tatu, nyingine nitazieleza kwa ufasaha zaidi wakati tunajadili Mpango kuanzia kesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa reli mpya ya kati kwa kiwango cha *standard gauge,* natambua Watanzania wana kiu kubwa sana ya kuwa na reli ya kisasa, lakini ni ukweli pia kwamba haitawezekana kujenga reli hiyo kwa Bajeti ya Serikali. Inakadiriwa ujenzi wa reli hiyo utagharimu kati ya dola za Kimarekani bilioni sita mpaka saba ambayo ni sawa na shilingi za Kitanzania trilioni 13.15 mpaka trilioni 15. Ni fedha nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Ununuzi wa Umma, niwataarifu kwamba Wizara iko katika hatua ya mwisho wa kuandaa marekebisho ya sheria hiyo na tutaileta *for first reading* nafasi ikipatikana ndani ya Mkutano huu wa Bunge. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Sekunde thelathini, malizia!

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, nawaomba Watanzania wote wamuunge mkono kwa vitendo vya dhati Mheshimiwa Rais wetu na viongozi wasaidizi wake waandamizi kujenga Tanzania mpya. Tunaiunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa asilimia 200 na tunawaahidi Watanzania usimamizi mahiri kwa bajeti ya Serikali na maendeleo ya uchumi wa Taifa letu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu uhitimishe hoja. *(Makofi)*

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote namimi niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumshukuru Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hotuba yake nzuri

aliyoitoa wakati wa akizindua Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 20 Novemba, 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina shaka kuwa majadiliano ya hotuba hiyo hapa Bungeni yamedhihirisha umakini wa namna Waheshimiwa Wabunge walivyoielewa hotuba ile na umakini uliotumika katika kutayarisha na uwasilishaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Spika na wewe Mheshimiwa Naibu Spika kwa jinsi ambavyo mmesimamia mjadala huu. Aidha, kwa pekee kabisa, nampongeza Mheshimiwa Mtemi Andrew Chenge ambaye alipata fursa ya kusimamia mjadala wa hotuba hii ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nachukua nafasi hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia mjadala huu wa hotuba hii ya Mheshimiwa Rais. Aidha, nawashukuru kwa kuunga mkono maeneo mbalimbali yaliyobainishwa katika hotuba hiyo. Kitendo cha kuunga mkono kimeipa Serikali nguvu ya kutekeleza ushauri wa michango mizuri iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwadhihirishia kwamba michango ya Waheshimiwa Wabunge yote kwa ujumla itasaidia sana Serikali kutekeleza ufanisi zaidi, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 mwaka 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, itasaidia kutekeleza pia Mpango wa Miaka Mitano, kutoka mwaka 2016/2017 kwenda mwaka wa fedha 2020/2021 na Dira ya Maendeleo ya mwaka 2025. Jumla ya Waheshimiwa Wabunge 171 wamechangia mjadala huu, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhitimisha hoja hii, siyo nia yangu kujadili tena hoja moja baada ya nyingine kama ilivyotolewa wakati wa Waheshimiwa Wabunge wakichangia hotuba ya Mheshimiwa Rais, bali nitajielekeza katika ujumla wake. Aidha, Waheshimiwa Mawaziri tayari wameshatoa maelezo ya maeneo muhimu na ambayo yanayotakiwa kuzingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya awamu ya tano imeweka msisitizo katika kuhakikisha inarejesha nidhamu katika Utumishi wa Umma kwa kuweka mkazo katika misingi ya uadilifu, uwajibikaji, kutoa huduma kwa wakati na kuchukua hatua za haraka dhidi ya watumishi wote wanaokwenda kinyume na misingi ya utendaji kazi Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa Serikali ya awamu ya tano kwa kuzingatia falsafa ya Hapa Kazi Tu, ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, itaendelea kuhakikisha kwamba inawakumbusha kuwa kila Mtanzania anatumia muda wake katika kufanya kazi zaidi na kila Mtendaji Serikalini anatimiza wajibu wake na pia Serikali itahakikisha inachukua hatua dhidi ya wote watakaokiuka maadili ya kazi na sheria zilizowekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusisitiza kuwa kila mtumishi mahali popote alipo ni lazima atimize wajibu wake ipasavyo. Tunataka kujenga utumishi wa umma wenye kuzingatia uadilifu unaowajibika na watumishi wanaofanya kazi kwa bidii na maalifa na kamwe hatutavumilia mtumishi mzembe na anayefanya kazi kwa mazoea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa mjadala wa hotuba ya Mheshimiwa Rais, zipo hoja zilitolewa na Waheshimiwa Wabunge ambazo utekelezaji wake utahitaji kufanya maandilizi ya kutenga Bajeti ya Serikali. Baadhi ya maeneo hayo ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya barabara, mawasiliano, uchukuzi, ikiwemo bandari pamoja na miundombinu ya usambazaji wa maji na nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ipo miradi mbalimbali inayoendelea kutekelezwa nchini katika sekta za uzalishaji mali ikiwemo kilimo, mifugo, maliasili, madini na kadhalika na sekta za huduma ya jamii, kama vile elimu na afya ambayo inahitaji pia kukamilishwa wakati huu sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa Serikali itajitahidi kupanga vipaumbele vyake vya Mpango na Bajeti kwa kuzingatia ahadi za Mheshimiwa Rais kuanzia mwaka huu wa fedha na kuendelea. Maoni na hoja za Wabunge zitazingatiwa wakati wowote wa utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa zaidi ni kuomba ushirikiano wa wananchi wote ili utekelezaji uwe wa ufanisi na tija. Ili kutimiza azma ya kutekeleza miradi yote hiyo, Serikali itahakikisha inasimamia ukusanyaji wa mapato yake ipasavyo ili kuwahudumia Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sekta ya kilimo, Waheshimiwa Wabunge wameeleza changamoto nyingi zinazowakabili wakulima ikiwemo kupatikana kwa pembejeo, uchelewaji wake wa kuwafikia pia wakulima wetu. Tatizo la ununuzi wa mazao hasa tumbaku, pamba, kahawa na korosho na huduma chini ya Stakabadhi Ghalani, Serikali imepokea ushauri wa Wabunge na utazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia fursa hii kueleza kuwa kutokana na baadhi ya maeneo katika nchi yetu kukumbwa na uhaba wa chakula, uliotokana na aidha uzalishaji hafifu katika msimu uliopita ama kutokana na mazao ya vyakula kusombwa na mafuriko, Serikali inaendelea kutumia akiba yake ya chakula kuhakikisha kwamba waathirika wote wanapata chakula.

Nachukua fursa hii kuwataka Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kusimamia kikamilifu ugawaji wa chakula hicho ili kuwafikia walengwa bila ya upendeleo na bila ya kuchepusha na kukipeleka mahali pengine. Aidha, chakula hicho kigawanywe hadharani ili kuondoa malalamiko ya wananchi ili kuhakikisha walengwa wa chakula cha msaada wanafikiwa na kuhudumiwa pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, viongozi wakuu na watendaji wa Serikali katika ngazi zote, watoke maofisini kwenda vijijini ili kuhakikisha kwamba kila mwananchi anajishughulisha na shughuli za kilimo kwa lengo la kuzalisha chakula zaidi kwa ajili ya matumizi ya msimu ujao. Wakulima katika maeneo yaliyopata mafuriko wapatiwe mbegu za mazao yanayokomaa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usambazaji wa pembejeo, Halmashauri zote zihakikishe kuwa pembejeo zinafika mapema katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za masika na zipelekwe kwa walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili limesisitizwa vizuri na Waziri wa Kilimo lakini pia Serikali itaendelea kuangalia mfumo bora wa kusambaza pembejeo hizo za ruzuku ili kuondoa malalamiko ya wakulima. Halmashauri na Wizara ya Kilimo wakae kuondoa tozo za ushuru zenye kero kwa mazao yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la maji ni changamoto ya nchi nzima. Ili kuboresha huduma ya maji Serikali itajitahidi sana kutumia mbinu zake zikiwemo kuvuna na kuhifadhi maji ya mvua ili yatumike wakati wa kiangazi. Aidha, Serikali imepanga kuhakikisha kwamba fedha kwa ajili ya miradi ya maji ambayo haijakamilika, zinapatikana na kutumwa kwa wakati katika maeneo husika. *(Makofi)*

Vilevile Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa wakandarasi wanaopewa kazi za kujenga miradi ya maji, wana uwezo wa kutosha ili miradi hiyo iwe na ubora unaotakiwa na itaendelea kulipa madeni ya wakandarasi na wataalam washauri kama ambavyo imeelekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo yanayoikabili sekta ya maliasili na utalii yakiwepo ya ujangili wa wanyamapori na nyara, migogoro ya mipaka kati ya vijiji na hifadhi na upotevu wa mapato yanayoshughulikiwa kwa wakati ili kuifanya Serikali hii muhimu kuchangia katika uchumi wa Taifa na kuhifadhi

rasilimali hii kwa ajili ya kizazi kijacho. Ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge wote utazingatiwa na wadau wote pia ili kuhakikisha wanyamapori hususan tembo na faru hawaendelei kuuawa na majangili.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala haya ya uvuvi yataimarishwa kwa kuwatafutia wananchi na wadau wa sekta ya uvuvi nchini na kuhakikisha kwamba wanapatiwa vifaa vya kisasa vya uvuvi; kuwatafutia masoko na kuongeza kasi ya uwekezaji katika viwanda vya mazao ya samaki hususan katika ukanda wa bahari kuu na maziwa makuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufanya uvuvi katika maeneo ya bahari, maziwa na mito unakua endelevu, usimamizi na doria utafanyika kwa nguvu zote ili kukabiliana na uvuvi haramu. Serikali pia itaendelea kuhimiza wananchi kuanzisha ufugaji wa nyuki kwa kutumia mizinga ya kisasa, lakini pia Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na Halmashauri zote nchini ili kuhakikisha wananchi wanapata mizinga ya kisasa kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tuzingatie sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi kwa mtazamo wa kibiashara zaidi na viwanda kwa lengo la kuwa na viwanda vya kisasa vya kuongeza thamani ya mazao yake. Mkazo utakuwa katika kuanzisha viwanda ambavyo sehemu kubwa ya malighafi itatoka ndani hususan kwenye sekta za kilimo, mifugo, uvuvi, madini na maliasili nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na migogoro ya ardhi nchini; na malalamiko katika maeneo mengi nchini yanahusu matumizi ya ardhi. Maeneo ambayo yamekuwa yakilalamikiwa ni kati ya wakulima na wafugaji, wananchi kuhodhi maeneo makubwa bila ya kuyaendeleza, mipango miji na ujenzi katika maeneo ya wazi. Serikali imepokea michango mbalimbali ya Wabunge na namna bora ya kumaliza migogoro hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwahakikishia kwamba Serikali kupitia michango yenu itasimamia utekelezaji wa ushauri wenu ili tupate kupunguza migogoro iliyopo. Wizara zinazohusika zitashirikiana na wadau wa sekta ya ardhi nchini ili kubaini vyanzo vya migogoro hiyo na kuipatia ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali inayo dhamira ya dhati kuona migogoro hii inakwesha. Wito wangu ni kuwa watumiaji wote nchini lazima waheshimu sheria, kanuni na taratibu zilizopo kwenye matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nimeona nielezee haya kwa kifupi kama njia ya kuwaomba sana Waheshimiwa Wabunge wote na wale wenzangu wa upinzani ambao kwa hulka yao waliamua kufanya waliyofanya, lengo letu sote ni kujenga nchi yetu na kuleta maendeleo ya nchi yetu. Tunalo jukumu la kufanya kama wadau ikiwemo Serikali. Sisi kama Wabunge na

wananchi wote, tuna wajibu wa kuishauri Serikali jukumu letu ni kuwaongoza wananchi na kutekeleza yaliyomo katika hotuba ya Mheshimiwa Rais. Nawaomba sana Wabunge wenzangu wa vyama vyote vya siasa na wananchi wote nchini, kutambua wajibu wetu na kwa umoja wetu, kujenga nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna sababu na wala siyo busara kubeza juhudi za kila mmoja wetu ambazo zinasaidia sana kujenga nchi yetu. Nawaomba tuunge mkono na tuungane pamoja katika juhudi za kuwaendeleza wananchi na maendeleo yao. Michango yetu na mawazo yenu ndani na nje ya Bunge ndiyo kielelezo chetu kama Wabunge wenye mtazamo wa mbele kwa Watanzania waliotupatia dhamana ya kuwaongoza na kwamba tutatekeleza wajibu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayoyafanya hapa Bungeni yawe yanalenga maslahi ya Taifa. Hivyo basi, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge hasa wenzangu wa Kambi ya Upinzani kwamba tunalo jukumu la kufanya jambo ambalo tumepewa deni na wapigakura wetu waliotuchagua, tujitahidi sana kuondoa tofauti zetu kwa maslahi ya Watanzania.

Aidha, sisi wote ni Watanzania, hivyo hatuna budi kufanya juhudi za dhati kudumisha upendo, amani, mshikamano na kusaidiana kwa masilahi ya Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wote, baada ya kusema hayo, namshukuru tena Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa kunipa nafasi hii ili kusema hayo ambayo nimeyasema kufuatia michango iliyotokana na hotuba ya Mheshimiwa Rais. Kupitia hotuba hii, nimeridhishwa na michango yenu na sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WALEMAVU): Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa kipindi hiki cha mchana kwa siku ya leo. Sasa naahirisha Bunge mpaka kesho siku ya Ijumaa, tarehe 29, saa 3.00 asubuhi.

Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Bunge, tafadhali utatupa taarifa kesho kuhusu Kivuko kama tulivyotoa ahadi.

(Saa 2.00 usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,
Tarehe 29 Januari, 2016 Saa Tatu Asubuhi)